**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

## Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 9 Juni, 2015

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

## DUA

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua*

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 78

### Utangazaji wa Vituo vipya vya Daladala

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu namba 78 nitoe masikitiko yangu sana kwa serikali kuhusu kituo cha daladala cha Darajani, baada ya kuonekana gari tayari zimewekwa na kituo kile kimefungwa na wananchi wamekutwa na butwaa kati ya Baraza la Mji na Wizara ya Miundombinu. Baada ya maelezo haya naomba swali langu namba 78 lipate jawabu.

Vyombo vya Habari vimetangaza siku ya Alhamisi tarehe 16/4/2015 kuwa vituo vipya vya Daladala vitatangazwa hivi karibuni ili kuwaondolea usumbufu wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali itatangaza vituo hivyo.

(b) Kwa vile wananchi wanayo haki yao ya msingi kwa Serikali hivi vituo vitatengenezwa kwa namna itakayowawezesha wananchi kujificha mvua na jua au vitatangazwa tu kuwa sehemu ya wazi.

(c) Kilio hiki ni cha muda mrefu sana na wananchi wanaendelea kuteseka huku Serikali ikijipanga. Je, ni kwa nini Serikali isitangaze japo vituo vitatu (3) ikiwemo maeneo ya Darajani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, tarehe 16/4/2015 kulifanyika Semina ya Wadau wa Sekta ya Usafiri wa Barabara kutoka Visiwa vya Unguja na Pemba na katika Semina hiyo

ilielezwa kwamba tayari Serikali iliunda Kamati ili kuangalia na hatimae kupendekeza Vituo vipya vya daladala kwa kuanzia na Mkoa wa Mjini Magharibi.

(a) Serikali itatangaza vituo hivyo baada ya taratibu za Kisheria kukamilika.

(b) Suala la Vituo vya daladala ni suala Mtambuka**.** Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano baada ya kuyahakiki maeneo yanayofaa kuwekwa vituo hivyo na kuvitangaza itawaandikia rasmi wenye maeneo kwa upande wa sehemu ya Mji wa Zanzibar, bila ya shaka Baraza la Manispaa litajulishwa rasmi na kwa upande wa Wilaya ya Magharibi Halmashauri itajulishwa rasmi ili ziweze kujenga na kutafuta taasisi ya kujenga kwa makubaliano watakayoridhiana lakini kwa Wizara ya Miundombinu jukumu lake kwa mujibu wa Sheria ni kutangaza sehemu zinazostahili kuwekwa vituo hivyo.

(c) Kwa sasa hivi vituo ambavyo vimetangazwa vipo na vinafanya kazi lakini kutokana na mabadiliko ya ujenzi katika Mji wa Zanzibar, Serikali kupitia Bodi ya Usafiri Barabarani iliunda Kamati ya kuviangalia upya vituo vyote vya daladala na kutoa mapendekezo ambayo yanafanyiwa kazi na kama nilivyotangulia kujibu katika jibu (a) kwamba Serikali itatangaza vituo hivyo vipya mara tu baada ya taratibu za Kisheria kukamilika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kusikitisha sana kwa wananchi na wananchi chombo hiki wanakisikia na chombo hiki kisingekuwepo kama si wananchi, wametutuma wananchi, wametuchagua ili kuja kuwasemea. Lakini majibu haya hayaendani na matakwa ya wananchi.

(a) Kwa nini serikali ikatangaza kupitia vyombo vya habari na kuwadanganya wananchi kwa kuwa vituo hivi vitatangazwa muda si mrefu na leo hii tunafidia wimbo huu unazidi kuendelea haujulikani hatima yake utaishia lini.

(b) Mhe. Naiu Waziri unasema katika jibu lako la msingi mabadiliko ya ujenzi katika Mji wa Zanzibar. Mhe. Naibu Waziri mabadiliko vituo siku zote huwa barabarani mabadiliko ya ujenzi unahusu nini na vituo vya barabarani. Barabara mnazitanua au ndio hayasemeki Mheshimiwa ni kitu cha kusikitisha toka Ukoloni mtu akitoka anakotoka kituo cha daladala Darajani kinajulikana Ukoloni. Ndio mji unavyokuwa msongamano, leo kituo kile kimeondoshwa mtu anapata shida.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya msingi nimeeleza kwamba vituo vitatangazwa baada ya kukamilika taratibu za kisheria. Lakini Mjumbe analalamika kwamba tangazo

linasema kwamba tutangaza si muda mrefu na yeye anasema kwamba serikali inadanganya wananchi.

Mimi nasema kwamba kauli hii si kweli na serikali haijadanganya wananchi. Tangazo limetoka mwezi wa April leo hii mwezi wa Juni pana tafauti ya siku 60 kilichokwamisha ni taratibu za kisheria kukamilika na maelezo yako wazi, kwamba suala la vituo vya daladala ni suala Mtambuka bila shaka wizara yetu sisi na Wizara inayohusiana na Tawala za Miko kwa kushirikiana na Halmshauri na Manispaa pamoja na wadau wengine lazima tukae pamoja.

Jitihada za kukaa pamoja sote tumezishuhudia Jumamosi iliyopita kulikuwa na semina maalum ambayo ni maendelezo wa hizo taratibu za kisheria kwa bahati mbaya kwamba Mjumbe ni mtoro, angelikuja katika kikao kile cha semina asingeweza kuyasema haya. Kutoroka kwake kumepelekea kutokujua kipi ambacho kimezungumzwa na ile mipango ya serikali.

Nataka nimthibitie tu kwamba utaratibu wetu wa serikali kama tulivyaohidi tutakamilisha utaratibu wa serikali zitakapokamika taratibu hizi pamoja na za kisheria tutatangaza vituo hivyo kwa ajili ya matumizi ya wananchi wetu na suala la mabadiliko ya ujenzi wa mji wa Zanzibar wala halihitaji utaalamu kuona mtu yeyote anaona, ongezeko la watu limeongeza nyumba, maana yake vituo lazima muongeze na mubuni maeneo mapya ya kuweza kuweka vituo si watu wote ambao wanatumia Darajani.

Sasa hivi kuna njia ambayo inatoka Kiembesamaki inakwenda Bububu, kuna njia ambayo inatoka Fuoni inakwenda Bububu; hawa wote hawataki kwenda Darajani. Lazima kama serikali tufikirie zaidi ya hapa ambapo tuko leo. Kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba dhamira ya serikali jambo hili tunalifanyia kazi na litakapokamilika tutatangaza vituo.

**Nam. 27**

**Kubadili Mitaala ya Elimu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (kny Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza**:**

Kwa kuwa mfumo wa elimu Zanzibar kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari huwa zaidi unamjenga mwanafunzi kupata elimu (*knowledge)* na sio ujuzi (*skills)* na ndio maana wanafunzi wanapomaliza kidato cha pili, cha nne na cha sita hutegemea zaidi wapate ajira toka Serikalini au taasisi binafsi jambo ambalo kwa sasa ni shida na adimu mno.

Je, ni lini Serikali itabadilisha mitaala yake badala ya kutoa elimu ya Nadharia pekee katika ngazi ya shule za msingi na sekondari vile vile iweze kutoa taaluma ya ujuzi (*skills)*, biashara pamoja na ujasiriamali (*entrepreneurship)*, kusudi vijana waweze kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza shule.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 kwanza naomba kutoa maelezo kama ifutavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa mfumo wetu wa elimu, umeweka mkazo zaidi katika kuwapatia wanafunzi maarifa kuliko ujuzi. Matokeo yake wanafunzi wengi wanapomaliza masomo yao hutegemea kupata ajira kutoka Serikalini au Taasisi binafsi baada ya wao kujiajiri wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifutavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali inachukua hatua mbali mbali katika kuwaandaa wanafunzi katika kupata ujuzi. Marekebisho yamefanywa ya mitaala ya masomo kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi katika maisha ya kujiajiri wenyewe mara wanapomaliza masomo badala ya kutegemea zaidi kazi za kuajiriwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka kipaumbele katika uanzishaji wa Vituo vya Mafunzo ya Amali na Ufundi kwa madhumuni ya kuwapatia vijana ujuzi mbali mbali utakaowawezesha kujitegemea. Vituo viwili vya Mafunzo ya Amali vimejengwa huko Mkokotoni, Unguja na Vitongoji Pemba ambavyo vinachangia katika kutoa ujuzi wa fani mbali mbali za ufundi.

Pia, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali inakusudia kujenga vituo vyengine viwili vya Mafunzo ya Amali huko Makunduchi kwa upande wa Unguja na Daya Mtambwe kwa Pemba. Vituo hivi vitaongeza idadi ya vijana watakaopata mafunzo ya vitendo.

Vile vile, Wizara imefanya marekebisho ya Mtaala wa skuli za msingi yaliyoanza kufanywa mwaka 2009. Mabadiliko hayo yalihusu mbinu za ufundishaji unaozingatia nadharia na kwenda katika mbinu za ufundishaji zinazozingatia ujuzi. Mabadiliko haya yaliongozwa na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Wizara yangu imo katika mchakato wa kuingiza somo la ujasiri amali katika mitaala ya skuli za msingi na za sekondari. Hata hivyo, somo la Mafunzo ya Amali tayari linafundishwa katika mtaala ya Elimu ya Msingi. Mabadiliko haya yatakapokamilika yatasaidia katika kuwaandaa wanafunzi kuwa

na mtazamo wa kujitegemea zaidi kuliko kusubiri ajira kutoka Serikalini au katika sekta binafsi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:**Mhe. Naibu Waziri alitaja kituo cha Amali cha Mkokotoni, nafikiri bajeti yako si muda mrefu inataka kupitishwa na watendaji wako wapo. Kulikuwa kuna ada kule walimu wanaokwenda kule hupewa nauli ya shilingi elfu tatu kwa siku.

(a) Unaweza kuwaambia kuna sababu gani ya msingi mpaka hii leo walimu wale nauli zao hawajalipwa karibu mwezi wa saba.

(b) Mhe. Naibu Spika, bila ya mwalimu elimu haipatikani, kuna sababu za msingi hata Mhe. Bi Panya Ali jana alizungumza; walimu waliokwenda kusoma Iran kwa nini hamtaki kuwapa posho zao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, suala la walimu wa Iran silo swala mama katika swala ambalo liliulizwa naomba Mheshimiwa awe na subira. Jibu lake lipo na tutalijibu.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri hasa katika swala lake la msingi ameeleza baada ya kukosekana *skills* katika madarasa, lakini bado wameandaa mfumo mzuri wa kutoletea vyuo vya amali. Tunaishukuru serikali na tunaipongeza sana kwa jambo hili.

Lakini katika vyuo vya amali jana hata katika mchango wangu nilipochangia nilisema bado kuna ukosefu wa vifaa ambavyo walimu wanapaswa kupata hivyo vifaa, ili wakaweza kuwasomesha hao wanafunzi na wanafunzi wenyewe pia wanatakiwa kupata vifaa vya zile fani zao, ili wakitoka pale waende wakajiendeleze huko wanakokwenda.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini serikali itajikita katika kuwapatia walimu vifaa hivi muhimu ili masomo haya yaweze kuendelea, lakini pia kuwapatia wanafunzi vifaa baada ya kumaliza masomo yao ili wakaendeleze ujuzi wao waliopata.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu jana katika bajeti yetu Mhe. Bi Panya Ali alilizungumza hili kwa urefu wake na mimi nilimjibu kwa upana wake na nikamueleza kama wizara yangu iko katika matayarisho makubwa ya kuhakikisha vifaa hivi vya kusomeshea, kufundishia kati ya walimu na wanafunzi vinapatikana kwa umuhimu wake ambao wizara unauona.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Bi Panya Ali astahamili kidogo tu tayari kuna wafadhili ambao tumefikia nao mazungumzo vizuri, nadhani muda si mrefu tutaweza kuondoa hili tatizo la vifaa katika vituo vyetu hivi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe tulitegemea kwamba leo asubuhi *quorum* tutaipata ili tuweze kufanya majumuisho tupitishe vifungu baada ya maswali. Lakini mpaka sasa hivi nasikitika kusema kwamba tuna Wajumbe 36 tu kwenye 41. Sasa kanuni inaniruhusu ya 27 kifungu cha 4 niendelee na utaratibu mwengine.

Kwa maana hiyo, tutasoma hotuba ya Wizara ya Kilimo, baadae itakapotimia *quorum* huko mbele tutapitisha wizara zote mbili kwa pamoja. Kwa hivyo, namwita Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kuwasilisha bajeti. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2015/16 - Wizira ya Kilimo na Maliasili

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (kny Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili):** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Hotuba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama kamati kwa ajili ya kupokea kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (*PBB*).

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuibariki nchi yetu kuwa ya amani, utulivu na kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambao wengi wao ni wakulima.

Mhe. Naibu Spika, nachukuwa fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/2015, katika kuendeleza kwa vitendo Mapinduzi ya Kilimo ni dhamira ya kuendeleza wakulima na kuongeza tija katika sekta ya kilimo na maliasili.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuwapongeza viongozi wetu wakuu wa kitaifa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Idd Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa juhudi zao za kuhamisisha na kutoa miongozo katika kuendeleza sekta ya kilimo ya kilimo nchini.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha Biashara na Kilimo. Aidha, napenda kumtakia rehema aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Salmin Awadh Salmin Muwakilishi wa Jimbo la Magomeni Mungu amuweke mahali pemba peponi amin.

Naishukuru kamati hii kwa miongozo na ushauri uliipa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kufanikisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2014/15. Pia, tunaishukuru kamati kwa maelekezo waliyotupa katika maandalizi ya bajeti ya wizara ya mwaka 2015/16. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba maoni na ushauri na mapendekezo ya kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukuwa fursa hii kukupongeza wewe binafsi, pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango na miongozo katika kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kipindi chote cha miaka mitano.

## UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Kilimo bado inaendelea kuwa ni tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar, ambapo inatoa mchango mkubwa katika kujikimu kimaisha na kupatikana kwa chakula na lishe bora. Mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa kwa mwaka 2014 limeshuka kutoka asilimia 30.4 ya mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 27.9 mwaka 2014. Hali hii imesababishwa na kushuka kwa mchango wa sekta ndogo ya mazao kutoka asilimia 19.4 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 15.9 mwaka 2014. Aidha, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hii kwa kuwapatia ajira na mapato.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2014 ukuaji wa Sekta ya Kilimo umeshuka kidogo kwa asilimia 0.4, kutoka wastani wa asilimia 13.2 ya mwaka 2013. Miongoni mwa sababu zilizochangia ushukaji wa ongezeko hilo ni kupungua kwa eneo lililolimwa

la uzalishaji kutoka ekari 94,701 mwaka 2013 hadi ekari 87,944 mwaka 2014. Sababu nyengine ni hali mbaya ya hewa.

**HALI YA UZALISHAJI**

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha kupanda kwa mavuno kwa baadhi ya mazao ya kilimo ikilinganishwa na mwaka 2013. Zao la viazi vidogo limepanda kutoka tani 53,656.61 mwaka 2013 hadi kufikia tani 65,136.61 mwaka 2014, Mananasi kutoka tani 11,583.00 mwaka 2013 hadi kufikia tani 13,258.50 mwaka 2014 pamoja na mazao ya mboga na matunda kutoka tani 7,754.24 mwaka 2013 hadi kufikia tani 14,442.43 mwaka 2014 inayojumuisha na matikiti tani 8,293.00. Hali hii imetokana na wakulima walio wengi kulima mazao ya mboga na matunda ambayo ni ya muda mfupi na tija ya haraka pamoja na huduma zinazotolewa na sekta binafsi zikiwemo Taasisi ya Wazalishaji wa mazao ya mboga, matunda na maua-*Tanzania Horticultural Association (TAHA)* na Kampuni ya *Zanzibar Agricultural Investment and Development (ZAIDI*) ambayo inajihusisha na utoaji wa taaluma na vifaa vya umwagiliaji maji kwa njia ya matone pamoja na mradi wa *Tanzania Agricultural Productivity Project (TAPP)* ambao pia unatoa huduma katika kilimo cha mboga na matunda.

Mhe. Naibu Spika, msimu wa kilimo wa mwaka 2013/2014 takwimu zinaonesha pia kushuka kwa mavuno kwa baadhi ya mazao ikiwemo karafuu ambayo imeshuka kutoka tani 5,280 mwaka 2013 hadi kufikia tani 4,153 mwaka 2014, mpunga kutoka tani 33,655 mwaka 2013 hadi tani 29,564 mwaka 2014, muhogo kutoka tani 164,332.29 mwaka 2013 hadi tani 158,703.55 mwaka 2014 na ndizi kutoka tani 68,357.60 mwaka 2013 hadi kufikia tani 57,437.42 mwaka 2014. Hali hii imetokana na kupungua kwa eneo linalolimwa, maradhi na wakulima kutumia mbegu za asili **(Kiambatisho Nam. 1 kinaeleza maelezo hayo).**

**KILIMO CHA MAWENI**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikiongeza nguvu katika kuendeleza kilimo cha maweni ikiwemo kilimo cha ndimu, mbaazi, mtama, uwele na viazi vikuu ikiwa ni mazao ya chakula na biashara jambo ambalo limewapa wakulima tija ya haraka na kipato kizuri. Aidha, Wizara inaendelea kushajiisha jamii katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili katika maeneo ya hifadhi ya wananchi, kwa kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na jumuiya hizo kwa kuhifadhi maliasili na kubuni mbinu mbadala za kupunguza uharibifu wa rasilmali za misitu.

**MWELEKEO WA BAJETI KWA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI 2015/2016**

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mipango na Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (*ATI*).

Aidha, Wizara ya Kilimo na Maliasili imezingatia programu inayotumiya programu ambapo Wizara ina programu kuu tatu. Kila programu kuu imegawika katika programu ndogo ndogo.

Mhe. Spika, programu ya kwanza ya maendeleo ya kilimo, lengo lake ni kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa chakula. Programu hii inatekeleza lengo la pili la MKUTA II na kuendeleza mpango endelevu wa kupunguza umaskini, kuendeleza uhakika wa chakula na kuimarisha hali ya lishe kwa watoto na akinamama kwa kutoa kipa umbele kwa makundi hatarishi. Programu hii ina programu ndogo tatu kama ifuatavyo:-

1. Programu ndogo ya maendeleo umwagiliaji maji.

2. Programu ndogo ya utafiti na mafunzo ya kilimo.

3. Programu ndogo ya maendeleo ya huduma za kilimo na uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Naibu Spika, programu ya pili ya maendeleo ya raslimali za misitu na maliasili sizorejesheka, lengo lake kubwa ni kuimarisha matumizi endelevu ya maliasili ili kuchangia huduma za uchumi, kijamii na kimazingira zitokazonazo na raslimali za misitu na maliasili zizorejesheka.

Programu hii inatekeleza programu lengo la pili la MKUZA II na kuendeleza mpango wa endelevu wa kupunguza umaskini wa kipato na kuwepo uhakika wa chakula na lishe. Programu hii ina programu ndogo mbili kama zifuatavyo:-

1. Programu ndogo ya maendeleo ya uhifadhi wa raslimali za misitu na maliasili.

2. Programu ndogo ya uhifadhi wa usimamizi wa maliasili na mali zisizorejesheka.

Mhe. Naibu Spika, programu ya tatu ya mipango na usimamizi wa kazi za kilimo na maliasili. Lengo lake ni kuimarika kwa utawala wa sheria na ufanisi wa kazi za maendeleo pamoja na kusimamia maslahi ya wafanyakazi na raslimali za Wizara. Programu hii inatekeleza lengo la pili MKUZA II na kuweka mazingira bora kwa wafanyakazi. Programu hii ina programu ndogo tatu kama ifuatavyo:-

1. Programu ndogo ya uratibu wa kazi za mipango na utafiti.

2. Programu ndogo ya utawala.

3. Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia bajeti inayotumia mfumo wa PBB, Wizara ya Kilimo na Maliasi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itatoa huduma zifuatazo:-

- Kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji;

- Matumizi ya zana za kisasa na teknolojia za ukulimawa mpunga;

- Kuendeleza kuhifadhi raslimali za misitu na kuongeza uzalishaji wa matunda, karafuu, viungo na asili kwa kutoa elimu kwa wakulima na uoteshaji miche bora;

- Kufanya tafiti ili kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo na ushauri wa kitaalamu

- Kuimarisha huduma za matrekta na zana za kilimo, elimu kwa wakulima na upatikanaji wa pembejeo za kilimo;

- Kushajihisha utalii wa kimaumbile *eco-tourism* katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa;

- Kuendeleza kuwajengea uwezo wa kitaaluma wakulima na wafanyakazi;

- Kuanzisha na kuendeleza hifadhi ya chakula ya Zanzibar;

- Kuendelea na mapitio ya sera, sheria, mipango na kuendeleza sekta ya kilimo ili iendane na mabadiliko ya kiuchumi na kimazingira; na

- Kusimamia upatikanaji wa hati miliki za mali za Serikali zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya dira ya 2020, ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2010-2015, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUZA II), malengo ya milenia *MDG's*, mipango na mikakati ya kisekta pamoja na mpango wa mageuzi wa sekta ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yalitekelezwa kwa ufanisi kabisa.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikadiriwa kukusanya mapato ya Tsh. 845,000,000. Hadi kufikia Aprili, 2015 Wizara imekusanya jumla ya Tsh. 889,250,360 sawa na asilimia 108 ya malengo ya ukusanyaji. **(Kiambatisho Nam. 2 kinajieleza)**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 23,597,479,400. Kati ya fedha hizo, Tsh. 13,331,000,000 ni matumizi ya kazi za kawaida. Kwa kazi za maendeleo iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 9,839,479,400 **na** Ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani ni Tsh. 427,000,000. Hadi kufikia Aprili, 2015, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni TSh. 9,923,574,352 sawa na asilimia 72. Kwa miradi ya maendeleo Wizara imepata Tsh. 5,839,168,957 sawa na asilimia 60. Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani ni Tsh. 193,476,924 sawa na asilimia 45. **(Kiambatisho Nam 3 na 4 kinajieleza).**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imepata mafanikio yafuatayo:

- Wizara imeotesha jumla ya miche 627,250 ya mikarafuu (Unguja 304,150 na Pemba 323,100) sawa na asilimia 63 ya lengo;
- Miche ya misitu 1,027,685 (Unguja 882,385 na Pemba 145,300), miche ya matunda na viungo 261,583 (Unguja 220,915 na Pemba 40,667) imeoteshwa;
- Pembejeo za kilimo cha mpunga, kwa msimu wa masika 2015 jumla ya ekari 16,197 (Unguja 5,608 na Pemba 10,589) zimeshachimbuliwa, mbolea tani 750 (TSP tani 150 na UREA tani 600), dawa ya kuulia magugu lita 15,000 pamoja na mbegu ya mpunga tani 114 zimenunuliwa kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku;
- Kukamilika ujenzi wa miundombinu katika bonde la Umwagiliaji maji liliopo Makombeni ambapo ekari 22.5 zimelimwa na kunufaisha wakulima 120;
- Kutayarisha michoro ya miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Makwararani, Mlemele, Kibokwa, Kilombero na Cheju;
- Ujenzi wa tuta la kuzuia maji ya bahari yasiingie katika maeneo ya kilimo huko Koowe unaendelea vizuri. Jumla ya mita 800 zimekamilika sawa na wastani wa asilimia 70 ya kazi;
- Ujenzi wa Barabara za maeneo ya kilimo Unguja na Pemba umeanza na umewekewa kifusi kilomita 20.8;
- Wizara imekamilisha mapitio ya Sera, Sheria na Mpango wa Muda Mrefu wa Matumizi ya Misitu;
- Mipango 50 ya usimamizi wa misitu ya jamii imekamilika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali;
- Mipango Mikakati wa Chuo cha Kilimo cha Kizimbani na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar imekamilika;
- Wizara imefanikiwa kununua mtambo wa kukamulia mafuta ya alizeti wenye uwezo wa kukamua tani 6.5 za alizeti kwa siku. Sambamba na utoaji wa mafunzo maalum ya ukamuaji kwa wakulima na watendaji wa Wizara. Aidha, kwa mwaka huu tani tatu za mbegu ya alizeti ambayo itapandwa katika ekari 3,000 (1,500 maeneo ya juu na 1,500 mabondeni baada ya kuvuna mpunga) Unguja na Pemba zimenunuliwa;
- Jumla ya lita 422 za mafuta ya alizeti yamekamuliwa na kilo 863 za mashudu zimepatikana kutokana na alizeti iliyozalishwa;

- Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini *(M&E Framework)* pamoja na mpango mpya wa ukusanyaji wa takwimu za Kilimo na Maliasili umekamilika na umeanza kutumika;
- Mashirikiano na taasisi binafsi zinazojihusisha na kilimo cha mboga na matunda nchini zikiwemo *Zanzibar Agricultural Investment and Development Inc (ZAIDI) ya Zanzibar, Tanzania Horticultural Association (TAHA)* ya Tanzania Bara zimeendelea na *Tanzania Agriculture Productivity Program (TAPP), Feed the Future (USAID)*, Ubalozi wa Norway, *Pemba Foundation Program, European Union* na wengineo yamefanyika;
- Wizara pia imeendeleza mahusiano pamoja na kupanua wigo huo na Wakala wa Mbegu - Tanzania (ASA), MVIWATA, *Comparative Africa Rice Initiatives (CARI), Zamzam Irrigation Infrastructure Company* ya Marekani;
- Wanafunzi 91 wamehitimu Chuo cha Kilimo Kizimbani (24 Diploma, 67 Cheti). Wahitimu 7 tayari wamejiunga na vyuo vikuu Tanzania Bara. Aidha, wanafunzi 194 wanaendelea na mafunzo (Diploma 49 na Cheti 145); na
- Jumla ya hekta 110 zimepandwa miti katika mashamba ya Serikali na maeneo yaliyochimbwa mchanga.

Mhe. Naibu Spika**,** utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara na Taasisi zake ulikuwa kama ifuatavyo:

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya Idara hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti. Idara pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

## MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuipitia Sera ya Kilimo, kukamilisha Sheria ya Uhifadhi na utibabu wa mimea;
- Kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kuzisambaza kwa wadau wote;
- Kufanya tafiti za kijamii, kiuchumi ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika jamii katika uzalishaji na tija;

- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu muhimu za kijamii na kiuchumi katika sekta ya kilimo ikiwemo uzalishaji na masoko ya mazao ya chakula na biashara, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya Wizara;
- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara na taasisi za ndani, kikanda na nje ya nchi pamoja na kushiriki katika vikundi kazi vya kitaifa, mikutano na makongamano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
- Kukamilisha mapitio ya tafiti zilizowasilishwa pamoja na uchapishaji wa Toleo la tatu la Utafiti wa Kilimo (*3rd Annual Agricultural Research Proceeding); na*
- Kuratibu na kusimamia miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2014/2015 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Utayarishaji wa Sheria mpya ya Pembejeo na matayarisho ya mapitio ya Sera ya Kilimo yamefanyika. Sheria ya Utibabu na Uhifadhi wa Mimea bado ipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupata maoni. Aidha, mafunzo ya siku tatu kwa watafiti, wakulima na wanasheria 25 juu ya utekelezaji wa Sheria ya Haki miliki kwa wagunduzi wa mbegu mpya (*PBR*) yamefanyika;
- Nakala 1,000 za Jarida la mkulima zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau wa kilimo pamoja na vipindi 3 vya kuelemisha jamii kupitia TV na 6 vya Redio vimetayarishwa;
- Utafiti wa mazao ya mboga na matunda katika soko la kitalii nchini umeanza kwa ukusanyaji wa takwimu kwa Unguja na Pemba. Utafiti na ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji wa ndizi katika Wilaya za Wete, Micheweni na Mkoani kwa lengo la kutathmini ununuzi wa zao hilo kutoka kwa wakulima na wasafirishaji kutoka Pemba kwenda Unguja unaendelea;
- Mfumo mpya wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara pamoja na mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Kilimo na Maliasili umetayarishwa. Mafunzo ya ujazaji wa fomu za takwimu kwa mabwana/mabibi shamba 189 Unguja na Pemba yamefanyika. Aidha, kitengo cha takwimu kimeimarishwa kwa kununuliwa kompyuta 3 (2 Unguja na 1 Pemba);
- Mashirikiano kati ya Wizara na taasisi za ndani, kikanda na nje ya nchi yamefanyika baina ya *USAID*, *EPINAV*, *KOICA*, Bunge la Norway,

*IFAD*, *AfDB* na Tume ya Mipango Zanzibar, *Milele Foundation, AVRDC, VSO* na *CARI*; na

- Jumla ya maandiko ya tafiti 12 "yamekusanywa na matayarisho ya uchapishaji wa toleo la Tatu la Tafiti *(3rd Research Proceeding)* yanaendelea. Aidha, mapitio ya Sekta ya Kilimo *(Agriculture Sector Review na Public Expenditure Review)* kwa mwaka 2013 yamefanyika.

**Mhe. Naibu Spika,** kwa mwaka 2014/2015 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji a programu tatu na mradi mmoja pamoja kama ifuatavyo:

- Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Kilimo na kuongeza Thamani ya Mazao (*MIVARF*) **(Kiambatisho Nam. 5).**
- Mradi wa Usarifu wa Mazao **(Kiambatisho Nam. 6).**
- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–*ASDP-L*, **(Kiambatisho Nam.7).**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara iliombewa jumla ya Tsh. 377,129,000 kutoka Serikalini, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2015 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 252,165,273 (Mishahara Tsh. 146,497,600 sawa na asilmia 83 na matumizi mengineyo Tsh. 105,667,673 sawa na asilimia 53).

## IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, Idara inaratibu masuala mtambuka kama Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

## MALENGO YA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa 2014/2015 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuendelea na uhakiki wa mali za Serikali zilizo katika Wizara ya Kilimo na Maliasili na kuzipatia hati miliki;
- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 20 Unguja na Pemba;
- Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;

- Kuratibu ukusanyaji wa mapato ambayo yanakadiriwa kuwa ni Tsh 845,000,000;na
- Kuhakiki wafanyakazi wa Wizara Pemba kwa kutumia mfumo wa Database.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Jumla ya wafanyakazi 100 wanaendelea na masomo katika vyuo na fani tofauti;
- Mafunzo ya Sheria ya manunuzi Na. 9 ya mwaka 2005 kwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi (PMU) yamefanyika;
- Mafunzo ya uelimishaji Rika, Sheria Na. 2 ya Utumishi wa Umma na mafunzo ya utengenezaji wa Nominal Roll ya Wizara yametolewa kwa wafanyakazi husika;
- Mafunzo pia yametolewa kwa maafisa wa ukusanyaji mapato, uwekaji kumbukumbu na watunzaji ghala;
- Utaratibu wa kuyapatia hati miliki maeneo na majengo ya Wizara umefanyika kwa maeneo ya Bonde la Cheju, Kibonde Mzungu, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani, eneo la Kibokwa na Nyumba iliyopo Migombani;
- Jumla ya wafanyakazi 36 wamestaafu na kupatiwa stahiki zao;
- Wafanyakazi 25 (Wanaume 19 na Mwanamke 6) wamekwenda likizo bila ya malipo;
- Jumla ya wafanyakazi 37 wakiwemo Mabwana/mabibishamba 37 na 11 kada nyenginezo wameajiriwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015; na
- Jumla ya mapato ya Tsh. 889,250,360 sawa na asilimia 105 yamekusanywa kutoka vyanzo vya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara iliombewa Tsh. 1,543,027,000 hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2015 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 1,223,550,520 (Mishahara Tsh. 689,340,450 sawa na asilmia 79 na matumizi mengineyo Tsh. 534,210,070 sawa na asilimia 53).

## IDARA YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalam, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao yanayosafirishwa na kuingizwa nchini.

## MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ililenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi juu ya mbinu shirikishi za kilimo bora kwa mabibi na mabwanashamba 140 (90 Unguja na 50 Pemba);
- Kuendeleza kazi ya usambazaji wa dawa katika mitego 21,615 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda pamoja na kununua mitego mipya 500 na kutoa mafunzo kwa kutumia mbinu mchanganyiko Unguja na Pemba;
- Kuendeleza kazi za Karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu kwa ajili ya usafirishaji na kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima;
- Kuzalisha tani 350 kutoka kwa wakulima na kununua tani 150 ya mbegu ya mpunga kutoka Tanzania Bara na kuzalisha tani 5 za mbegu ya mahindi, 2 za mtama na tani 8 za jamii ya kunde katika kituo cha uzalishaji mbegu Bambi na mashamba ya JKU;
- Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kutengeneza matrekta 29 na zana zake (10 Pemba na Unguja 19);
- 1,500 juu ya mbinu za kilimo bora kwa kupitia Mabwana/Mabibishamba, skuli za wakulima na jumuia zao; na
- Kununua na kusambaza tani 750 za mbolea (TSP tani 150 na UREA tani 600) na lita 20,000 za dawa ya kuulia magugu.

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imetekeleza kazi zake kama ifuatavyo:

- Mafunzo ya muda mfupi juu ya mbinu shirikishi za kilimo bora kwa mabibi na mabwana shamba 178 (Unguja 103 na Pemba 75) yametolewa; (wanawake 57 na wanaume 121);
- Mitego mipya 2,000 na dawa lita 400 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda imenunuliwa. Mitego 3,530 imebadilishiwa dawa na kusambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba; Pia wakulima katika Shehia 156 wamepatiwa mafunzo ya utengenezaji wa mitego ya nzi waharibifu wa matunda kwa kutumia chupa za maji ya kunywa;
- Jumla ya tani 14 za karafuu na tani 325 za mwani zimekaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi, tani 1,584 za mazao ya chakula kutoka Tanzania Bara na tani 9,958 za mazao ya chakula kutoka nje ya nchi zimekaguliwa;
- Tani 159 za mbegu ya mpunga zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima;
- Jumla ya matrekta 31 na zana zake (12 Pemba na Unguja 19) yalifanyiwa matengenezo ya kawaida; na
- Jumla ya tani 750 za mbolea (TSP tani 150 na UREA tani 600) na lita 15,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara iliombewa jumla ya Tsh. 4,802,444,000 kutoka serikalini. Hadi kufikia Aprili, 2015 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 3,504,258,830 kutoka SMZ (Mishahara Tsh. 1,847,919,550 sawa na asilmia 79 na matumizi mengineyo Tsh. 165,339,280 sawa na asilimia 67).

**TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO**

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti katika sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi ya Uafiti wa Kilimo inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo ndani ya sekta ya kilimo na Maliasili.

**MALENGO YA TAASISI YA UTAFITI KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi ililenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuanzisha na kuendeleza tafiti za mbegu na mbinu mpya za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara yakiwemo nazi, mpunga, mazao ya mizizi, migomba, mboga na matunda.;

- Kukarabati maabara ya mazao ya Matangatuani, majengo ya uchunguzi wa mimea (*screen house*) na kujenga uzio katika maabara mpya ya utafiti wa mpunga ilioko Kizimbani; na
- Kukamilisha Mpango Mkakati wa miaka kumi (2015-2025) na utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ili kuweka mazingira mazuri katika utekelezaji wa kazi za utafiti.

**UTEKELZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2014/15**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Taasisi imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Tafiti tatu zenye kujumuisha mbegu 56 mpya za mpunga zimeanzishwa na tafiti nyengine 3 zimeendelezwa kwa lengo la kupata mbegu zenye uzalishaji mzuri na zenye kustahamili maradhi na wadudu;
- Kukamilika kwa kazi ya uzalishaji ya mbegu tani 6.7 aina ya *SUPA BC* kwa ajili ya utafiti na kuisambaza kwa wakulima kwa kushirikiana na Mradi wa NAFAKA;
- Wakulima 2,000 (Unguja 1,300 na Pemba 700) wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za uzalishaji wa zao la mpunga chini ya mradi wa NAFAKA;
- Majaribio ya aina mpya za mbolea ya YaraMilla (ya kupandia) na *UDP* (ya kukuzia) yamefanyika katika maeneo matatu Pemba moja na Unguja mawili;
- Majaribio matano ya mbegu bora za muhogo yamefanyika kwa kushirikiana na wakulima 120 wa Unguja na Pemba;
- Majaribio ya mbegu za viazi vitamu vyenye viini lishe yamefanyika katika maeneo ya Kiliombero, Kizimbani, Bambi, Matangatuani na Makangale. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kwamba mbegu mbili kati ya 10 zina uwezo wa kutoa hadi tani 15 kwa hekta moja na zinastahamili wadudu na maradhi na hivyo kupendekezwa kwa wakulima kwa uzalishaji;
- Tafiti nne za matumizi ya aina tofauti ya mbolea ya samadi kwa mazao ya mboga yakiwemo tungule, mchicha, bilingani na bamia zimefanyika katika kituo cha Matangatuani, tafiti hizo zinaendelea;
- Utafiti wa ukuaji wa miche ya mikarafuu kwa kutumia udongo tofauti unaendelea katika kituo cha utafiti cha Matangatuani;
- Ukarabati wa mfumo wa maji katika Kituo cha Utafiti Matangatuani umefanyika sambamba na kununua na kufunga kifaa cha uchunguzi wa udongo (*soil sample testing kits*); na

- Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Taasisi ya Utafiti umekamilika.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Taasisi iliombewa jumla ya Tsh. 1,221,269,000 kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 300,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2015 imepata Tsh. 976,523,880 (Mishahara Tsh. 940,189,300 sawa na asilmia 81 na matumizi mengineyo Tsh. 36,334,580 sawa na asilimia 57) na Tsh. 20,000,000 sawa na asilimia 6.6 kwa kazi za maendeleo zimepatikana.

**CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI**

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, malasili na mifugo katika ngazi tofauti.

**MALENGO KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimelenga kutekeleza kazi zifuatazo:

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 184, ngazi ya Cheti 135 na Diploma 49;
- Kuendelea na kazi za ujenzi wa dakhalia moja yenye ghorofa 4 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 wa kike kwa wakati mmoja;
- Kufanya ukarabati wa dakhalia mbili;
- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji katika bonde moja kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II*.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2014/2015**

- Jumla ya wanafunzi 168 (Cheti 130 na Diploma 38) wanaendelea na masomo;
- Ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi wa kike umeshaanza na unaendelea;
- Ukarabati wa dakhalia mbili (ya wanafunzi wa kike na wa kiume) umeshafanyika; na
- Mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa Umwagliaji maji na kutegemea mvua yamefanyika kwa wakulima 81 na mabwana/bibi shamba 40 kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II* kwa ufadhili wa *JICA* na Mradi wa NAFAKA kwa ufadhili wa *USAID*.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2014/2015 kwa kushirikiana na mradi wa *EPINAV*, Chuo kimeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

- Mpango Mkakati wa miaka 10 umekamilika;
- Huduma za maktaba zimeimarishwa kwa kuwekwa huduma za mtandao;
- Tafiti mbili za kunenepesha mbuzi na kondoo zimefanyika. Aidha, utafiti umeonesha malisho kwa kutumia dagaa, mashudu ya nazi na unga wa makapi ya mpunga unanenepesha mbuzi (unaongeza nyama na maziwa); na
- Ziara za kimasomo kwa wafanyakazi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani zimefanyika baina ya Chuo cha Kilimo - Sokoine, Vyuo vya Kilimo na Mifugo vya Tanzania Bara zimefanyika, *University of Life Sciences*, Taasisi inayotoa Huduma za Kujitolea ya Norway.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kilimo kinaendelea kuwajengea uwezo walimu na wafanyakazi wake kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Jumla ya Walimu wanne wanaendelea na masomo ya Shahada ya pili na Mwalimu mmoja anendelea na Shahada ya tatu katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, wafanyakazi wanne wanaendelea na masomo ya Diploma katika Vyuo tofauti.

Mhe. Naibu Spika, Chuo kwa kushirikiana na Chuo cha *SJH Norway* kinaendelea kubadilishana walimu wawili kwa kila Chuo ambao watafanya kazi za kujitolea kwa muda wa mwaka mmoja. Mradi huu wa ushirikiano utakua wa miaka mitatu ambapo jumla ya walimu sita kutoka katika kila Chuo watapata fursa ya kushiriki. Kwa mwak wa fedha 2014/15, walimu wawili wamekweda Norway kwa ajili ya program hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kiliombewa Tsh. 427,000,000 kama Ruzuku na Tsh. 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2015, Chuo kimepatiwa ruzuku ya Tshs. 193,476,924 sawa na asilimia 45 ya makadirio. Kwa kazi za maendeleo Chuo kimepatiwa Tsh.15,000,000 sawa na asilimia 15 ya makadirio.

**IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA**

Mhe. Naibu Spika, Sekta hii ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wananyama pori na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu.

**MALENGO KWA MWAKA 2014/2015**

- Kuotesha miche 1,000,000 ya misitu na miche 500,000 ya matunda na viungo katika vitalu vya serikali na kuzalisha miche 1,000,000 ya mikarafuu;
- Kupanda miti ya misitu eneo la hekta 300 katika mashamba ya Serikali, hekta 40 za mikoko na kilomita 60 katika maeneo ya barabarani;
- Kukamilisha mipango shirikishi ya matumizi endelevu ya maliasili zizisorejesheka katika Wilaya za Kaskazini 'A', 'B' na Kati kwa Unguja na Wilaya za Mkoani na Wete kwa Pemba;
- Kukamilisha na kutekeleza mpango wa kujikinga na matukio ya moto kwenye misitu ya serikali na jamii;
- Kuimarisha na kuendeleza ufugaji nyuki wa kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa asali, kuoengeza kipato kwa wanajamii na utunzaji wa misitu katika maeneo yanayozunguka misitu ya hifadhi ya asili;
- Kufanya tathmini ya akiba ya mchanga na kujua mahitaji kwa mwaka;
- Kuendeleza uhifadhi na kuimarisha utalii endelevu katika hifadhi za misitu;
- Kuifanyia marekebisho Sheria ya Misitu; na
- Kuyatambua na kutayarisha mpango wa usimamizi wa mashamba ya Serikali pamoja na eka tatu.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

- Miche 2,076,397 imeoteshwa katika vitalu vya Serikali, mikarafuu 692,372 (Unguja 317,530 na Pemba 374,842), miche ya misitu 1,089,140 (Unguja 917,140 na Pemba 172,000) na miche ya matunda na viungo ni 294,885 (Unguja 230,385 na Pemba 64,500);
- Hekta 110 zimepandwa miti katika mashamba ya serikali (Chaani, Dunga na Masingini) na maeneo yaliyochimbwa mchanga. Aidha, hekta 98.5 zimepandwa miti ya mikoko katika maeneo yaliyo wazi;
- Mikutano ya ndani ya maandalizi ya mpango mkakati wa utekelezaji ilifanyika Unguja na Pemba ambapo ‘Mpango’ wa pamoja wa utekelezaji umeandaliwa tayari kwa utekelezaji;
- Mpango wa kujikinga na matukio ya moto umetayarishwa, uchimbaji wa visima 11 katika maeneo ya Jozani na Ghuba ya Chwaka,

Jambiani-Muyuni na Kiwengwa-Pongwe umekamilika pamoja na ununuzi wa vifaa vya uzimaji wa moto. Aidha, Idara ilichukua juhudi za uzimaji wa moto uliotokea maeneo ya Jozani, Kiwengwa-Pongwe, Dunga, Kichwele na Ngezi Vumawimbi ambapo jumla ya hekta 93.2 zimeathirika;

- Ufuatiliaji na ukusanyaji wa takwimu za ufugaji wa nyuki umefanyika katika Shehia za Kianga, Dole, Kizimbani na Bububu. Aidha, mafunzo ya njia bora za uzalishaji wa asali yametolewa pamoja na kuwapatia mizinga 35 wanajamii;
- Utalii wa kimazingira umeweza kuwapatia Dola za kimarekani 5,800 wanajumuiya wa Shehia za Mtende na Muyuni kwa uwindaji wa Paa nunga wawili, Ngombo vidole vinne, Hondo hondo, Kima mweusi, Ngombo misaraba na Paa mwekundu;

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Miradi miwili kama ifuatavyo:

- Mradi wa kuimarisha zao la Karafuu (Kiambatisho Nam. 8); na
- Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili – HIMA (Kiambatisho Nam. 9).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara iliombewa jumla ya Tsh. 1,605,448,000 kutoka SMZ na Tsh. 84,000,000 kutoka Norway hadi kufikia Aprili, 2015 Idara imepatiwa Tsh.1,283,604,957 (Mishahara Tsh. 1,183,845,350 sawa na asilmia 82 na matumizi mengineyo Tsh. 99,759,607 sawa na asilimia 59). na Tsh. 84,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Norway.

**IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE**

Mhe. Naibu Spika, Idara ya uhakika wa chakula na lishe ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe na tahadhari ya mapema juu ya matukio yanayohusiana na hali ya usalama wa chakula nchini.

**MALENGO KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe imelenga kutekeleza kazi zifuatazo:

- Kuchapisha na kusambaza matokeo ya ufuatiliaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe ikiwemo (*Food Balance Sheet Report*);

- Kuandaa vipindi vya redio na kuchapisha majarida juu ya masuala ya lishe bora;
- Kuendeleza database ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kuanzisha timu ya wataalamu wa ufuatiliaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe; na
- Kukarabati ghala moja la Hifadhi ya Taifa ya Chakula.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2014/2015**

- *Database* ya uhakika wa chakula na lishe imekamilika na hivi sasa ipo katika hatua za kuingiza takwimu na taarifa husika kwenye tovuti; Vikundi kazi vya ufuatiliaji wa taarifa za masoko na masuala ya lishe katika jamii vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo;
- Ukarabati wa ghala haukufanyika kutokana na ukosefu wa fedha;
- Miongozo ya mawasiliano juu ya masuala ya lishe yamekamilika na yapo katika hatua ya uchapishaji;
- Nakala 1,970 za Kijarida cha Lishe juu ya njia sahihi za unyonyeshaji wa maziwa ya mama na nakala 2,000 za kijarida juu ya aina za vyakula bora vya asili kwa watoto vimechapishwa na kusambazwa katika Shehia za Wilaya za Kaskazini A, Micheweni na Chake chake;
- Jumla ya vikundi 161 vya mama kwa mama na baba kwa baba vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo juu ya masuala ya lishe bora kwa mama wajawazito na wanaonyonyesha. Wanajamii 1,444 (wanaume 207 na wanawake 1,237) wamefaidika na mafunzo haya;
- Kamati 24 za Uhakika wa chakula na Lishe zimeanzishwa, 12 kutoka Wilaya ya KaskaziniA, 6 Wilaya ya Chake chake na 6 Wilaya ya Micheweni. Na kupatiwa mafunzo juu ya kuzuia Upungufu wa Damu kwa Wajawazito na Wanaonyonyesha pia na udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka miwili.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Lishe wa Mwanzobora (Kiambatisho Nam. 10).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara iliombewa jumla ya Tsh. 194,500,000 kutoka SMZ na Tsh. 64,800,000 kutoka *USAID*. Hadi kufikia Aprili, 2015 Idara imepatiwa Tsh. 153,852,105 kutoka SMZ (Mishahara Tsh. 125,412,600 sawa na asilmia 93 na matumizi mengineyo Tsh. 28,439,505 sawa na asilimia 47) na Tsh. 43,800,000 sawa na asilimia 68 kutoka *USAID*.

## IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Umwagiliaji Maji inajukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini. Katika kutekeleza kazi hiyo Idara inatoa taaluma za uzalishaji na kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

## MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

- Kukarabati njia za mashambani zenye urefu wa mita 400 katika vituo vya Bumbwi sudi na Mtwango;
- Kuchimba visima viwili katika vituo vya Kibondemzungu (Unguja) na Ole (Pemba) pamoja na vibanda vya kuhifadhia pampu;
- Kuunga umeme katika vituo vya Machigini, Mtwango na Bumbwisudi;
- Utayarishaji wa eneo la hekta saba kwa upimaji na ukataji wa plot katika kituo cha Makombeni Pemba;
- Ukarabati wa pumpu sita na visima vitatu katika vituo vya Makombeni, Bumbwisudi, Cheju, Kibokwa, Mtwango na Uzini;
- Ujenzi wa banio katika tuta la kuzuia maji ya bahari bonde la *CHAMAWE (spillway)*
- Kukarabati majengo ya vituo vinne vya Umwagiliaji maji (Mtwango, Bumbwisudi, Weni na Mbweni) pamoja na kujenga kituo kipya cha Kianga;
- Kutoa mafunzo kwa wakulima wa umwagiliaji maji na kuanzisha skuli kumi za wakulima (Koani, Kianga, Bumbwisudi field 1 na 3, Kibokwa na Uzini kwa Unguja pamoja na Tibirinzi, Ole, Kinyakuzi, Mangwena kwa Pemba; na
- Kutoa mafunzo kwa njia ya ziara kwa wakulima wa Makombeni Pemba.

## UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

- Kisima kimoja kimechimbwa katika skimu ya Kibokwa;
- Vishamba viwili vya maonesho juu ya kilimo bora cha uzalishaji wa mpunga vimetayarishwa katika skimu za Makombeni na Saninga – Pemba;
- Usambazaji wa maji katika skimu ya Mtwango umekamilika;

- Usawazishaji wa eneo la hekta saba *(land levelling)*, upimaji na ukataji wa ploti katika skimu ya Makombeni umekamilika;
- Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ukarabati wa bwawa la bonde la Mwera na ujenzi wa njia za kutolea maji ya dharura 'spill way' umekamilika;
- Ujenzi wa banio katika tuta la kuzuia maji ya bahari bonde la Chamawe umekamilika;
- Ujenzi wa tuta mita 400 la kuzuia maji ya bahari bonde la Koowe umeanza na unaendelea;
- Ukarabati wa bwawa katika bonde la Kinyakuzi umefanyika kazi inaendelea; na
- Kisima kimoja kimechimbwa katika bonde la Muyuni. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika hekta 10 haukukamilika kutokana na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha chumvi katika kisima hicho.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji (Kiambatisho Nam. 11).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara iliombewa jumla ya Tsh. 725,370,000 kutoka SMZ hadi kufikia Aprili, 2015 Idara imepatiwa Tsh.543,213,400 kutoka SMZ (Mishahara Tsh. 508,213,700 sawa na asilmia 78 na matumizi mengineyo Tsh. 34,999,700 sawa na asilimia 49). Tsh. 3,858,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2015 Idara imepatiwa Tsh. 1,254,288,990 kutoka KOREA EXIM BANK sawa na asilimia 30.

**MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI 2015/2016**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Malengo ya Milenia (MDGs), Mipango na Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI). Aidha, Wizara ya Kilimo na Maliasili imezingatia bajeti inayotumia mfumo wa Programu (PBB) ambapo Wizara ina Programu kuu tatu, kila programu kuu imegawika katika programu ndogo:

Mhe. Naibu Spika, Programu ya kwanza ya Maendeleo ya Kilimo lengo lake ni kuongeza uzalishaji na kupunguza uagiziaji wa chakula. Programu hii inatekeleza

lengo la pili la MKUZA II la kuendeleza mpango endelevu wa kupunguza umasikini, kuendeleza uhakika wa chakula na kuimarisha hali ya lishe kwa watoto na kina mama, kwa kutoa kipaumbele kwa makundi hatarishi. Programu hii ina programu ndogo tatu kama ifuatavyo:

i. Programu ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji;
ii. Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo; na
iii. Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na uhakika wa chakula na lishe

Mhe. Naibu Spika, Programu ya pili ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Malasili Zisizorejesheka, lengo lake kubwa ni kuimarisha matumizi endelevu ya Maliasili ili kuchangia huduma za kiuchumi, kijamii na kimazingira zitokanazo na Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Programu hii inatekeleza lengo la pili la MKUZA II la kuendeleza mpango endelevu wa kupunguza umaskini wa kipato na kuwepo uhakika wa chakula na lishe. Programu hii ina programu ndogo mbili kama zifuatazo:

i. Programu ndogo ya Maendeleo ya uhifadhi wa rasilimali za misitu na maliasili; na
ii. Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliaisili Zisizorejesheka.

Mhe. Naibu Spika, Programu ya tatu ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Kilimo na Maliasili, lengo lake ni kuimarika kwa utawala wa sheria na ufanisi wa kazi za maendeleo pamoja na kusimamia maslahi ya wafanyakazi na rasilimali za Wizara. Programu hii inatekeleza lengo la pili la MKUZA II la kuweka mazingira bora kwa wafanyakazi. Programu hii ina programu ndogo tatu kama ifuatavyo:

i. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Mipango na Utafiti;
ii. Programu ndogo ya Utawala; na
iii. Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia Bajeti inayotumia mfumo wa *PBB* Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itatoa huduma zifuatazo:

- Kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji, matumizi ya zana za kisasa na teknolojia za ukulima wa mpunga;

- Kuendelea kuhifadhi rasilmali za misitu na kuongeza uzalishaji wa matunda, karafuu, viungo na asali kwa kutoa elimu kwa wakulima na uoteshaji wa miche bora;
- Kufanya tafiti ili kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo na kutoa ushauri wa kitaalamu;
- Kuimarisha huduma za matrekta na zana za kilimo, elimu kwa wakulima na upatikanaji wa pembejeo za kilimo;
- Kushajiisha utalii wa kimaumbile *(eco-tourism)* katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa;
- Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma wakulima na wafanyakazi;
- Kuanzisha na kuendeleza hifadhi ya chakula ya Zanzibar;
- Kuendelea na mapitio ya Sera, Sheria na Mipango ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ili iendane na mabadiliko ya kiuchumi na kimazingira;
- Kusimamia upatikanaji wa hati miliki za mali za Serikali zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

**MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MGAWANYO WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara inakadiriwa kukusanya mapato ya TSh. 966,393,000 na matumizi ya TSh. 13,191,100,000 kwa Programu za Wizara ya Kilimo na Maliasili yenye kuzingatia gharama za Idara /Vitengo vilivyomo katika programu husika, Mishahara na ruzuku kwa Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya TSh. 34,983,200,000 zimetengwa (TSh. 33,323,200,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo na TSh. 1,660,000,000 ikiwa ni mchango kutoka Serikali kuu). Jumla ya gharama kwa programu zote za Wizara ya Kilimo na Maliasili ni Shilingi 48,174,300,000.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili itatoa huduma na itatekeleza Shabaha zilizowekwa katika Programu. Aidha, taarifa kamili za Wizara hii zinaelezwa katika kitabu cha makadirio, mapato na matumizi ya Serikali kuanzia ukurasa wa 546 hadi 571. Mchanganuo wa matumizi katika programu kuu na ndogo unaonekana katika viambatisho *(Kiambatisho Nam. 13, 14 na 15).* Aidha, utekelezaji wa huduma katika programu ni kama ifuatavyo:

Programu ya Maendelo ya Kilimo inahusisha Idara ya Umwagiliaji Maji, Kilimo, Uhakika wa Chakula na Lishe, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani. Jumla ya Tsh. 32,888,154,000 (TSh. 7,189,412,000 kwa kazi za kawaida, ruzuku na mishahara na TSh. 25,698,742,000 kwa kazi za Maendeleo) zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha malengo yaliyowekwa kwa kipindi cha 2015/2016, hii ni sawa na asilimia 68 ya bajeti ya Wizara.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji**

Mhe. Naibu Spika, kazi za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Umwagiliaji Maji. Lengo la Programu hii ni kuongeza maeneo ya umwagiliaji na kutumia teknolojia ya umwagiliaji, matokeo ya muda mfupi yanayotarajiwa ni pamoja na kuwepo kwa miundombinu ya umwagiliaji, jumuiya imara za watumiaji maji kwa umwagiliaji na kuongezeka kwa uzalishaji. Vile vile, kutakuwa na viashiria vya utekelezaji vikiwemo idadi ya maeneo ya umwagiliaji, idadi ya visima vilivyochimbwa, pampu zilizowekwa na mavuno kwa hekta. Programu hii ina shabaha zifuatazo:

- Kuweka Miundombinu ya Umwagiliaji maji

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo, lengo ni kuimarisha na kuendeleza Tafiti za Kilimo na Maliasili pamoja na kuimarisha uwezo wa Chuo cha Kilimo Kizimbani na kuongeza wataalamu 697 wa fani ya Kilimo na Mifugo. Matokeo ya muda mfupi yanayotarajiwa ni wakulima kutumia matokeo ya utafiti na kuongezeka kwa uzalishaji, Viashiria vya Utekelezaji ni idadi ya mbinu mpya (teknolojia) zilizotumiwa na wakulima pamoja na idadi ya nyenzo/vifaa, walimu wenye sifa na wanafunzi waliohitimu katika ngazi ya Cheti na Diploma. Shabaha za utekelezaji ni kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na misitu. Huduma zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:

- Kutoa taaluma ya kilimo na Mifugo ngazi ya cheti kwa wanafunzi 150 na Diploma wanafunzi 50;
- Kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Kilimo Kizimbani kwakujenga Dakhalia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 56 na kukarabati majengo ya Chuo;
- Kuimarisha ulinzi na kutayarisha mpango wa matumizi ya shamba la Razaba kule Bagamoyo; na
- Kutoa mafunzo ya Kilimo bora cha Mpunga na umwagiliaji maji kwa wakulima 491 kwa kushirikiana na mradi wa TANRAYS 2

Mhe. Spika, kwa upande wa utafiti shabaha zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Kuanzisha na kuendeleza tafiti kumi na tano za mbinu za usalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara yakiwemo Mpunga, mhogo, viazi vitamu, mboga, minazi na mikarafuu;
- Kukarabati maabara moja utafiti wa mazao ya Matangatuani;
- Kujenga uzio katika maabara mpya ya utafiti Kizimbani na ununuzi wa madawa na vifaa vya maabara za utafiti kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utafiti wa mazao;
- Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa kufundisha wafanyakazi watatu katika shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu ifikapo June, 2016;
- Kusambaza matokeo ya utafiti kupitia vishamba darasa 15;
- Vipindi vya TV vitano, Redio 5 na vipeperushi 1,500; na
- Kutayarisha kanuni za taasisi ya utafiti na kuimarisha mashirikiano na taasisi za utafiti za ndani na nje ya nchi.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Kilimo, lengo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za kilimo kwa wakulima. Matokeo ya muda mfupi ni kuwepo kwa ongezeko la wakulima kutumia pembejeo za kilimo, wakulima kutumia mbinu bora za kilimo na kuwepo kwa ongezeko la mazao ya chakula na biashara. Viashiria vya Utekelezaji vya programu hii ni maeneo yaliyolimwa, kiwango cha uzalishaji, asilimia ya wakulima wanaotumia mbinu na teknolojia bora za kilimo, idadi ya wakulima waliopata ruzuku za pembejeo za kilimo. Shabaha ya Programu hii ni wakulima kupata huduma za elimu kwa wakulima na matumizi ya mbegu na miche bora kama ifuatavyo:

- Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kutengeneza matrekta 30 na zana zake Unguja 20 na Pemba 10;
- Kutoa mafunzo kwa madereva 70 n mafundi 30 juu ya matumizi bora ya zana za kilimo;
- Kununua tani 350 za mbegu ya mpunga kutoka kwa wakulima tani tano za mahindi, tani mbili za mtama na tani mbili za jamii ya kuende;
- Kununua na kusambaza tani 700 za mbolea TSP tani 100 na Urea tani 600 na lita 15,000 za dawa ya kuulia magugu;
- Kutayarisha mpango mkakati wa idara ya Kilimo na kupitia mfumo wa Elimu kwa wakulima;
- Kutoa elimu kwa wakulima 400 juu ya udhibiti wa nzi waharibifu wa matunda; na
- Kuendelea na kazi za kukarantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo mikarafuu.

**Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe (*UCL*)**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe, dhumuni lake kuu ni kuratibu upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe katika kaya. Matokeo ya muda mfupi yanayotarajiwa ni kufanyakazi kwa kamati za uhakika wa chakula na lishe katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia, uelewa wa matumizi bora ya chakula na kuwepo kwa mfumo wa Tahadhari ya Mapema na kuanzishwa kwa hifadhi ya chakula ya Taifa.

Mhe. Naibu Spika, viashiria vya utekelezaji wa Programu hii ni idadi ya taasisi zinazoshiriki katika *UCL*, idadi ya kamati zilizoanzishwa, kuwepo kwa kitengo cha

tahadhari ya mapema, idadi ya programu zilizowasilishwa kwa jamii, idadi ya maghala ya chakula pamoja na tani za chakula zilizohifadhiwa. Huduma za utekelezaji wa programu hii, kuwepo kwa mfumo wa ufuatiliaji na tahadhari ya mapema na mpango wa akiba ya chakula cha dharura. Huduma zinazotolewa na Programu hii ni kama ifuatavyo:

- Kuazisha hifadhi ya chakula;
- Kutekeleza mfumo wa kufuatilia hali ya lishe na afya ya shehia 24 Unguja na Pemba;
- Kujenga uwezo wa wana jamii katika kusimamia masuala ya lishe katika Shehia 37 za Wilaya ya Kaskazini (A) Micheweni na Chake Chake; na
- Kuandaa mikutano mitatu na wadau husika hujadili masuala ya kuimarisha viwango na ubora wa mchele.

Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, Jumla ya Shs. 2, 008, 236,000 katika hizo Shs. 1,648,236,000 ukiwa ni mshahara na Matumizi Mwengineyo n Shs. 360,000,000 kwa kazi za maendeleo, zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha program hii sawa na asilimia 3 ya bajeti ya Wizara.

**Programu ndogo ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii lengo lake ni kusimamia na kuhifadhi misitu na viumbe hai pamoja na mazingira yao. Viashiria vya matokeo ya Programu hii ni pamoja na ukubwa wa maeneo (hekta) za misitu iliyopandishwa hadhi kisheria, idadi ya wafanyakazi waliopata mafunzo ya ugunduzi wa moto kwa kutumia *satellite*, idadi ya hekta zilizopandwa mikoko, idadi ya ramani za maeneo yaliyopimwa, idadi ya maeneo ya uhifadhi yaliyoimarisha utalii endelevu, idadi ya vivutio/miundombinu ya utalii vilivyoimarishwa, idadi ya watalii waliotembelea hifadhi, idadi ya wanyamapori walio hatarini kutoweka, idadi ya kesi za uwindaji haramu na idadi ya wanyama vamizi waliodhibitiwa. Shabaha za utekelezaji wa mwaka 2015/2016 ni pamoja na:

- Upandishaji wa Hadhi ya maeneo ya Dole na Masingini, Jambiyani Muyuni, yenye ukubwa wa hekta 4,780;
- Kuwapatia mafunzo ya ugunduzi wa matukio ya moto wafanyakazi 5;
- Kupanda mikoko hekta 40;

- Kutoa mafunzo ya vitendo kwa watembezaji watalii katika misitu ya Masingini na Kiwengwa kufikia watalii 30,000 wanaotembelea hifadhi;
- Kufanya utafiti wa wanyama pori walio hatarini kutoweka pamoja na kuangamiza adui kunguru laki tano;
- Kuendeleza na kusimamia hekta 35,493 za misitu ya hifadhi ikiwemo na mikoko; na
- Kuimarisha utalii endelevu katika hifadhi za Serikali na kuhamasisha uhifadhi wa wanyapori adimu wakiwemo kimapunju, paa, popo wa Pemba na jogoo mwitu.

**Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina lengo la uhifadhi na usimamizi wa maliaisili zisizorejesheka kwa kuimarisha maeneo yote ya uchimbaji wa mawe, kokoto mchanga, udongo na matofali ya mawe. Viashiria vya utekelezaji katika programu hii ndogo ya pili ni pamoja na idadi ya maeneo yanayochimbwa rasmi, idadi ya hekta zilizochimbwa rasmi, Idadi ya hekta zilizorejeshewa, idadi ya tani za maliasili zisizorejesheka zilizosafirishwa,Idadi ya doria zilizofanyika, Idadi ya maeneo yaliyochini ya usimamizi wa jamii yalioendelezwa kisheria, idadi ya walengwa waliopata mafunzo ya usimamizi wa misitu ya jamii, Idadi ya hekta zilizopandwa miti ya misitu, idadi ya kaya zinazotumia majiko sanifu, idadi ya tani za asali zilizozalishwa, idadi ya hekta zilizopandwa miti, asilimia ya miche iliyostawi, idadi ya hekta zilizopandwa miti, asilimia ya miche iliyostawi, idadi ya hekta na ujazo ya miti iliyovunwa na idadi ya miti iliyooteshwa.

Shabaha ya Utekelezaji kwa Mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:

- Kukamilisha taratibu za kisheria juu ya mipango 12 ya usimamizi wa rasilimali za misitu ya Shehia;

- Kutoa mafunzo juu ya usimamizi wa misitu ya jamii kwa shehia 45;

- Kuhamasisha uzalishaji wa asali hadi kufikia wastani wa tani sita kwa mwaka;

- Kuotesha miche milioni mbili na laki tano (2,500,000);

- Kupanda miti ya misitu hekta mia tano;

- Kuimarisha na kuendeleza hekta 17 elfu za misitu ya jamii;

- Kushajihisha jamii kuongeza uzalishaji wa asali kutoka tani 3 hadi kufikia tani 6 kwa mwaka;

- Kuendeleza na kusimamia mashamba ya misitu ya serikali hekta elfu mbili, mia tano sitini na moja (2,561).

- Kuotesha miche ya misitu, matunda, mikarafuu na viongo; na

- Kuendeleza na kusimamia mashamba ya mikarafuu ya serikali, Makuwe, Daya na Gando.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Misitu na Maliasili imejitapanga kuendeleza programu ya maendeleo ya zao la karafuu kupitia mradi wa kuendeleza zao la karafuu pamoja na kukamilisha utayarishaji na uendelezaji wa program za mazao ya matunda na viungo.

Uoteshaji wa miche bora milioni moja na laki tano ya mikarafuu, matunda na viungo katika vitalu vya serikali. Kuhamasisha uoteshaji wa miche ya matunda na viungo kwa wananchi wenye vitalu binafsi. Kutoa elimu kwa wakulima wa matunda, viungo na mikarafuu, katika Wilaya 9 za Unguja na Pemba. Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mazao ya karafuu, matunda na viungo. Kufanya tathmini ya miche yote ya mikarafu na matunda. Kuanzisha program maalum ya kuendeleza zao la nazi. Kutayarisha kitabu cha muungozo mpya wa uoteshaji wa mazao ya karafuu matunda na viungo.

Programu ya Utawala, Mipango na Usimamizi wa kazi za Kilimo na Maliasili inayojumuisha Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Ofisi kuu Pemba. Jumla ya Shilingi 4,263,452,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii sawa na asilimia **7** ya bajeti ya Wizara.

Programu Ndogo ya Uratibu wa kazi za Mipango na Utafiti, kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 Programu hii itatekeleza shabaha zifuatazo:

- Kukamilisha utaratibu wa mapitio ya Sera ya Kilimo na Sheria ya Uhifadhi ya utibabu wa mimea pamoja na kutayarisha sheria ya pembejeo.Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa sheria ya haki miliki ya wagunduzi wa mbegu mpya za mimea;

- Kutoa elimu kwa jamii kupitia tovuti, jarida la mkulima nakala 2000 na vipeperushi 100 na kuvisambaza kwa wadau wote;

- Kufanya tafiti mbili za kijamii na kiuchumi ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika jamii kwa uzalishaji na tija;
- Kukusanya takwimu muhimu za mazao ya kilimo na maliasili pamoja na uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya Wizara;

- Kuendeleza mashirikiano baina ya Wizara, taasisi za ndani na nje ya nchi pamoja na kushiriki katika mikutano na makongamano; na

- Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa ufatiliaji na tathmini kwa wizara.

**Programu Ndogo ya Utawala**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, lengo lake ni Kusimamia utawala na rasilimali za Wizara kwa kufuata misingi ya Sheria. Matokeo ya muda mfupi ni usimamizi bora wa fedha, kuongezeka viwango vya elimu kwa wafanyakazi, manunuzi yenye kufuata taratibu za Serikali. Viashiria vya Utekelezaji vya programu hii ni idadi kwa hoja za wakaguzi wa ndani na nje, idadi ya shahada za wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 Programu itatekeleza shabaha zifuatazo;

- Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 100 kwa viwango tofauti;

- Kuendelea kuhakiki mali za serikali zilizokuwa chini ya Wizara ya Kilimo na kuzipatia Hatimiliki;

- Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;

- Kusimamia manunuzi ya Wizara; na

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato yayokadiriwa kuwa shilingi mia tisa sitini na sita milioni, laki tatu na tisini na tatu (966,393).

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, lengo lake ni kuratibu na kusimamia kazi na rasilimali za Wizara kwa kufuata misingi ya Sheria. Matokeo ya muda mfupi ni kuwepo kwa ongezeko la ufanisi wa kazi za Wizara ya Kilimo na Maliasili Pemba. Viashiria vya Utekelezaji vya programu kiwango cha ufanisi wa kazi za kila idara. Shabaha ya programu hii ni kuongeza ufanisi wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaomba idhini ya matumizi ya Tsh. 64,914,110,250 kwa mwaka wa fedha 2015/16 ikiwa bilioni kumi na mbili, mia nne na kumi na nne milioni la saba kwa matumizi ya program zenye kuzingatia gharama za idara na vitengo vilivyoma katika programu husika, mishahara na ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani pamoja na Jumla ya shilingi bilioni hamsini na mbili mia nne tisini na tisa milioni laki nne na elfu kumi, mia mbili na hamsini kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo. Kati ya hizo milioni arubaini na nane mia tatu na sita milioni, laki tisa sabini na sita kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi bilioni moja, mia sita na sitini milioni, ikiwa ni mchango kutoka Serikali Kuu.

**SHUKRANI**

Mhe. Naibu Spika, baada ya uwasilishaji naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo, zikiwemo nchi za Japan, Finland, Norway, Ireland, China, India, Israel, Mouritius, Korea ya Kusini, Marekani, Misri na Uholanzi.

Aidha, niayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IFAD, UNDP, FAO, JICA, UNICEF, WFP, USAID, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, *Rockfeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. Pia tunazishukuru taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo na maliasili zikiwemo ZSTC, TAHA, UWAMWIMA, ZAIDI, COSTECH, Milele Foundation, Kilimo Trust, CARE, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika T/Bara,

Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ushirikiano ya Afrika Mashariki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika,, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Napenda kuwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Naibu Katibu Mkuu wa Kilimo, Naibu Katibu Mkuu wa Maliasili, Ofisa Mdhamini Wizara ya Kilimo na Maliasili Pemba pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Taasisi na asasi zote zilizo chini ya Wizara hii, watumishi wote wa wizara paso na kuwasahau wadau wote wa sekta ya kilimo, kwa juhudi, ushirikiano, ushauri waliowezsha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara mwaka 2014/2015. Kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2015/2016.

Mwisho natoa shukrani za pekee kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja imetolwa ijadiliwe)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri hoja imeungwa mkono, tunakushukuru Mheshimiwa sasa bajeti ijadiliwe. Tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Kwanza kabla ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Haji Omar Kheir, pale alipotoa mapendekezo yake kuhusu hotuba zinazosomwa hapa wasome wenyewe wenye viti na kama hayupo awe ni Makamu Mwenyekiti. Niungane naye sana na rafikiri yangu Mhe. Haji Omar Kheir kwa wazo lake hilo.

Vile vile niombe tena maswali pale yanapojibiwa bora wajibu wenyewe Mawaziri badala ya Manaibu Waziri baada ya mchango huo Mhe. Naibu Spika, nianze.

Mhe. Naibu Spika, ifuatayo sasa hivi ni hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Makadirio ya Mapatoama matumizi ya Wizara ya Kilimo Maliasili ya Mwaka 2015/2016.

Mwanza kabla ya yote nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu

yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu ambapo leo tunajadili Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa, napenda pia kukushukuru wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, lakini kabla ya kuwasilisha hotuba hii, nami niungane na wenzangu waliotangulia kwa kutoa mkono wa pole Kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza La Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa Kufiliwa na dada yake kipenzi Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu pahala pema peponi "Amin".

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ufanisi na umahiri mkubwa katika mfumo mpya wa bajeti unaozingatia programu *"Program Based Budget"* (PBB).

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku, Mhe. Jaku.

## UTARATIBU

**Mhe. Salum Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tumo kwenye bajeti na hii ni hotuba ya Kamati na ni muhimu sana kweli kweli, lakini kasi anayokwenda Mheshimiwa hatufahamu kitu, tutashindwa kuchangia. Kwa hivyo tunamuomba asome kwa utaratibu na sisi sote tusikie.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa unakwenda *speed* Wajumbe hawasikii kitu na wanataka wachangie hotuba yako. Kwa hivyo tunakuomba uwende kwa *speed* ndogo tupate kufahamu zote. Endelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee sasa napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati wa kuipitia bajeti ya Wizara hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wake kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hija Hassan Hija - Mwenyekiti
2. Mhe.Viwe Khamis Abdalla - M/ Mwenyekiti

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hamad Masoud Hamad | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Raya Suleiman Hamad | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Asha Abdu Haji | - | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Fatma Omar Ali | - | Katibu |
| 8. | Ndg. Haji Khatib Haji | - | Katibu |

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2014 umeshuka kidogo kwa asilimia 0.4 kutoka wastani wa asilimia 13.2 ya mwaka 2013, hali ambayo imeripotiwa kusababishwa pamoja na mambo mengine na hali ya hewa kuwa mbaya. Hali hiyo imekuwa ni moja kati ya changamoto kubwa kwa Wizara pamoja na wananchi ambao wanategemea kilimo kuwa ndio utii wa mgongo wa maisha yao. Hivyo, jitihada za pamoja zinahitajika kati ya viongozi, watendaji wa sekta hii ya Kilimo pamoja na wananchi kwa ujumla ili hali ya ukuaji wa Sekta ya kilimo ipate kuimarika.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa Sekta hii ya Kilimo kwa nchi yetu, bado uingizwaji wa fedha kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kama ni msimamizi mkuu wa kuziendeleza Sekta ya kilimo umekuwa ni wa wastani tu kwani hadi kufikia mwezi wa April, 2015 fedha zilizopatikana kwa kazi za maendekleo ni asilimia 60 na Ruzuku kwa jili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani ni asilimia 45 tu.

Mhe. Naibu Spika, tathmini ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015 inaonesha kuwa uingizwaji wa fedha kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili haulingani na umuhimu wa sekta yenyewe ya Kilimo, hali ambayo imepelekea utekelezaji wa kazi za wizara hii kuwa katika mazingira magumu. Kwa mfano, Programu ya Utafiti wa Kilimo na Maliasili imepatiwa asilimia saba tu (7).

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha lakini nazungumza hivi sasa watendaji wa Wizara ya Fedha wenyewe hawapo, tuendelee Mhe. Naibu Spika.Kwa makadirio hadi kufikia mwezi Aprili, 2015. Hali hii imepelekea kwa wananchi wengi ambao wanategemea huduma mbali mbali zinazotolewa na Wizara hii kwa njia moja au nyengine wakiwemo wakulima kupungua matumaini hususan katika Sekta hii ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na uingizwaji mdogo wa fedha kwa wizara hii muhimu ya Kilimo na Maliasili, bado watendaji wa wizara hii wanaonekana kufanya kazi kwa bidii kubwa na maarifa. Jitihada za watendaji wa wizara hii zinaonekana wazi katika eneo la ukusanyaji wa mapato katika wizara hii. Taarifa zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi mia nane na arubaini na tano millioni (Tsh,

845,000,000) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, wizara ilikuwa imeshakusanya shillingi mia nane Thamani na tisa tillioni, laki mbili hamsini elfu, mia tatu na sitini (Tsh. 889,250,360) sawa na asilimia 108.

Wajumbe naomba tupige makofi kwa mashirikiano makubwa kwa Wizara na jitihada walizochukuwa kwa hapa ya makadirio ya malengo ya ukusanyaji. (*Makofi*)

Hivyo, Kamati inaipongeza sana wizara hii kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato na kukuza mapato ya serikali. Kamati inawataka watendaji wa wizara hii kuzidisha bidii ya kufanya kazi, ili mapato ya Serikali kupitia wizara hii yaweze kukua zaidi kwa mwaka ujao wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelezwa kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inakadiriwa kukusanya mapato ya Tshs. 966,393,000 kwa matumizi ya Tshs. 13,191,100,000 kwa Programu za Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara na Vitengo husika, mishahara na ruzuku kwa Chuo cha Kilimo, Kizimbani.

Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya Tshs. 34,983,200,000 zimetengwa (Tshs.33,323,200,000) kutoka kwa washirika wa maendeleo na Tshs. 1,660,000,000 ikiwa ni mchango kutoka serikalini. Jumla ya fedha kwa ajili ya Programu zote za Wizara ya Kilimo na Maliasili ni Tshs. 48,174,300,000. Aidha**,** Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imejipangia kutekeleza Programu Kuu 3 ambazo ni;

- Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
- Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu; na
- Programu ya Utawala.

Mipango na Usimamizi wa Kazi za Kilimo na Maliasili ambapo katika Programu hizo kuu kuna Programu Ndogo tisa (9) kama zilivyofafanuliwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii iliyowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu hivi punde. Kamati inaitaka Wizara kuwa makini sana na matumizi ya fedha zitakazoingizwa katika Programu hizo kwani licha ya uhaba wa fedha, matokeo ya fedha zitakazoingizwa yatahitaji kuonekana na kupimwa ufanisi wake.

**Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usarifu wa Mazao, Kizimbani**

Mhe. Naibu Spika, hapa Kamati ilipata masikitiko makubwa sana katika utendaji wake kazi.

Mhe. Naibu Spika,  kwa kuwa kituo cha Usarifu wa Mazao ni muhimu sana kwa wakulima pamoja kwa wadau wengine ikiwemo Taasisi ya Viwango (ZBS). Na kwa kuwa ukamilishaji wa ujenzi wa kituo hicho umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu sasa. Na kwa kuwa ujenzi wa kituo hicho umeshafikia hatua kubwa za ujenzi wake.Na kwa kuwa mashine na vifaa kwa ajili ya kituo hicho vimekaa bure kwa muda mrefu vikisubiri kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho.

Hivyo basi Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo wakati wa kupitia bajeti ya Wizara hii iliamua kufanya marekebisho katika baadhi ya sehemu za makadirio ya matumizi katika kazi za maendeleo kwa kupunguza fedha katika baadhi ya miradi na kuzielekeza fedha hizo katika Mradi huo wa Ujenzi wa Kituo cha Usarifu Mazao, Kizimbani. Marekebisho hayo yanalengo la kutenga fedha zipatazo Tshs. 400 millioni kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Kituo hicho.

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo naomba nirudie tena kwa umakini wa hali ya juu kwa faida ya wananchi pamoja na serikali.

Mhe. Naibu Spika,  kwa kuwa kituo cha Usarifu wa Mazao ni muhimu sana kwa wakulima pamoja kwa wadau wengine ikiwemo Taasisi ya Viwango (ZBS). Na kwa kuwa ukamilishaji wa ujenzi wa kituo hicho umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu sasa. Na kwa kuwa ujenzi wa kituo hicho umeshafikia hatua kubwa za ujenzi wake. Mashine na vifaa kwa ajili ya kituo hicho vimekaa bure kwa muda mrefu vikisubiri kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho. Hivyo basi Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo wakati wa kupitia bajeti ya Wizara hii iliamua kufanya marekebisho katika baadhi ya sehemu za makadirio ya matumizi katika kazi za maendeleo kwa kupunguza fedha katika baadhi ya miradi na kuzielekeza fedha hizo katika Mradi huo wa Ujenzi wa Kituo cha Usarifu Mazao, Kizimbani. Marekebisho hayo yanalengo la kutenga fedha zipatazo Tshs. 400 millioni kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Kituo hicho.

Mhe. Naibu Spika**,** marekebisho hayo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Katika Programu ya Maendeleo ya Kilimo, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji ilikuwa jumla ya Tshs. 25,938,742,000 katika Programu hiyo Kamati ilipunguza Tshs. 140,000,000. Naomba Mhe. Kaimu Waziri ukaanza ku-note hivi vitu maana hapa pahali pazito kidogo utakuja kupata shida katika uchangiaji. Aidha, kamati pia imefanya marekebisho ya kupunguza fedha katika Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Mali Zisizorejesheka, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu katika Programu Ndogo hii kamati imepunguza Tshs. 60,000,000 kati ya Tshs. 360,000,000.

Kamati pia imefanya marekebisho katika Programu ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Kilimo na Maliasili, Programu Ndogo ya Mipango na Utafiti katika shughuli ya "Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo jumla ya shughuli hii ni Tshs. 4,218,863,000 Kamati imepunguza Tshs. 100,000,000 na katika Programu ya Mendeleo ya Kilimo, Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo katika Programu Ndogo hii Kamati imepunguza Tshs. 100,000,000 katika shughuli ya Programu ya Utafiti wa Kilimo na Maliasli jumla yake ilikuwa ni Tshs. 300,000,000.

Mhe. Kaimu Waziri hapa kidogo hapa shughuli itakuja kuwa pevu Kamati haikuridhika na utendaji huu.

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UTAFITI NA MAFUNZO YA KILIMO**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti unaoikabili Taasisi hii, Kamati inashangazwa sana kuona kuwa Taasisi hii imefanywa kama kijitengo tu cha Wizara wakati Taasisi hii imepewa nguvu na mamlaka ya kisheria ya kutekeleza majukumu yake. Kamati imegundua kuwa tangu mwaka 2012 ilipopitishwa Sheria ya kuanzisha Taasisi hii, Taasisi hii imekuwa ikifanyakazi bila ya kuwa na Kanuni wala Baraza lake ambalo linatakiwa liwepo kwa mujibu wa Sheria hiyo. Hali ambayo inaifanya Taasisi hii kufanya kazi zake katika mazingira magumu kiutendaji na kifedha.

Hapa ipo shughuli Mhe. Kaimu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mapungufu hayo Kamati inaitaka Wizara kutoa maelezo ya kina na ya uhakika na yaweze kufahamika kwa sababu zilizopelekea wizara kushindwa kukamilisha Kanuni za Sheria ya Taasisi hiyo ya Utafiti wa Kilimo hadi hivi sasa. Aidha, Kamati inaitaka Wizara itoe kauli mbele ya Baraza lako Tukufu juu ya lini Kanuni za Sheria ya Taasisi hiyo zitakuwa tayari ili Taasisi hiyo iweze kufanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu za Sheria, kwani kukosekana kwa Kanuni hizo kumesababisha kutokuwepo kwa Baraza la kusimamia Taasisi hiyo. Mhe. Naibu Spika, hapa pana shughuli vile vile.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ambapo sekta hii ina jukumu la kuwashirikisha wananchi katika kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na mafanikio makubwa yanayopatikana katika Idara hii bado kuna baadhi ya changamoto zinazoikabili Idara hii hususan katika sekta ya misitu na maliasili zisizorejesheka kwa kujitokeza baadhi ya wananchi waharibifu wanaotumia misumeno ya moto kwa kukata miti na kupelekea athari kubwa za kimazingira.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipokea taarifa ya kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 misumeno ya moto iliyoripotiwa ni jumla ya 400 kati misumeno hiyo ya moto 200 ni kwa upande wa Unguja na 200 kwa upande wa Pemba. Hapa imekwenda sawa sawa, pamoja na hayo, Idara hadi wakati huu ilifanikiwa kuikamata misumeno ya moto 90 tu. Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri ......

**Utaratibu**

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Msomaji hapo ilikuwa asome taarifa na kama ana mchango wowote baada ya taarifa atoe mchango wake, anaharibu ripoti yote.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe kwanza taarifa ya Kamati halafu utaomba muda utatoa mawazo yako, usichanganye humo humo. Kwa hivyo ukimaliza utaomba utapewa muda utatoa mawazo yako. Kwanza soma maoni ya kamati.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi ninafikiri angefatilia, mimi ni mjumbe wa kamati ndio nikaja kukaa huku mbele nikaanza kusoma, sasa asije akatia aibu kufatia gari mwendo wake haujui, inaweza ikamuangusha.

Wizara hii pamoja na Serikali kwa ujumla kuweza kushirikiana na masheha wa Sehemu husika na kutoa elimu kwa masheha hao, kutotoa vibali kinyume na taratibu za Sheria ili kuweza kupunguza upotevu wa maliasili hizo ambazo ni muhimu kwa Taifa, kwani baada ya utafiti wa kina Kamati imegundua baadhi ya masheha wana uhusiano wa karibu na watu wenye misumeno ya moto.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya

Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2015/2016, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae waweze kuipitisha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba uniruhusu kwa dakika 5 kuchangia mchango wangu hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, nianze na shamba la Makurunge; shamba letu la Bagamoyo. Kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi akiwemo Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na Waziri wa Kilimo kwa jitihada alizochukua na baadae suala hili mimi nikalifikisha bungeni na naomba nilinukuu kama nilivyosema:-

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha shamba la mifugo ya ng'ombe huko Makurunge Bagamoyo baada ya kupata ridhaa ya Serikali ya Muungano kupatiwa shamba mnamo mwaka 1976 Suala:

a) Je shamba hilo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;
b) Je, Serikali inaweza kuonesha hati miliki ya shamba hilo ambapo kwa muda mrefu haijulikani ukweli pamoja na vikao vingi kufanyika bila mafanikio; na
c) Kuna ugumu gani wa kutoa hati ya umiliki wa shamba hilo kwa tangu mwaka 1976, hati ya kumiliki ardhi ya shamba hilo haijatolewa.

Hili suala limefika Bungeni na hatimaye mwezi huu taarifa nilizopata tarehe 30 Juni baada ya kubishana kwa mabishano makubwa hati hii iko tayari. Alipojibu swali hili Naibu Waziri wa Ardhi Angela Kariuki, alikubali tarehe 30 Juni ataikabidhi hati kwa wahusika Wizara ya Kilimo, hili suala lifatilieni lishafika hatua kubwa pamoja na viongozi wetu na waheshimiwa wabunge kule kulihakikisha vizuri ni jambo la kutia moyo. Ingawa kuna hekta kama 20,000 zimeshatolewa zimebaki hekta 6,000 kwa muda huu. Huo ndio mchango wa mwanzo Mhe. Naibu Spika.

Baada ya hapo nije katika bonde la mpunga la umwagiliaji maji Muyuni, pamoja na kuwa Wizara imejitahidi kujibu hoja hii katika vitabu na hotuba iliyoletwa hapa lakini hali hii ni ya muda mrefu kweli. Kisima imetokea kikawa na chumvi lakini huu karibu mwaka wa pili na hakuna hatua yoyote inayoendelea. Na hivi sasa ukizingatia kilimo ndio uti wa mgongo wa wananchi ukizingatia sasa kila kitu madukani kimepanda bei.

Mchele sasa umepanda bei haijulikani, sukari imepanda bei haijulikani, unga wa ngano, kilimo wanakitegea sana wananchi, suala hili ni la muda mrefu

ninamuawakilisha yule mpiga kelele katika Kamati na wananchi wa Muyuni hivi sasa wanasikia hawajui hatima yao, angalau mwende mkawape elimu kule wananchi wa Jimbo la Muyuni. Kuna tatizo gani hivi sasa. Huu ni msaada wenyewe waliotoa pesa karibu milioni 350. Mimi ninashukuru sana ndugu zetu wa Japan kwa msaada huu kupitia kwa Mbunge na Mwakilishi Jimbo la Muyuni.

Sasa wizara niiombe hebu iende ikatoe darasa ikawafahamishe wale watu kimya kimekuwa cha muda mrefu, kisima kimekaa maji ya chumvi muda mrefu, hakuna hatua yoyote hawajui kinachoendelea huu mwaka wa pili. Kweli hapana pahala pengine pa kuchimba, hakuna hatua nyengine ya kufanya, bidhaa zote zimepanda. Hapa nitakuwa mgumu sana katika kupitisha vifungu.

Suala la Kituo cha Kizimbani ninafikiri tumezungumza sana, nije katika kilio chengine, fedha milioni kumi na tano kweli Wizara imeshindwa kwa ajili ya kutengeneza kilimo cha mikarafuu. Vile vile Serikali ningeishauri ipendekeze angalau ingefungua dirisha dogo la PBZ kwa ajili ya wakulima. Tatizo kubwa wakulima wetu wanaumia sasa hivi hali ya uchumi hairidhishi, bidhaa zote zimepanda kwa hali ya juu kutokana na *rate* ya dola ilivyo juu. Kwa hivyo Wizara ichukuwe suala hili la kuanzisha Benki ya Wakulima japo dirisha, *otherwise* wananchi watazidi kuumia kwa hali inavyokwenda.

Jengine kidogo kwa hali ya Pemba ilivyokwenda kufanyakazi Kamati kidogo, mimi nimepata masikitiko baada ya wananchi kutokuchimbiwa/kuburugiwa mabonde yao kwa sababu ya kutokuwa na pesa. Hili jambo ilikuwa mmefikiria wale wananchi ingawa pesa zenyewe zile kidogo ikawa kwa matrekta mawili wamepewa Kikosi cha KVZ kwa mkopo. Ikawa wananchi wale nao wangefikiriwa angalau kulimiwa yale matrekta yao, shilingi ngapi baada ya kulipa mpunga ule baadae wakaja wakalipa lile deni. Kutoa matrekta mapya, kilimo hivi sasa kimekua tabu.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaendelea na mchangiaji mmoja mmoja, nina wachangiaji watano, ataanza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, afatie Mhe. Hamad Masoud na Mhe. Bi Raya Suleiman Hamad ajitayarishe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kunipa nafasi ya mwanzo katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo lakini kabla hujawasha *stop watch* yako naomba dakika moja tu, nipitishe haki niliyokuwa nayo ndani ya nafsi yangu.

Jana Mheshimiwa wangu Waziri wa Elimu amenipa cheo kikubwa sana cha u-*brigadier*. Nimshukuru sana Mhe. Waziri na nimpongeze sana kwa cheo kile ambacho alichonitunuku na akathubutu kunipa saluti, leo Zanzibar nzima inarindima kutokana na uwezo alionipa Mheshimiwa wangu waziri. Ninamshukuru sana Mhe. Waziri na niombe wenzangu leo tutakapopitisha tusimpigie buti kutokana na heshima kubwa aliyonipa kijana wake. Lakini Mheshimiwa nilikuomba kuna kopo nne zile za rangi, ukiondoka niambie leo nikufate zile kopo 4 za rangi ili uweze kunisaidia katika lile lengo nililokutajia jana na kuwaonea huruma wale walimu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika hotuba hii, wizara hii ni kubwa sana na mara nyingi sana hupenda sana kuzisemea wizara zilizokuwa mihimili mikubwa. Afya, Wizara ya Kilimo na Wizara nyengine nitaikumbuka baadae ikiwemo na hii kilimo chenyewe na Wizara ya Elimu. Mihimili mikubwa sana na hasa katika watendaji wake.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii msomi wa chini basi ana cheti, wizara hii ina watu *PHD*, ina watu *master*, ina watu wenye *degree*, ina watu wenye diploma, ina watu wenye cheti ndio nasema hao ni watu wa mwisho. Kwa nini Mhe. Naibu Spika, nikathubutu kusema hivyo nikawagawa watu nikawaeleza jinsi gani wizara hii ina watu wa aina hiyo, halafu wataniuliza wazanzibari kwa nini, sababu ninazo kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, tukiwa leo tuna watu wana ma-*PHD*, tuna watu wana *master*, tuna watu wenye ma-*degree*, kuna watu wenye vyeti na taaluma nyengine ambazo zinoelekea na vyeti zinoelekea na kwenda kwenye *PHD* halafu leo Mhe. Naibu Spika, kuwa bado Zanzibar tuko katika hali ya mwisho kabisa ya masuala ya Kilimo, inasikitisha sana. Inasikitisha kwa sababu gani Mheshimiwa mazingira ya hawa watendaji wetu hatujawatendea haki, tuna wataalam wazuri sana lakini ukiangalia mazingira ya kifedha ya kimshahara iko duni sana. Wakivuka Dar hapo tayari wanakwenda kula mshahara mkubwa sana. Hili suala linasikitisha na ndio maana kwa sababu nikikwambia hali halisi, hasa nilitegemea mimi Zanzibar tutakuwa na nchi yenyewe ilivyokuwa ni ndogo halafu ardhi yetu Mheshimiwa kwa utafiti mimi *brigadier* utafiti wangu nimefanya ardhi yetu bado ingali ina rutba nzuri.

Lakini nasema hatujajipanga hasa katika *level* hizo za hawa niliowataja, hatujajipanga kabisa. Wanaumia hawa katika utendaji wao wa kazi. Hili ukweli tuuseme tusifiche. Mheshimiwa kweli hawa tungeliwatengeneza vizuri, wana vitu vizuri sana hawa, *wallahi* tusingekuwa masikini. Mshahara wa *PHD* ukenda Dar es Salaam hapo ndio wanapata fedha za mshahara na mtu mwenye cheti inasikitisha kwa sababu wanatembea hawa, tuna udugu wizara zinatembeleana hizo

wanafahamu wananon'gonezana wale, tutakimbiwa na siku zote Kilimo Zanzibar tutaendelea kuwa duni, tuwe *serious* na suala hili hasa katika kilimo.

Tumesema kilimo ni uti wa mgongo lakini utapindika huo, ma-*specialist* hao wanakwenda zao watashindwa kuutibu. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana Serikali na hasa leo msimamizi hasa mkuu wa Serikali kaka yangu Mhe. Mohammed Aboud ni mtu mmoja ambaye anapenda sana maendeleo, atasikiliza kilio hiki atajaribu na yeye kutoa *proposal* yoyote kwa kumpelekea Rais kuangalia mapitio mapya ya mishahara yao hawa wataalam hasa kutokana na Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, leo tuna mabonde mengi sana ya mpunga, mabonde yetu bado ya mpunga kwa utafiti tu mdogo mdogo bado yangali yana nguvu kabisa, lakini tatizo linalotukuta kutokana na vianzio, vitendea kazi halikadhalika, Mheshimiwa bado vingali duni sana.

Mhe. Naibu Spika, leo niseme safari ya matumaini ya mradi ambao tunaotaka kuuleta Zanzibar wa kuwezesha wakulima wa mpunga katika mabonde ya Kilombero, Pangeni, Upenja pamoja na wenzetu jirani zetu wa Cheju, umaskini kwaheri sasa hivi. Na mimi si *professor* ni *brigadier* tu, *brigadier* ni mtu shujuaa, *brigadier* ni mpiganaji, Mhe. Shamuhuna nakusalutia na mimi vile vile.

Mhe. Naibu Spika, angalia sasa mimi ni *brigadier* lakini ninatafuta nyenzo ya kuweza kupigana kwa kuwagomboa wazanzibari katika umaskini wa kilimo cha mpunga, Mheshimiwa tumepata kampuni ikisimamiwa na Mkurugenzi wa *Vigor* ambaye kwa jina lake anaitwa Ndugu yangu Tofiki, tayari tumefika pahali pazuri nimshukuru sana Naibu wa Wizara hii. Nimshukuru sana Naibu mwengine wa Wizara hii tulikuwa pamoja katika *meeting* kwa kuwapokea wafadhili na kuwasikiliza nini wanachotwambia. *Wallahi* inasikitisha sana, alitwambia kuwa Zanzibar bado tuna uwezo wa kulima mpunga wa kutosha, nimefarijika sana. Sasa hivi trekta ziko njiani, si chini trekta 100 wakati wowote mambo yakikamilika mikataba Mheshimiwa trekta zinaingia hapa na utaziona.

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze sana na Katibu wao, wameukubali wameupokea na tukakubali kukaa pamoja na ndio inavyotakiwa neema ikija lazima uikumbatie sifa inakwenda kwa nani, kwa Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Waziri na Naibu Waziri na Wakurugenzi. Sisi baadae mkitaka tena ndio tunaanza kupata nani kachochea jambo kama hili. Watafiti wetu wamezunguka katika mabonde yetu yote niliyoyataja hapa; Kilombero, Pangeni, Upenja, pamoja na Cheju yenyewe. Wamegundua kuwa uwezekano Mheshimiwa wa kupatikana mpunga ambao unozalishwa Zanzibar kwa asilimia nzuri kabisa, Mheshimiwa jamani matumaini yapo.

Mhe. Naibu Spika, wazee wetu walikuwa wanalima mpunga wa kujitosheleza wao wenyewe hawendi upande mwengine hata wa kununulia dagaa hana, anaula hivi hivi kwa sababu kwa kuwa ni mpunga mpya inawezekana kula hivi hivi bila ya kupata dagaa. Lakini dhana ya kampuni hii sasa hivi unapata chakula chako na unapata pesa ya kununulia samaki ndani na maendeleo unayapata. Na baadae kampuni ile ile utakuwa na *share* yako mwenyewe itakayokusaidia uzeeni pamoja na watoto Mheshimiwa, hiyo ni neema. *Alhamdulillahi* Zanzibar sasa waheshimiwa sisi wengine tunafarijika, yaani tukiona mambo kama haya Mhe. Naibu Spika, tunafarajika sana, na ndio maana nikasema kwamba si mchezo wizara hii ina wasomi wazuri, kila siku zikicha wana-*search* mambo mazuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nisione tabu kusema kwa kuwapongeza sana kwa sababu unajua kuna wataalamu, yaani nikisema kwamba Zanzibar tuna uwezo wa kutengeneza maziwa kwa njia ya kokwa za mafenesi zinatokana na wao, sio mimi. Haki ya Mungu Mheshimiwa, watu wanashangaa sana kwa kuwa ni suala jipya Zanzibar Mhe. Waziri, unaye-*act* hiki sio kitu, mashine zipo na ninakwambia Mheshimiwa, niombee dua Mungu akinijaalia nikirudi nazileta mashine za kutengenezea, nimeshamaliza *research*. Matumaini ya watu wa Jimbo la Kitope sasa wao watatengeneza mapema maziwa haya, maziwa ya kokwa ya fenezi, maziwa ya kokwa ya boga, maziwa ya kokwa ya doriani. Kokwa ya doriani ni *first quality* tena yana bei kutoka nchi za nje. Hivyo, tunangoja nini, hao wataalamu wetu wamo humu kwenye hiki kitabu Mhe. Waziri, ni hawa tu hakuna wengine, hawakutoka Ulaya hawa ila wamo humu humu, tunawadharau hatuwapaishi vizuri. *Wallahilaadhim* mimi nimepata wapi vitu kama hivi Mheshimiwa, lakini ninacheza nao kabisa na wako karibu.

Mhe. Naibu Spika, sisemi kwa kutania, maana yake brigedia hasemi kwa kutania, akisema anasema la ukweli. Ninawahakikishia nitaanza *example* katika Jimbo la Kitope tutatengeneza maziwa ya aina hiyo, nimeshaulizia mashine, India zipo. Mhe. Mwanasheria Mkuu, weka sheria sasa tuweke kazi na tumalizie.

Mhe. Naibu Spika, lakini haitoshi hayo na hii yote tunafanya nini, ni kwamba tunakuza uchumi wa Zanzibar, tunataka kuondoa umasikini hata majani haya ya karafuu Mheshimiwa, ni moja katika mafuta *best,* hicho si kitu cha mchezo tena utashangaa sana, si mchezo Mheshimiwa, dhana hii mkiikosa, kichwa hiki cha brigedia shauri yenu nakwambieni, kwa sababu vitu vipo na tunavyo ndani ya uwezo wetu. Sasa mimi nakwambia suala jengine Mheshimiwa, leo vijusi vile rangi ya kijani ukipeleka nje ni dola 50, uki-*organize* vijana leo huwatariji hapo. Kuna kaa mnazi, sijui kama wanawajua watu wengine kaa mnazi, kuna kaa anafua anazi kabisa, adimu Zanzibar. Watu wanacheka kwa sababu Mheshimiwa, hawafatilii, ndio maana nikakwambia mimi Mhe. Shamuhuna, hakupoteza kunipa

jina hilo, hawafuatilii, kaa mnazi anafua nazi si kitu cha mchezo, ukimuwekea kidole chako hapa anakikata.

Lakini leo wako wachache, sasa tungeweza kuwakusanya vijana kwa njia za ushirika na tukawapa mradi ule, Mheshimiwa, nani atakufa masikini kitu *very simple* kabisa. Sasa Mheshimiwa, nimeamua mwenyewe kutoa *example* katika Jimbo langu la Kitope. Nitawa-*approach* vizuri muda ambao nitaingia tena madarakani nitawa-*organize* vizuri, nitahakikisha kuwa kwa muda wa mwaka mmoja Kitope kila mtu atakuwa anamiliki na wao magari yao, watamiliki kwa kupitia misingi ya *projects* kama hizi.

Sasa Mheshimiwa mambo kama haya ikienda na jimbo jengine na jimbo jengine tuko wapi Zanzibar, itakuwa tuko mbali sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa, naomba sana kwa kuwa wizara hii ni wizara ambayo imejipanga sana hasa katika taaluma.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 27 Idara ya Umwagiliaji Maji, hebu angalia Mheshimiwa, sasa ukiangalia sasa hivi hali halisi ilivyo hatujasimama vizuri. Nilitegemea sana hapa tutakuwa tunazalisha sana, lakini kampuni inayokuja itawakusanya watu mpaka Bumbwisudi tutawatafuta, tutakaa nao vizuri, tutawaelimisha na wao, tutawapatia zana zote za ukulima kwa wakati. Unajua Mheshimiwa, tatizo letu dogo hatupati kulima mpunga kwa wakati, basi, tatizo dogo tu Mhe. Naibu Spika, na serikali lazima tuisaidie sisi wananchi. Serikali wafadhili lazima itie mikono yao kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, matrekta sasa hivi nani asiyejua kwamba matrekta, ni ghali sana, tunachelewa kwa matrekta ni kidogo sana. Kwa hiyo, tungekuwa tuna matrekta mengi Mheshimiwa, basi ningekwambia sasa hivi *Alhamdulillah.* Sasa hii kampuni itakuja na matrekta yake kama mia moja na kuendelea huko mbele ya safari na *power tillers* zake na mambo mengine na vile vitrekta vidogo vikawa kwa wale wanaoshughulikia mambo ya umwagiliaji maji na wao watapewa vitrekta vyao vya kuweza kufanikisha malengo hayo.

Mhe. Naibu Spika, niishukuru sana kampuni hiyo na walivyoniahidi wamesema kuwa kabla ya uchaguzi wakimaliza tu masuala ya mikataba basi wataanza kuleta vifaa ambavyo vya kujitayarisha mwaka huo wa mbele wa ukulima wa mpunga. Hili kwanza Mheshimiwa, niwashukuru sana na wamejitahidi sana katika masuala haya ambayo tumekusudia kutaka kuwasaidia sana.

Mhe. Naibu Spika, huu ukurasa wa 25, Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Mheshimiwa, mimi ndio maana nikasema hii ina watu wenye fani nyingi sana, nani asiyejua kwamba kuna umuhimu wa binadamu kuwa na lishe hapa, nani asiyejua? Lakini kutokana na hali halisi ilivyo lazima Mheshimiwa, hiki kitengo tuweze

kukisaidia na kusaidia kwake makubwa ni masuala ya fedha tu, hakuna kitu chengine chochote, yaani masuala ya fedha lazima tuweze kuwatilia kwa asilimia ambayo inalingana na wao.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Idara ya Misitu, hapo ndio kwenye wataalamu. Mheshimiwa, idara hii imesheheni wataalamu hapo, maana yake niseme kwamba hapa kuna wataalamu wengi sana, wengine wanasubutu hata kutengeneza dawa za mijiti. Lakini Mheshimiwa watu kama hawa ni adimu katika nchi za wenzetu Ulaya, si kitu cha mchezo watu kama hawa, mtu leo kwenye *department* tu mtaalamu anaweza kutengeneza kwa kutumia misitu, kwa kutumia mijiti yetu wenyewe ya Zanzibar ku-*product* dawa ambazo zinaweza zikasaidia, huyu mtu adimu sana katika nchi zetu. Lazima wizara iringie, wizara ijivunie kuwa nae mtu kama huyo, Mheshimiwa, lazima wizara ijivunie kabisa, mimi namuonea choyo.

Simuonei choyo kwa kumuonea choyo, namuonea kwamba na mimi kwa nini Mungu asinipe nikaujua utaalamu ule, ndio choyo chenyewe ninachokipenda mimi hicho, sitafuti jini nikampachika yeye kwa kuwa anajua, aah, hiyo Mungu atanisuru kwa yeyote atakayekuja, hata mtu akija jimboni mimi simpigi jini mwache aje tu mwenyewe, lakini tushindane katika *activities* za kazi. Ndio inavyotakiwa, uje pale ujitangaze nini utawafanyia wananchi kama nilivyosema kwamba nawafanyia wananchi moja, mbili, tatu, kama hili moja nilitangaza kuwa nawaondolea umasikini kwa ajili ya mpunga, wewe njoo useme utawaondolea umasikini kwa ajili ya nazi, lakini si kuchukua jini ukampachike mtu, Mungu atakufanya nini, atakumaliza na wewe duniani au anakusubiria huko.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana nilisema masuala ya sheria, kwa kuwa sheria ndio zitakazoweza kulinda misitu yetu. Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana sheria hizo zingali ziko vizuri na zinalindwa vizuri na sasa hivi hata ule ukataji unakuwa ni mdogo sana.

Mhe. Naibu Spika, bado sheria ya hawa wanaovuta sigara wakaturushia vichechea katika misitu yetu ikaungua, bado sheria ni nyepesi, hawa ndio sasa hivi wanatutia mashaka ya roho. Wale wanaokata kata misitu wamekuwa kidogo tofauti na zamani, zamani Mheshimiwa, kipindi hiki kinachoanzia Ramadhani "afanaleki kufa hakuna breki", Mheshimiwa, msitu ukikaribia kipindi kama hiki msitu unalia,eee.Lakini kwa kuwa sasa hivi Mheshimiwa, sheria ipo, si mchezo nimshukuru sana Mhe. Mkurugenzi yuko *active* vizuri kwa sheria, tunamuharibu sisi tu viongozi na ni kweli kwa sababu na sisi Mhe. Naibu Spikam atakujia mtu wako mnyonge keshafanya makosa, utafanya nini Mhe. Mwakilishi, itabidi uende tu huna njia ya kufanya.

Mkurugenzi lakini hivyo hivyo usimuache, mpige hivyo hivyo, ata akikubali wewe jua limetua na huondoki mtupu lazima umlipie faini ambayo inayolingana na ile kesi yenyewe. Hilo namshukuru sana Mheshimiwa tena namshukuru sana utusaidia hivyo hivyo tutafanya nini sasa na sisi ndio hivyo tunataka kura kwa wananchi. Lakini usikubali tukavusha sheria hapo uwe mgumu, uwe na nadharia. hii kesi ina uzito gani hata kuweza Mheshimiwa, umsaidie, ukiona ngumu binya Mheshimiwa, hapo mimi nakushukuru sana anaitekeleza. Mhe. Waziri, Mkurugenzi halali analinda msitu, halali analinda malighafi ambazo zisizohamishika ambazo zinatuletea tija kwa kukamata watu. Mhe. Naibu Spika, sijapata kuona Mkurugenzi mjasiri kama huyu, nampongeza sana, tena sana pamoja na watendaji wake, kwa sababu ana timu nzuri, ana wataalamu wazuri, sio akili yake inachangiwa na wataalamu wake na anapanga vizuri kazi.

Mhe. Naibu Spika, leo *Alhamdulillah* tizama mikarafuu kwenye vitalu sasa hivi tumeona humu kwenye kitabu, nimeona mwenyewe Mheshimiwa, kwa pozi kabisa amekaa Mhe. Waziri, anapata *lecture* hapa, anaambiwa hapa sasa hivi tuna mikarafuu si chini milioni moja na zaidi tunayo hapa, anaringa yote ni sifa hiyo. Sasa hivi ndio inavyotakiwa, lakini Mheshimiwa, nimeamini kama Zanzibar ardhi yetu ni nzuri, leo Mhe. Naibu, nae yupo hapa nae anapozi hapa, anaonesha jinsi gani *sunflower* linaweza likazaliwa ndani ya Zanzibar, lakini tatizo letu moja Mhe. Naibu, tunaanza tunaishia mwisho mbaya, sijui kwa nini.

Hebu angalia shuke hili lilivyojitoa hapo kwenye kitabu, Mheshimiwa, kapozi kabisa, lakini leo sidhani kama *organization* hii inaendelea katika vijiji vyetu, sidhani kabisa njooni tukusaidieni jamani. Mhe. Katibu huu ndio utendaji tunaomba sana Mheshimiwa, tizama shuke, nimekwenda Dodoma sijaona shuke kama hili *Wallahi laadhim* kumbe yanakubali sana Zanzibar, mafuta ya alizeti. Jamani *cholesterol* nyingi tunaomba sana alizeti tunaambiwa mafuta haya hayatii *cholesterol* ndani tumbo kutokana na mafuta haya ni mazuri sana. Kwa nini tusishajihishe, watu wengi sasa hivi wanapata maradhi chungu nzima kama *pressure*, kisukari kutokana na mafuta mabovu, naomba Mheshimiwa, sana.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba hii kampeni iendelee kwa nguvu zote, tukijipanga tunaweza, tukilala tumelala, tuwatumie hawa hawa wataalamu wetu tusiwaachie kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa, ninaomba sana nitoe ushauri kwenye Idara ya Misitu, brigedia anasema sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara ile nimefanya *research*, mimi mwenyewe ya ghafla tu akiwemo mwenyewe Mkurugenzi kwa sababu na yeye ana vitu yule, lakini kwa kuwa kiti kinamnyima uhuru wa kumwaga zaidi basi ningeomba tuunde *teamwork*. Tuunde timu Pemba na Unguja na kwa hizi *activities* ambazo

nilizozisema mimi kwa muda wa mwaka mmoja au kwa muda wa miezi kadhaa huko mbele tuweze kufanikisha. Sasa iweje sasa?

Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi atoe wataalamu wake, ofisi sasa ile isiwe tena ya kukalia watu waondokane na ofisi sasa hivi na nakuhakikishieni kama atafanya hivyo nikifa nitilieni fatha tu jamani eeh, brigedia amekufa *minalfaidhina* Mungu amlaze mahala pema *Inalilahi waina ilayhi rajiun* tumalize. Sasa ile Mheshimiwa, ndio itabakia hiyo ndio kawaida yetu hapa sisi basi, eeh, tena ndio unakwenda na amali ile kwa sababu watu hawajui unaposaidia kila binadamu kwa sababu kiongozi mtu mkubwa sana, si kitu cha mchezo, hatuutizami uongozi huu. Uongozi ni jambo kubwa hata kwa Mwenyezi Mungu ameusimamia uongozi na atakuuliza wewe ulikuwa Mwakilishi ulitekeleza nini kwa wananchi wangu, kwa waja wangu. Sasa ukishindwa kusema tuh unakula rungu, sasa nalo hilo tuwe *alert* nalo kwa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, aondokane na ofisi ende katika shehia hadi shehia au nilivyokusudia wilaya *include* na shehia zenyewe akatoe mafundisho Mheshimiwa, sasa hivi yakuweza vitu ambavyo vitaweza kutupatia tija na inawezekana, *wallahi* Mhe. Naibu Spika, inawezekana sana tu. Mbona wanatoa taaluma sasa hivi ya nyuki, tizama sasa hivi hawatajwi karibu na sisi tutatoa tani kwa tani. Mheshimiwa, angalia sasa hivi hii misitu si wengine hawa, wanaelimisha watu kutengeneza nyuki, lakini iko *slow* sana, kusema la ukweli.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sababu nimezieleza mapema hapo wanakuwa wanavunjika watu wetu hawa, hebu tuwatengenezee mazingira tuwaeke *special* posho wakitoka *out* katika vijiji waekewe *special* posho ya kujikimu katika utekelezaji wao, halafu leo njoo mnambie kama hatukuweza kufanikiwa. Kwa sababu leo wenzetu Bara sasa hivi wana asali za kila aina, lakini kiasi chao wale watakuwa kwa sababu huyo mtu wao akiuinua mguu tu kaekewa fedha, akiinua mguu na akienda mbele kaekewa fedha, sisi leo wetu yule pale hamna kitu atafanyaje, atabakia kutizama vitabu hatimae muda umeisha haoni.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mheshimiwa, ushauri wangu Mhe. Mkurugenzi auchukue wakiambatana na Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Mkuu wakae jamani watuoneshe hiyo misingi hiyo, inawezekana bila ya tatizo lolote. Kwa hivyo, Mheshimiwa, mimi napenda sana lakini nione huku kuna mashine ya kukaushia, kweli kukaushia mazao, mimi niseme na nilicheka sana siku hiyo, *Wallahi* kuna mambo mengine hasa yanasikitisha sana. Tungule zinalimwa Matemwe ndio *official* yake, lakini *Wallahi* nimezikuta Spain tungule za Matemwe, nimezikuta katika *Supermarket* tungule za Matemwe tena ni ghali kweli, ni nne tu kwa *Euro* 4 tena zimetiwa kwenye kiplastiki, mimi nimeshangaa hee imetoka Matemwe

imefika kule, zile ndogo ndogo *Wallahi* mimi kitu kile kimenishangaza sana tena zimenunuliwa kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, niwezesheni jamani nikauze, nitakwenda na jamaa zangu wa Matemwe wapo hapa, Abdi Mossi yuko wapi ameingia mitini. Nitakwenda kuwaambia kuwa jamani eeh, tulime hizi si kitu cha mchezo. Halafu jengine nililoliona mimi nilishangaa sana tukenda pwani kule tunaita wale wanaotafuta chaza wale, tunamwita jogoo kama mnakumbuka, tunaikuta ile jogoo ile refu tunaseha ah, ana dharau, ndio nini kutuletea majogoo huyu. Leo nje pesa, huyo jogoo wako tunayemdharau hapa pwani ukampita na ukamkiyuka usichokoe chaza yule ukachukua mwengine, leo wenzetu pesa kule.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana, namuomba Mkurugenzi wangu niite brigedia wako nikusaidie kwa sababu na yeye ananisaidia, ananisaidia fikra na mawazo, ananisaidia kunipa taaluma na ndio maana nikawa nina *speed* yakuweza kufanya jambo la msingi, ninaloliokota nakwenda kukaa na wao katika *labor* yao tukawa tunazungumza na tukapanga nini nifanye katika maisha ya leo.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa, anikubalie hili na atengeneze *teamwork* kwa kuendea ofisi tuziache sasa hivi, mimi naomba sana Mhe. Waziri, waambie ofisi sasa hazina maana tena twende kwenye wananchi ndio kwenye mambo. Tukifanya hivyo Mheshimiwa na hili unajua tatizo liko wapi? Tatizo hata sisi mawaziri tunajisahau tuseme ukweli mawaziri wanakuwa wanajisahau, nikisema nafanya *evaluation* hapa nani anayekwenda katika *activities* zake kwa muda wa mwaka mmoja anakwenda mara ngapi, nitakosa jibu hapa, sitaki leo huko, tuingie huku kwa sababu wote nawapenda mawaziri wangu, lakini kidogo kidogo lazima tuambizane ukweli, kofi moja moja tupigane kidogo, naamini kutakuwa hakuna jibu. Sasa tukiwa hatuna jibu waziri hashuki, huyu wa chini anafanya nini na yeye anabweteka kwa kuwa anaona kile kiwango alichokipata hakijamridhisha.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mkurugenzi wangu kwa hilo naamini kabisa ataweza kunisikiliza na kuweza kufanya ile kazi na hiyo itamuwekea sifa yeye, unajua watu wengi sana wanashindwa kuweka kumbukumbu katika *department* zao, kwa sababu kumbukumbu ni muhimu sana hata atakayekuja na atakayekuja, tena ni muhimu.

Juzi Mhe. Ali Mzee Ali, profesa alitusomea sheria iliyokuwa nyuma masuala ya elimu bure, alituonesha hapa gazeti sijui la Kumekucha, mimi hata nia ya kuzaliwa siijui na sijui nitaumbwa lini. Lakini kumbukumbu imesaidia imeletwa hapa hadharani. Mhe. Ali Mzee Ali, Mwenyezi Mungu amuweke, imeletwa hapa na sote tumeona katusomea sote hapa. Mimi sipengi kumpa sifa mtu aliyokuwa hana hata

siku moja, ninampa sifa ambayo anayo na inaonesha katika hadhara ya watu. Hilo naambiwa mimi safi sana kabisa.

Mhe. Naibu Spika, unapokuwa katika sehemu hata kama viongozi, hata sisi Wawakilishi kwenye jimbo ukiondoka pahali watu walie waseme aa, tumemkosa mtu fulani, tutafanya nini ndio mambo imefika hatima, kwa sababu tayari katika lile jimbo umewekeza kwa wananchi, kila wakitizama wanaona Balozi, wakitizama wanaona Makame Mshimba, wanamuona mtu mwengine, hivi ndivyo inavyotakiwa Mheshimiwa. Lakini leo unaondoka wewe peu, hamna kitu watasema nini wananchi, wana hiari waseme bora uchaguzi uwepo haraka sana ili pawe na mabadiliko.

Kwa hivyo, mimi nawaambia hii Mkurugenzi itamuwekea sifa sana, itampandisha chati. Kwa sababu hata Marais, Rais anaangalia *CV* za watu, utendaji wa watu, acha kusoma tu, maana kama ingekuwa kusoma yule pale Mhe. Haji Omar Kheir, mwenzangu lakini *active* nzuri zimezidi vizuri tu, *Wallahi* huwezi kuamini kabisa. Mimi sikuamini kabisa shemegi yangu yule kama atakuwa zaidi na wengine wapo wazuri, lakini nasema kutokana na ile hali halisi kigezo cha mtu, msiingie wivu na nyinyi wazuri, lakini tunakwenda kwa daraja nitakupeni na nyinyi sifa zenu moja moja huko mbele ya safari, ukweli ulivyo. Mhe. Naibu Spika, naomba sana wawe katika kuweka kumbukumbu ya hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, nitoe ushauri wangu mwengine, sasa wananchi wanachimba michanga, tumesema anapomaliza mtu kuchimba mchanga waifanye ardhi iwe na rutba upya, hili usimamizi wake uko mdogo sana. Ninaomba sana Mheshimiwa, natoa ushauri wa bure kwanza kabla mtu hujamtangazia wakati umeshajua kwamba huyu ndiye atakayechimba kesho, anajitayarisha unamwita mapema mnafunga mikataba ya kuwa akubali amri ambayo itaweza kuwa ardhi ile atairudisha tena kama alivyoikuta kwa kupanda miti, *otherwise*, kashindwa yule mtu ondoa, katisha. Mheshimiwa, hiyo itatusaidia sana, Mkurugenzi kwa hilo sidhani kama mtu atamfumbia macho kwa sababu hatari hiyo na hatari baadae, kisiwa chenyewe kinajulikana ni maji na tuwe na *level* ya *deep* kwenda kuchimba chini. Kwa sababu kuna kipindi fulani watu walichimba mpaka maji yanatoka, tishio.

Kwa hiyo, mimi namuomba sana Mkurugenzi kwa hili asilifumbie macho hata siku moja na mimi namuamini. Mkurugenzi wangu anacheka kwenye ncha ya ulimi, lakini *be careful* naye baba. Utamuona anacheka lakini wee, yuko *strict* sana na sheria, ukiondoka pale wembe ule ule anakamata sheria, hiyo ndio sifa ninayompa. Lakini hii ni hali ya hatari...

**Mhe. Naibu Spika:** Malizia dakika tano.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Nishaona mkono namalizia usiwe na wasiwasi. Mhe. Naibu Spika, hii ni hatari, sheria ya Mheshimiwa ni lazima li-*stick* katika wakati wake, aifanyie hiyo asikubali. Mhe. Waziri, hili suala msikubaliane sio hao tu, wakati wa mawasiliano nao nitasema lao, lakini na wao wanachimba kifusi nitasema lao. Lakini hapa ninasema kwa sababu kila siku watu wanachimba mchanga na kila ukiangalia mpaka leo mahoba, mwisho utakuta hatari watoto wanazama, maji yakiwemo mle, juzi tu Kazole mtoto kazama kwa sababu yale mashimo yaliyochimbwa hayana hata mti pa kujizuia mtu, ni suala linasikitisha sana.

Kwa hivyo, naomba sana hili lisifumbie macho, hawezi mtu achana naye mtafute mtu mwenye kuweza kufanya hilo jambo mara moja.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie. Kulikuwa na mradi wa umwagiliaji maji kati ya Kilombero, Pangeni na Upenja, tulifikia katika *stage* ya mwisho ya kuweza kufanikisha mradi huo na nilitegemea bajeti hii nitaambiwa tayari uchimbaji unaendelea na tayari utafiti umekamilika. Nimesema jamani kwamba sasa hivi sisi tunaunda safari ya matumaini ya watu wetu kupata utajiri katika jimbo letu la Kitope kutokana na ukulima. Sasa leo mtanambia nini suala hili, mje kunambia vizuri kwamba tayari tumefikia pahali, tayari kuna tatizo hili, ili tuweze kusaidiana kwa sababu umwagiliaji wa mpunga maji na huyu mwekezaji akija ni kazi rahisi sana ni kama tende kwa uji au niseme kahawa kwa haluwa, ni rahisi inateleza tu Mheshimiwa, wala huoni uchungu wa kawaha. Sasa mimi ningeomba sana nipate jibu muwafaka.

Mhe. Naibu Spika, namalizia nimshukuru sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri, Naibu Katibu Mkuu wake na Manaibu wake wawili mashujaa nao niwashukuru sana, pamoja na Wakurugenzi na watendaji wote waliokuwepo juu pale, wengine wamejificha lakini ndio mambo. Mheshimiwa, naomba niwapongeze sana kutokana na kupamba kitabu hiki, niwaombe Waheshimiwa wenzangu tuwasaidie, tuwapigie debe kwa sababu nalo muhimu, ni muhimili mkubwa sana sehemu ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kuna vijana pale Upenja waliwahi kulima masuala ya mboga mboga na tuliambiwa watasaidiwa, lakini mpaka leo sidhani serikali kama imesaidia, tumewasaidia sisi kama viongozi wa jimbo, lakini na serikali iliahidi pale alipokwenda Mhe. Rais wakati ule Mhe. Amani Abeid Karume wakasema kuwa watasaidiwa. Kwa sababu pale Upenja lililimwa bilingani mimi kichwa changu kidogo, huamini utasema limetoka Bara, kumbe tunaweza tukiwasaidia, tunaweza ku-*product* vizuri, tuwatafutie na masoko. Mheshimiwa, tunaweza lakini tatizo nirudie tena hatujawawezesha wataalamu, ndio tatizo lenyewe kubwa.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana naunga mkono na wenzangu tuunge mkono wizara hii kwa *style* yake. Jana nilitoa *one fifty,* leo natoa *two hundred* kwa asilimia naunga mkono. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Nimekupa muda mrefu kwa sababu na wewe ni mwana kilimo.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa nataka kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa awali wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kama hotuba ilivyosomwa na kaimu waziri, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe, mimi nimekuwa Mjumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo tangu *August*, 2012 hadi leo hii ni karibu miaka mitatu. Nimejifunza mengi katika miaka hii mitatu katika kamati hii na wizara hizi tatu. Miongoni mwa niliyojifunza ni kuona kwamba pamoja na kuwa serikali inapiga kelele kwa mdomo mpana na sio serikali tu, ni uhalisia wa jambo lenyewe kwamba sekta ya kilimo kwa ujumla wake ndiye muajiri mkuu wa Wazanzibari, zaidi ya asilimia 75 ya Wazanzibari wenye akili timamu na nguvu zao za kufanya kazi wameajiriwa na sekta hii. Hata wengine wanasema kwamba; "Kilimo ndio uti wa mgongo".

Sasa kama kilimo ni uti wa mgongo basi uti wa mgongo lazima uenziwe, uhifadhiwe, utunzwe, ulindwe na uthaminiwe, lakini inaonekana ni maneno tu. Katika jambo linalonisikitisha katika wizara hii ni kuona serikali, mimi nasema serikali kama vile wizara hii ni mtoto wa kambu.

Mfano mdogo tu katika taarifa ya kamati yetu kuna mahali imeandikwa hivi na ndivyo ilivyosomwa;

"Mhe. Naibu Spika, tathmini ya bajeti ya wizara hii kwa mwaka 2014/2015 inaonesha kuwa uingizwaji wa fedha kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili haulingani na umuhimu wa sekta yenyewe ya kilimo, hali ambayo imepelekea utekelezaji wa kazi za wizara hii kuwa katika mazingira magumu. Kwa mfano, programu ya utafiti wa kilimo na maliasili imepatiwa asilimia saba tu ya makadirio hadi kufikia Aprili mwaka huu".

Mwaka umekwisha, Aprili ni *quarter* ya mwisho ya bajeti, utafiti, maana yake kilimo pamoja na yote katika wizara ambayo ina tafiti nyingi ni Wizara ya Kilimo na Maliasili, unaambiwa mpaka Aprili mwaka huu *Seven percent*. *Seven percent* ni 0.07. Hii katika mahesabu una-*ignore one percent* haukufika halafu unasema

kilimo ni uti wa mgongo na ni kweli inaajiri zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wa nchi hii, maneno mengi vitendo hakuna.

Mhe. Naibu Spika, kingine ambacho nimejifunza katika miaka hii mitatu kwa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili ni kwamba watendaji wa wizara hii kuanzia Katibu Mkuu na huku, hawa ndio watendaji, Waziri na Naibu Waziri si watendaji, ni wasimamizi wa sera, ni viongozi wakuu wa wizara, lakini hawa ni wasimamizi watendaji ni hao. Nilichojifunza katika miaka hii mitatu ni kwamba ujasiri na uzalendo kwa watendaji hawa ndio unaoonyesha kwamba wizara hii ipo kabisa. Kuna mambo mengine yamefanyika tunawauliza nyinyi hamtoi pesa, mbona hili limefanyika? Wanasema "Funika kombe mwana haramu apite", hapana, tusifunike kombe, twambieni, wanatwambia bwana bora tusiwaambieni, wanahangaika huku na huku wanajituma, lakini wapi! Ni usanii wa Afani? Sio, hapana ni vitu vinaonekana kweli. *(Kicheko)*

Kwa hivyo, mimi katika hili sitaki niendelee sana *message* yangu imefika, kilimo ni uti wa mgongo isiwe kwa maneno ila iwe kwa vitendo.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii miaka ya nyumba ilikuwa ni wizara inayoonewa choyo na wizara nyingi kwa wataalamu walivyokuwa wengi, ilikuwa Wizara ya Kilimo na Mifugo hii zamani. Sasa Waheshimiwa, tumegundua kwamba katika wizara hii kuna *erosion* kubwa sana, mmong'onyoko mkubwa sana wa wataalamu. Hapo awali tulikuwanao kina Mhe. Ali Juma Shamuhuna, Dr. Mwinyihaji Makame, kaka yangu namtaja hapa Kassim Biwi, nasema ni miongoni mwa wataalamu waliokuwa wanasifika katika Wizara ya Kilimo na Mifugo. Sasa hili ni wimbi la wanaostaafu wataalamu ni wengi mno na mna maeneo mengi *replacement* haijafanyika. Nashauri kama ni Wizara ya Elimu au ni kitengo gani lakini kuna umuhimu wa kutupa jicho si la huruma aa, la ulazima kui-*replenish* Wizara ya Kilimo kwa wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, sababu zimetolewa kwamba hatuna wanafunzi wanaosoma sayansi na kilimo ni sayansi ni kweli, lakini tutawapata tu kwani hapo zamani wakipatikanaje? Skuli ziko vile vile, kuna *Primary*, kuna *Secondary*, kuna *Collages and University*, watu ni wale wale. Sasa basi watu hawa washajihishwe kuwe na vivutio vya wanafunzi kupenda sayansi ili wanafunzi hao hatimaye tuwapate katika kilimo, mifugo, ujenzi na hizi idara ambazo zinahitaji sayansi zaidi kuliko *art*.

Sasa nakuelezeni tu kwamba *erosion* hii ya wataalamu inakwenda na kwa sababu ikifika umri wa kustaafu inabidi uondoke, sasa hakuna machipukizi na nafikiri hata huyo Katibu Mkuu wenyewe ambaye na yeye vile vile mtaalamu, sijui ana muda gani wa kustaafu. Yeye kapata ukatibu mkuu ni mtendaji lakini zaidi kwenye *desk*,

lakini wale wenyewe hasa walioko kwenye *field* ndio ninaozungumzia mimi hapa. Kwa hivyo, serikali itambue kwamba wataalamu katika Wizara ya Kilimo na Maliasili tutafikia mahali hawapo tena.

Mhe. Naibu Spika, pauro tuliite pauro, ukweli tusiufiche. Mimi katika miaka hii mitatu nimeona kwamba kilimo cha umwagiliaji maji kina umuhimu mkubwa sana, mpunga ni maji japo kidogo. Wenyewe wanajua kuna mpunga unalimwa juu, kuna mpunga unalimwa bondeni. Lakini vyovyote itakavyokuwa lazima maji yapatikane kama mboga mboga, huu wa juu upate maji na huu wa bondeni upate maji na ndio maana kukawa na *irrigation*. *Irrigation* ni kilimo ambacho saa zote mimea inatakiwa iwe na maji, maji tu yanategemea wakati mwengine maji ni kidogo lakini suala la unyevu unyevu lazima liwepo.

Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe, mabonde yote ambayo tumekwenda yale ambayo *irrigation* yenyewe, umwagiliaji wenyewe unafanywa kwa visima virefu ambavyo munaingizwa *pumps* za maji, ambazo lazima zipate umeme, ukifanya mahesabu *is almost impossible.* Gharama za umeme kwa wakulima wa bonde moja zinafika mpaka 1.3 bilioni, pia hata gharama hiyo ukiigawa ukiwaambia wakulima changieni haiwezekani kabisa na ukifanya mahesabu kama watachangia umeme na hicho wanachokipata basi hasara ni kubwa mno kuliko tija.

Mtu atasema kwamba lakini serikali inafidia, kweli serikali inafidia ni sawa. Lakini serikali inafidia ipate hasara. Kama wewe gharama zako za kupata kilo hamisini za mchele au za mpunga ni shilingi elfu sabini; gharama ya kupata polo moja la kilo hamisini za mpunga, ukizijumlisha zote zile kuanzia kulima kwa trekta, kuburuga, kupanda, maji hayo ya *irrigation* inayotokana na visima ni shilingi elfu sabini, sasa si bora ukanunue mbeya. Kwa sababu kilo hamsini za mbeya sana zitakugharimu elfu sitini.

Wewe umetumia elfu sabini na sio elfu sabini tu mbali na gharama nyengine pengine umelima na ukajikata kwa panga, pengine umekwenda kufanya shughuli za pale umepata matatizo, hayo hayamo kabisa. Sasa kwa alie na akili, anaefikiri, anaefanya mahesabu na unyonge huu uliotuingia wa masikini. Bora pesa zako zile elfu sitini ukanunue mchele ule bukheri wa hamsa ishirini.

Kwa hivyo, mimi katika hili kilimo cha umwagiliaji maji kwa kutumia visima vya maji na umeme ni ghali kupita kiasi. Nashauri inawezekana kabisa kwenye kilimo hasa cha umwagiliaji maji na mabonde tuliyonayo na wanatwambia watu wa kilimo kwamba mabonde tuliyonayo Unguja na Pemba Kibokwa, Mtwango na Bumbwisudi haya kama kweli yanalimwa kitaalamu na mbegu nzuri, umeme wa

uhakika na kwa hivyo, maana yake ni maji ya uhakika. Tunaweza tukatoa mchele wa kutosha kwa matumizi ya Zanzibar na ikiwezekana mwengine ukasafirishwa.

Sasa kwa nini hatuendi kwenye Programu wa *Public Private Partnership* (*PPP*), isiwe kwenye viwanda tu, isiwe kwenye miundombinu mingine ya Bandari, hata kilimo *PPP* inawezekana. Kama bonde lina wakulima elfu moja. Mimi naamini wako wawekezaji wanaweza kabisa mabonde haya wakayachukuwa pamoja na wakulima wenyewe ukafanywa utaratibu wakulima wenyewe wakanufaika zaidi kuliko wanavyonufaika hivi sasa.

Sasa mimi natoa shauri huo na naamini kwamba *investors* wapo kama hawapo watafutwe, kama unatafuta *investor* wa ku-*invest* kwenye *Airport* na Bandari, kwa nini tusitafute *investor* waku-*invest* kwenye mabonde wa mpunga. Ukishapata *investor* serikali haitalipa tena gharama ya umeme kwa wakulima wa umwagiliaji maji *never*, serikali hawatachimba tena visima, serikali hawatajenga tena miundombinu. Tumekwenda mahali huu ni mwaka wa tatu ile *channel* tu ya kupita maji kupita kwenye kisima kupeleka kwenye mabonde huko mwaka mzima panajengwa mita 250, tatizo nini fedha hakuna.

Kuna bonde la Mkoani kule ilifika mahali tukawambia Wizara ya Kilimo kama hali ni hii hakuna kinachokwenda na Programu imekwama, basi wapeni wakulima wenyewe wafanye wanavyotaka; wakulima mchicha alime, wakulima mihogo walime. Lakini ardhi imezuiwa msifanye hivi, kuna hichi na kila siku inakuja hichi, hakionekani. Huku na huku pakatatuliwa kidogo na kweli *Alhamdulillah* unakwenda pale ambapo pametatuliwa mpunga ni mzuri tu, maeneo mengine yote bado na naamini na hayo nayo yatachukuwa muda mrefu.

Mimi nashauri Wizara ya Kilimo mbele ya Baraza hili mtafute *investors* na maamini wako, mabonde yote haya yafanyiwe *Public Private Partnership* (*PPP),* yaani mradi wa wakulima wenyewe na wawekezaji kwa pamoja. Nifahamike vizuri hapo, yaani wakulima wenyewe iwe ni sehemu ya mradi ule, sio wakulima kuwaondoa na akapewa *investors* akalima, sisemi hivyo nasema *Public Private Partnership.* Wakulima wote wanajulikana Wizara ya Kilimo na wanaorodha ya wakulima wote katika mabonde yote, hao washirikishwe kikamilifu na naamini *investor* akipatikana, tija itakayopatikana ni kubwa kuliko tija inayopatikana sasa hivi kwa wakulima hawa.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kiasi miaka mitatu au minne nyuma kumejitokeza ukulima mpya kidogo wa mboga mboga *green houses*, yaani nyumba za kijani. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, siku moja wakati anajibu maswali ya asubuhi alituarifu kwamba *green houses* si *project* ya Wizara ya Kilimo rasmi. Lakini Wizara ya Kilimo kama watu wa kilimo na wao vile vile wanashiriki vizuri katika kuwaendeleza hao wanaofanya kilimo hicho.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tumetembelea baadhi ya *green houses* tumekwenda Dimani kabla ya kamati hii kulikuwa na Wajumbe, mmoja namkumbuka ni Mheshimiwa Mwakilishi wa Mkoani. Tumekwenda tukajionea sote tukashangaa eneo dogo la mita kumi na tano kwa mita nane lilozungushwa hiyo nyumba yenyewe inayoitwa *green houses* namna mitungule ilivyotapangwa na sisi tulikwenda wakati ule tungule tayari zinaanza kuiva. Huwezi kabisa kuamini na wataalamu wakatwambia kwamba gharama ya nyumba hii walitwambia milioni sita, lakini mavuno yake huku ile nyumba ikawa bado imebaki ni karibu milioni hamsini.

Kwa sababu mtungule unaopanda unaendelea kuvuna kwa muda wa miezi sita na kila mtungule unatoa angalau kilo mia tano. Sasa angalia ni mitungule mingapi katika eneo hilo kwa ufupi hesabu alizotupa ni kama milioni hamsini. Sasa kama una-*invest* milioni sitini, pamoja na utaalamu wote na shughuli zote maji, mbegu, utaalamu tumia milioni ishirini, ukipata milioni thalathini basi una hamsini milioni.

Sasa pamoja na kwamba si mradi rasmi wa Wizara ya Kilimo, mimi nasema kwa manufaa ambayo wameonekana Mheshimiwa Mwakilishi wa Mkoani alipewa bilingani mkono mmoja hakuweza kulishika ilibidi mikono miwili, kwa vile lilivyokuwa kubwa akapigwa na picha, hiyo ni *green house*, tulikuwa na hizi *cucumbers* wengine waliingia mle wakatoka walifikiri ni majoka, yaani vile vilivyokuwa vimenawiri vingi tu.

Sasa tunaweza kabisa tukaondoa uagiziaji wa matango, tungule, mabilingani, bamia na vitu vingi. Tumekwenda kuoneshwa mahali ambapo pamepandwa matikiti huamini, yaani matikiti yamekaliana kama mawe hivi, hivi kweli inawezekana hii, tunaambia sio inawezekana ndio imewezekana. Mboga mboga ni ghali, sasa hivi tuna mahoteli zaidi ya mia mbili wote wanahitaji, tena mbolea yenyewe inayotumika ni *organic* na siku hizi duniani watu wanapenda sana vitu ambavyo mbolea yake ni ya maumbile sio hii *chemical*.

Kwa hivyo, tunaweza tukawa na soko kubwa sana la mboga mboga na matunda. Naishauri kabisa Wizara ya Kilimo iwe na *special interest* na wakulima wa *green houses* na iwe ni mradi rasmi kabisa, kuwe na kitengo maalum kwa ajili ya shughuli hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ni Mjumbe wa kamati hii mambo mengi tumeelezana katika kamati yetu, lakini si mara nyingi kutamka kuunga mkono bajeti yoyote. Lakini hii nitamke kwamba naiunga mkono asilimia mia moja. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Ahsnate Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana huu wataala* alietujaalia, akatupa uzima na pumzi tukaweza kufika katika Baraza lako tukufu.

Na wewe nakushukuru vile vile kwa kunipatia nafasi kidogo Mheshimiwa na mimi ni Mjumbe wa kamati wala sitaki niharibu mazuri aliyoyazungumza Mjumbe mwenzangu nitazungumza kidogo na kuweza kuiunga mkono.

Vile vile, nimshukuru Waziri wetu, niwashukuru watendaji, Makatibu pamoja na watendaji wake wote na wizara zote zinazohusika. Vile vile, nimshukuri waziri wetu Mhe. Sira Ubwa Mamboya, kwa mashirikiano mazuri pamoja na katibu wake na Mwenyezi Mungu amjalie ampe nafuu kwa haraka tuweze kuja kujumuika katika kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo tunasema kwamba ni Wizara mama kwa watu wote hayuko hata mmoja aliekuwa hajapita katika kilimo. Masikitiko ya Wizara ya Kilimo tuliyonayo kwa kila tunapokwenda kuwatembelea ukiingia katika kilimo, ukiingia katika utafiti kuna ukosefu wa pesa. Pesa hazitoshi hazikidhi haja licha ya juhidi walizonazo basi angalu kile wanachokiomba watimiziwe sio atake milioni mia, agaiwe milioni arubaini tushakwenda kulikuta hilo na hichi ni kilio kikubwa. Wapewe fedha zao waweze kufanya yale waliyoyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, ukija katika miradi hawa wanavuka malengo kwa miradi yao tunakwenda kutembelea miradi mbali mbali katika Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo, tunawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awajaalie wawe na moyo wa kujenga uwezo na kuweza kujitolea katika nchi hii ili tuweze kupata mafanikio ya nchi sote kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kukagua hata barabara walizozijenga Wizara ya Kilimo na tukatoa ushauri kama kamati, lakini juzi nasema hapa Barazani nimekwenda mimi na nimezipita njia zile. Kwa kweli mvua iliyonyesha tayari ile hasara imerudi pale pale. Kwa sababu tulitoa ushauri angalau ilirashiwe lami kwa wembamba lakini tukaambiwa mkandarasi anajenga kwa kifusi.

Mheshimiwa, niliptia njia ya Mchanngamdogo kutokea Mzambarauni nilipita juzi, tayari ile njia inaharibika. Kwa hivyo, tunaomba katika miradi yao watakapoiomba angalau wakishaweza kuifanya basi serikali iweze kuwasaidia. Barabara zile wamezijenga lakini mawasiliano wangalishirikishwa wakaweza kuweka angalau lami nyembamba basi tungelipata miradi na ikaweza kudumu.

Mhe. Naibu Spika, halafu mimi nitakuja katika utafiti. Mheshimiwa, watafiti wetu ni wataalamu tuliokuwa tunawatamania kuweza kutufanyia utafiti wa mambo

mbali mbali; zikiwemo mbegu, udongo katika mashamba na hata mimea ile ikiingia wadudu lazima tupate hawa watafiti. Katika kuwatembelea Chuo cha Utafiti Kizimbani tulipokwenda pale, hawa na wao ukosefu walioulilia ni mkubwa ni kuwa pesa wanazozipata hazikidhi haja na wengi ni kama aliyoyasema Mhe. Hamad Masoud Hamad, tuliwakuta ni watu wazima na watu ambao wanaweza karibuni kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba Chuo cha Kilimo kitakaposomesha na wakawapata watafiti hawa Mheshimiwa, waweze kuajiriwa haraka bila ya wale bado hawajastaafu ili waweze kuwapa zile vitendea kazi wanavyotenda wao mpaka wakaweza kunufaisha yale mambo na yakawa ili na wale watoto wapate nyenzo kwa kusoma lakini wapate nyenzo za maarifa kwa wale watu wazima waliomo mle.

Mhe. Naibu Spika, halafu mimi nasema katika utafiti watakapofanya utafiti wa udongo, tujue ni shamba aina ngapi udongo uliokuwa haufai na ni aina ngapi za udongo uliokuwa unakubali kwa mazao mbali mbali. Hapa ndipo tutakapojua kama tayari kuwa mimi shamba yangu nitalima kitu fulani na mwezangu atalima kitu fulani, isiwe kwamba pakishafanyiwa utafiti watu waweze kupumzika, tunaona mazao mbali mbali yanavyoharibika ikiwemo migomba, hayo maboga aliyoyasema Mhe. Hamad Masoud Hamad, yanaingiwa na wadudu, ukipanda maboga yako yakizaa basi pengine unaweza kupata mazima mawili, yote yaliyobakia yanaweza yakaharibika.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba wawezeshwe na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie wawezeshwe na waweze kufanya taaluma hii iweze kutupelekea mbele kwa sababu mwanadamu ni chakula. Ukisema nanunua tu iko siku utakuwa pesa ya kununulia huna. Lakini utakapokuwa na kilimo chako kitakusaidia. Halafu kwenye utafiti wa mbegu za mpunga. Tujue mbegu wanazozifanyia utafiti kwa sababu kuna mbegu hizi ndogo ndogo zikija mara ya mwanzo utafikiri mbegu ni hizi, lakini ikifika mwaka wa pili mbegu ile inatoweka wala huna kitu chochote utakachokipata.

Tunaomba tufanyiwe utafiti kwa mbegu ambazo zinachukuwa kwa udongo wa ile shamba itakayolimwa jinsi kama watu walivyokuwa wakilima zamani. Mheshimiwa, zamani tulikuwa na mbegu za aina mbali mbali na tukilima wala tulikuwa hatuna mabwana shamba, wala hatuna watafiti na watu wakivuna. Wakivuna mbegu zilikuwa ni mbegu za zamani za asili na mbegu zile sasa hivi zimetoweka tumeingiwa na mbegu hizi mpya, lakini mbegu hizi kwa muda mdogo zinaondoka, ni sawa sawa na mbegu zilizokuwa haziwezi kustahamili ukame.

Sasa tunaomba katika watafiti wetu ndani ya utafiti wao wajue mbegu hii ni ya kudumu na iweze kufanyiwa kazi watu waweze kuitilia maanani na kuweza

kufanyia kazi. Mheshimiwa, changamoto tulizoziona kwa watu wa kilimo. Watu hawa wanajitihada kubwa ya kufanya kazi zao, lakini kuna mashamba mengi yaliyoathirika kwa kuingia maji ya chumvi. Sasa tunaomba Bajeti yao Wizara ya Kilimo, jamani usifumbatwe mkono ukunjuliwe, walioona watoto tusiwe na mkono wa buli, tuwe na mkono ukunjuke ili waweze kuzifanya zile kazi walizozikusudia na waweze kutuondolea sisi matatizo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, halafu mimi niwapongeze tu walitwambia mabwana shamba wamesoma na wamehitimu na wamewasambaza. Lakini tunataka tujuwe ni bwana mashamba wangapi walioko katika vijiji walijitangaza na wakulima wakawajua kama hawa ni mabwana shamba.

Mhe. Naibu Spika, anakaa bwana shamba katika kijiji anamaliza miaka mitano baadhi ya watu hawamjui. Kwa sababu kuna watu wanalima hivi sasa hivi nikikueleza huu msimu huu wa kilimo watu walituuliza hao mabwana shamba ndio wepi, lakini tulipokwenda kilimo tuliambiwa Ole yupo, sijui wapi yuko, bibi shamba na bwana shamba.

Tunaomba mabwana shamba hawa na mabibi mashamba watakapopelekwa vijijini wawe karibu na wananchi kuweza kuwaelekeza Mheshimiwa ili waweze kufanya zile kazi zao za kilimo zinazotarajiwa kuweza kupunguza umaskini katika jamii.

Halafu Mhe.Naibu Spika, kuhusu umwagiliaji maji. Wizara hii mimi ninaipongeza sana licha ya changamoto wanazozipata, lakini kidogo wamesukuma gurudumu lao na wanaweza. Tunaomba watakapopewa bajeti yao vile vile na wao waweze kupewa bajeti itakayokidhi mahitaji kwa sababu kilimo cha umwagiliaji maji walivyotueleza wenyewe kina gharama kubwa.

Mhe. Naibu Spika, hayo mabonde aliyozungumza Mhe. Hamad, tulikwenda. Mimi katika mabonde niliyoyatembelea basi Makombeni ilinimaliza. Tulikwenda *site* ndogo tu wananchi waliyoilima na wakapewa juhudi ya kuweza kupewa mafundisho, lakini kwa kweli mpunga ulishika ukenda hutaki utazame pahala pengine kwa mpunga ulivyoshika, mpaka sisi wenyewe pale tuliingiwa na ragba tukawaambia tukatieni alau kipande kipande tuje tulime jinsi ule mpunga ulivyoshika.(*Makofi*)

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunaomba katika haya Mawizara watakapofanya kazi zao, Wizara ya Kilimo iwezeshwe ili waweze kuwawezesha wananchi na kuwapatia taaluma ili waweze kufanya yale mambo tunayoyakusudia na sisi vile vile tuweze kupata tija katika nchi hii. Bila ya kilimo hufanyi kazi, bila ya kilimo husomi, bila ya kula huwezi kufanya kitu chochote Mhe. Naibu Spika, ninawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile mimi ni mwana Kamati na hii Kamati yetu imesomwa, katika michango yetu tuliyoichangia basi namuomba Mhe. Hija Hassan Hija, asizuie kifungu kwa sababu haya yaliomo humu katika hichi chote tulikaa nao, tukatoa maoni, tukakubaliana na ndiyo tukisha tukaandika hii. Kwa hivyo, naomba asiwazuilie kifungu.

Mhe. Naibu Spika, hivyo mimi ninaiunga mkono asilimia mia kwa mia na Mwenyezi Mungu akitujaalia naomba wenzangu waiunge mkono ili ipite na waweze kufanya yale mambo wanayohitajia.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Raya Suleiman Hamad. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mohammed Haji Khalid baadae Mhe. Bikame Yussuf Hamad na baadae afuatie Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kusema machache sana katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha asubuhi hii kufika hapa katika kazi zetu za kawaida. Pia, nimpongeze Kaimu Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wale walioleta kitabu hichi kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ni moja katika Wizara ambayo haina bahati. Bahati yake ni ndogo, ni finyu na nyembamba. Katika miaka mitano hii kama sikosei ni bajeti moja tu ambayo ilisomwa na Waziri wa Kilimo hasa, nyengine zote zinakaimiwa, hii ni bahati mbaya sana kwa Wizara hii. Kwani bajeti moja tu kama sikosei iliyosomwa na Waziri wa Kilimo mwenyewe, nyengine zote zinakaimiwa. Kwa hivyo, ni bahati mbaya kweli kweli kwa Wizara hii ambayo ni muhimu mno katika maisha yetu. Sijui kuna mchawi gani katika Wizara hii hata ikawa kila mara inakaimiwa tu au sijui hawa Makaimu ndiyo wachawi. (*Makofi/Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyojieleza kuwa kilimo ni Wizara ambayo au kilimo katika ujumla wake ndiyo chenye waajiri wengi ya Wazanzibari. Hata sisi tuliomo humu wengine ni wakulima, pamoja na shughuli zetu nyengine zote tunazofanya lakini na kilimo ni sehemu ya shughuli zetu. Kwa hivyo, kilimo kimechukua watu wengi katika ajira. Lakini pamoja na kuwa wengi tumejiajiri katika kazi za kilimo, bado tunaishi katika maisha duni kabisa. Tuna upungufu wa chakula, tuna upungufu wa fedha na wengi wa Wazanzibari wanashindwa kumiliki milo mitatu ambayo mwananchi anahitajia, pamoja na kazi ngumu tunayoifanya ya kilimo na shughuli nyengine mbali mbali, lakini bado watu walio wengi hawajafikia lengo la

kujikimu kimaisha. Kwa nini, kwa sababu sekta ya kilimo haijapata umuhimu unaostahiki.

Kila mtu anasema pale kuwa kilimo ni uti wa mgongo. Hata Mhe. Hamad, kasema pale kuwa uti wa mgongo ni *back born* ya kitu chochote, ni kitu ambacho ni *very sensitive*, lazima kienziwe, kitunzwe na kiangaliwe kwa umakini sana ili huo uti wa mgongo uweze kufanya kazi zake vizuri. Sasa ili kilimo kiweze kutoa tija, lazima kiwe na wataalamu wenye taaluma ya kilimo, kama ni umwagiliaji iwe na wataalamu wa umwagiliaji, kama ni kilimo cha juu kuwe na wataalamu watakaoelekeza wakulima namna ya kilimo hicho cha juu au kilimo cha maweni, kama ni kilimo kinachostahamili ukame kuwe na wataalamu ambao wataelekeza wakulima kulima mazao ambayo yanaweza kustahimili ukame.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Wizara hii lazima ipambwe na wataalamu wa fani mbali mbali za kilimo ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Vyenginevyo, uzuri wake utamaliza katika vitabu na mapicha mazuri yanayoonekana katika vitabu vyenyewe. Lakini lengo halisi litakuwa halifikiliwi kama Wizara hii haikuwezeshwa. Wanawake wanasema wanaweza lakini tunaposema wawezeshwe wenyewe wanasema wanaweza. Je, hii Wizara ya Kilimo inaweza au iwezeshwe. Ninadhani kwa Wizara kama haikuwezeshwa haiwezi. Hivyo, Serikali iwe na *interest* maalum ya kuwezesha Wizara ya Kilimo ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kama walivyojipangia katika vitabu vyao vya bajeti.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika kitabu hichi kwenye ukuaji wa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa. Kitabu hichi kimeonesha kuwa pato hilo la Taifa limepungua. Mwaka juzi 2013 walikuwa na asilimia 30.4, mwaka 2014 ni asilimia 97.9. Kwa hivyo, pato lilipungua. Sababu waliyoitoa ni kushuka kwa sekta ndogo ya mazao. Sasa hii sekta ndogo ya mazao ni kitu gani kilichopelekea sekta hii ishuke. Hiyo sekta ndogo ya mazao ilishuka ndiyo maana hili pato la Taifa likashuka. Je, ni kitu gani au ni sababu gani iliyosababisha hii sekta ndogo ishuke.

Halafu Mhe. Naibu Spika, huo ushukaji wenyewe 2013 ilikuwa ni asilimia 19.4 na mwaka uliomalizika au unaoendelea ni asilimia 15.9. Sasa nilipoangalia ile takwimu ya mwanzo asilimia 30.4 na huku ipo asilimia 19.4. Sijui hizi ni kiutafiti au ni kupanga tu kimahesabu hesabu ili wapate jambo la kutwambia sisi, takriban huku upungufu ni ile ya mwanzo 2.5 na huku ni 3.5. Sasa hii inaonesha kama ni takwimu ya kupanga kimpango pango tu, haielekei kuwa ni ya kiutafiti hasa kuwa hivi ndivyo hali halisi ilivyo. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, nijue hasa kuwa hii takwimu hii ya upungufu huu ndiyo uhalisia au ni ya kubunibuni tu ili mambo yaende kama wenyewe walivyoyapanga.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kilimo cha maweni. Ninawapongeze wakulima na Wizara kwa kuwaelekeza kuwashajihisha wakulima wa mazao haya ya maweni, yakiwemo ndimu, mbaazi, mtama, uwele, viazi vikuu na mazao mengine ya chakula na biashara. Mhe. Naibu Spika, kama wakulima wetu wataelekezwa vizuri na hawa mabwana na mabibi shamba katika vilimo vya tofauti wanaweza wakaleta mazao yenye tija na huu uagiziaji wa chakula ukapungua kwa kima kikubwa. Kwa sababu hivi sasa Mhe. Naibu Spika, pamoja na kilimo chote tunachofanya lakini uagiziaji wa chakula ni mkubwa zaidi kuliko vile vitu ambavyo sisi tunasafirisha.

Kwa hivyo, fedha ya Zanzibar inakwenda nje zaidi kuliko ile fedha inayoingia ndani. Hii ni hasara kwa sababu tunatoa nyingi, tunaingiza kidogo. Hivyo, hawa wakulima pindipo wakielimishwa na wakaelekezwa, wanaweza na wao wakapata mazao ya kupeleka nje hata ndugu zetu wa damu nao wakaweza kuingiza pesa kuliko kila siku sisi kuagizia tungule na mambo mengine kutoka kwa ndugu zetu wa damu, jambo ambalo na sisi hapa tunaweza kulifanya wenyewe. Hapa panataka hawa wakulima waelimishwe na wapewe taaluma ili waweze kuzalisha hayo mazao tusiagizie tena kwa mazao ambayo uwezekano wa kuzalisha hapa Zanzibar upo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ya Kilimo pamoja na mambo yake mengine mengi wamesema kuwa Wizara imeotesha jumla ya miche, wameitaja mingi lakini haja yangu hii ya mikarafuu; miche ya mikarafuu karibu milioni moja na kidogo kwa Unguja na Pemba. Baada ya kuotesha wanaitoa kwa wakulima na pia wanashawashajihisha wakulima kufanya vitalu vya mikarafuu na hatimaye Serikali kupitia Shirika la *ZSTC* kununua hiyo miche na wananchi halafu kupewa miche hiyo bure.

Lakini katika mwaka uliopita miche kadhaa ya wakulima waliotesha wenyewe Serikali haikununua. Mimi katika Jimbo la Mtambile nilipita mara moja, nikaambiwa angalau na wewe njoo utununulie miche mia mbili. Kwa sababu shirika limetutelekeza, mikarafuu yetu ipo bado hatujapata soko hawajainunua. Kwa hivyo, ningeiomba Serikali pale ambapo inawahimiza wakulima kufanya kitu fulani wahakikishe kuwa wao itakuwa ndiyo soko, kwa sababu mkarafuu hausafirishwi nje, ni karafuu peke yake ndiyo inayokwenda nje, lakini mkarafuu unaoteshwa ndani ya Zanzibar. Pale tunapowataka wakulima wafanye hiyo kazi tuhakikishe kuwa miche yote ambayo itazalishwa au itaoteshwa inanunuliwa na Serikali na hatimaye kuigawa kwa wakulima kama mpango wa Serikali ilivyojiandaa wenyewe kuigawa hiyo miche.

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme kwenye kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu katika mabonde ya umwagiliaji sehemu mbali mbali ikiwemo Makombeni. Pongezi kwa Makombeni imetajwa kuwa kumekamilika. Lakini

katika suala hili Mhe. Naibu Spika, kwenye malengo kulikuwa na lengo kulitaja bonde ambalo nilidhania kuwa ni bonde la jimbo langu. Ulitaja katika malengo bonde la Machigini. Kama Unguja hakuna Machigini basi hilo bonde itakuwa ni bonde la Jimbo la Mtambile. Katika malengo lilitajwa kuwa litaekewa umeme, lakini utekelezaji halikutokea tena, halikuzuka hilo bonde la Machigini. Ina maana kwenye malengo liliwekwa lakini kwenye utekelezaji halikujitokeza.

Mhe. Naibu Spika, nikwambie kuwa bonde hili limeshagharimu pesa nyingi sana za ndani na za wenyewe munavyoita wahisani wa maendeleo au wafadhili, vyovyote munavyoita mpaka *World Bank* imetia pesa zake pale. Kwa hivyo, kuna pesa nyingi sana ambazo zimeshakwenda ovyo kwa kukosekana tu kuweka umeme katika kile kisima. Kwa hivyo, hata Serikali hii haina huruma ya ile misaada wanayoiomba na kupewa, wao jambo dogo ambalo ni kasoro ya milioni hamsini kuweka umeme pale, wanakubali mamilioni ya shilingi yaliyoingizwa pale yapotee bure. Sijui hii ni aina gani, maana yake kama mimi ningekuwa niliosaidia au kufadhili pale, kwa kweli msaada mwengine mukiniomba nisingeliwapa. Kwa sababu jambo dogo lile la kumalizia liliwashinda. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeiomba Wizara hii ijitahidi kwa sababu ule mradi si wa jana na juzi ni wa muda mrefu na kilichokwama ni uwekaji wa umeme tu, kisima kimechimbwa kwa gharama kubwa, shamba limetayarishwa na pesa zikatumika nyingi sana, lakini Wizara ya Kilimo katika kumalizia hiyo kazi wamekwama.

Mara nyengine ninapofuatilia wanasema ni Shirika la Umeme. Shirika la Umeme wanasema hii ni kazi ya Wizara ya Kilimo wenyewe. Kwa hivyo, wanaifanya kama mpira. Maana yake mpira ukenda kwa huyu anaupiga teke na huyu anaupiga teke. Lakini kuna mambo ukiyapiga teke ni kuwa unaharibu maendeleo ya pale pahala. Mhe. Naibu Spika, ilifika wakati wakulima wa bonde lile wakataka ile misingi waliyoichimba au ile miundombinu iliyotengenezwa pale kuiharibu ili watu wapate mashamba yao na hili Wizara ya Kilimo wanalijua kwa hali iliyofikia na bado wameliacha vile vile. Sijui lengo, dhamira ni nini hata ikawa jambo lile dogo hivi sasa Mhe. Naibu Spika, linashindwa kumaliziwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine na mimi kama Waziri wa Elimu usemaji wangu mdogo mdogo. Pametajwa hapa kwenye kuendelea na uhakiki wa mali za Serikali zilizomo katika Wizara ya Kilimo na Maliasili na kuipatia hati miliki.

Mhe. Naibu Spika, hakuna jambo linalonishangaza katika serikali hii kuwa leo tuko katika miaka zaidi ya 50, kuwa mali zao bado hawajazijua. Hili ni jambo la kusikitisha kweli kweli miaka 50 tunaanza kuhakiki mali zetu leo, akaa! Hivyo ni

kweli ndani ya miaka 50 hii mnafanya uhakiki wa mali zenu leo, mlikuwa wapi siku zote hizo? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa serikali kusema hivyo kuwa wanafanya uhakiki leo, sio hawa tu ni serikali nzima mali zake hawazijui. Hili ni jambo la ajabu na la kusikitisha na la kuvunja moyo. *50 years of Independence* hamjui mali zenu, sijui mtazigawa lini. Lakini kutaka kujulikana kwa hizi mali Mhe. Naibu Spika, ni kwa hiki kitu kinachoitwa rushwa. Kwa hivyo, mali zinafichwa fichwa zisijulikane. Haiwezekani kuwa ndani ya miaka 50 kwa mali za serikali Mhe. Naibu Spika, hazijulikani na kupatiwa hati miliki.

Kwa hivyo, ningeomba pamoja na kuwa serikali imechelewa sana kuzitambua mali zake. Kwa hivyo, katika huu mwaka wa fedha ujao, basi mali za serikali zitambuliwe na zile za kupatiwa hati miliki zipatiwe ili kila wizara, kila idara na kila sehemu ijuwe kuwa hii ni mali ya serikali na hati yake miliki ni hii, vyenginevyo, kila siku tutakuwa tuna tia maji ndani ya pakacha. Pakacho ukiizamisha maji yatajaa tele, lakini ukinyanyua yote yanatoka.

Mhe. Naibu Spika, jengine wizara hii wamesema; Uhakiki wa wafanyakazi wa wizara Pemba kwa kutumia mfumo wa *database*. Wafanyakazi wa Kilimo na Maliasili wa Pemba bado hawajahakikiwa, kwa hivyo, watakuwa hawajui kuna wafanyakazi wangapi. Kama hali ni hivyo, kwa sababu hawajui pengine hata mishahara hewa itakuwa ipo. Sina hakika, lakini kwa kuwa bado wafanyakazi hawajahakikiwa na kuhakiki ni kutafuta uhalisia wa kitu chenyewe. Jambo hili Mhe. Naibu Spika, katika miaka mitatu au minne hii, kila siku wafanyakazi wanahakikiwa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, msiwahalilia, wahakikieni tu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, miaka yote hii wafanyakazi hao wanahakikiwa. Kuna ugumu gani ambao serikali haimalizi kuhakiki wafanyakazi wake. Kwa hivyo, ningeomba hii *speed* ya kuwatia wafanyakazi wa Pemba kwenye *database* watieni. Lakini kwa sababu wamefanyiwa Wapemba tu hapa, basi itakuwa wa Unguja tayari wameshahakikiwa na wameingizwa kwenye *database*. Ningependa kujua hivyo Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala hili la wizara hii ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika wizara hii ni Idara ya Kilimo yenyewe. Idara hii kuna sehemu imesema kufanya ukaguzi wa mazao, kama upandaji wa ndizi kwa wilaya za Pemba, Wete, Micheweni na Mkoani na hatimaye wakulima wale kushusha ndizi zao kuja katika kisiwa cha Unguja.

Mhe. Naibu Spika, hili lazima lifanyiwe uhakika kwa sababu Pemba wanazalisha ndizi kwa wingi na wao wanazalisha tu lakini ndizi zaidi zinaliwa upande wa pili

huku, kwa sababu watu wanaleta kwa ajili ya biashara. Lakini migomba nayo inakabiliwa na magonjwa mbali mbali, kama zaidi ni migomba ya ndizi za mtwike, unaikuta ndizi bado haijapea, kwa nyinyi watu wa kisasa mnasema haijakomaa, lakini ni neno baya kwa mazao, kwa sababu kukomaa ni kwengine na kupea au kuwa tayari kuliwa ni jambo jengine. Mara nyingi ndizi kabla ya kupea inaanza kuwiva, kwa sababu imeingia wadudu waharibifu wa lile zao.

Kwa hivyo, sijui kwa wizara hii imepata tiba ya magonjwa haya ya migomba, kama haijapata ni kwamba hawa watafiti wetu wafanye utafiti wa hawa wadudu waharibifu wa migomba ili ndizi zetu ziwe salama. Lakini Mhe. Naibu Spika, ndizi hizi hatimaye zinasafirishwa kuja kisiwa cha pili.

Mhe. Naibu Spika, kuna kipindi fulani jambo linalonisikitisha Pemba kulikuwa na upungufu kidogo wa nazi, lakini mazao kutoka Unguja kusafirisha rasmi ilikuwa serikali hii haitaki. Wapemba walikuwa wanataka nazi wanazuiliwa na mara nyengine zinamwagwa pale bandarini. Sijui kwa mfumo huu bado unaendelea mpaka leo, kwa nini, mbona ndizi za Pemba mmazitaka wala hamzizuwii? Lakini nazi zenu kuja Pemba hamtaki kwa nini? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama hili liko hivi, basi ningeomba utata huu uondolewe, watu wa visiwa hivi ni wamoja zaidi kuliko hao ndugu zetu wa damu. Mhe. Naibu Spika, hili sisemi kwa kubahatisha, hayo yameshatokea. Wengine tulikuwa tunachukua nazi kwa kujificha, tulikuwa tunatia kwenye begi kuonesha kuwa tumechukua nguo kumbe tumetia nazi, kwa sababu tusije tukanyang'anywa pale bandarini.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kama sitakumbuka jengine na jumla ya tani 14 za karafuu na tani 325 za mwani zimekaguliwa, na kusafirishwa nje ya nchi, na tani 1,584 za mazao ya chakula kutoka Tanzania Bara, na tani 9.954 za mazao ya chakula kutoka nje ya nchi zimekaguliwa. Mhe. Naibu Spika, huu ukaguzi wa mazao ya chakula na biashara, sijui ukaguzi unafanyika wakati gani mpaka mara nyengine bidhaa za kilimo kutoka nje, kama mchele na mengineyo, ikawa zinaingia bidhaa ambazo ni *out of date,* yaani hazifai tena kwa matumizi ya mwanadamu.

Lakini hapa inaonesha kuwa kuna ukaguzi unaofanywa. Sasa huu ukaguzi unapofanywa ikionekana kuwa bidhaa fulani ina kasoro, basi isiruhusiwe kuingia moja kwa moja, kwa sababu na sisi hivi tunavyopeleka nje, kama vikiwa na kasoro nadhani havitopokelewa. Sasa hizi bidhaa zetu zinafanywa *packing* nzuri na mambo yake mazuri, ili vikapate soko vizuri. Lakini kwa upande mwengine baadhi ya wakati zinaingia bidhaa Zanzibar ambazo hazina ubora.

Mhe. Naibu Spika, sizungumzii bidhaa zote, hapa nazungumzia bidhaa za kilimo, wasijibu wakasema mambo mengine sio yetu, hapana. Hizi bidhaa za biashara za kilimo, mchele na kadhalika, ingawa ni mambo ya biashara, lakini hapa wao wenyewe wameyataja, baadhi ya wakati vinaingia vitu ambavyo havina *quality* ya kuingia hapa na vinaingia. Sasa ukaguzi huu nao uwe makini kama tunavyofanya ukaguzi wa karafuu zetu na mwani kabla hatujasafirisha nje, kwa sababu sisi tunazifanyia zile zetu ukaguzi mzuri ili zikapate bei kule zinakokwenda. Kwa hivyo, tufanye ukaguzi wa biashara zinazoingia ili kuwalinda walaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, magonjwa mengi tuliyonayo ni kutokana na madude mabovu tunayokula; mafuta mabovu na mchele mbovu, hatimaye aliyekuwa hana sukari anapata sukari, aliyekuwa hana *pressure* anapata *pressure*. Hayo ni magonjwa ya zamani ambayo ilikuwa unahesabu, unamtafuta bwana fulani ana *pressure* kaa! leo kila mmoja imekuwa ni jambo la kawaida kulingana na kutokuwa na udhibiti wa uingizaji wa baadhi ya vitu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia sina lolote la kusema katika wizara hii, nitakwambia ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii nikatoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili, hasa kwa vile waziri wake ni Kaimu Waziri, basi kwa hivyo, ni watu wa kuonelewa huruma sana hii wizara na tukaweza kuwapitishia hii bajeti yao kwa njia ya urahisi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia mchana huu tukiwa bado salama ndani ya Baraza hili, hatujapata matokeo yoyote yale mabaya. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee na vikao vyetu, lakini tumalize tukiwa ndani ya hali ya usalama.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nisiwe mwizi wa fadhila kwanza sina budi niipongeze Wizara hii ya Kilimo na Maliasili kwa kitabu chao hiki cha bajeti, lakini kwa utendaji wao juu ya kwamba wana Makaimu Mawaziri wengi wanaokaimiwa, lakini kwa utendaji wao na uzalendo wa hali ya juu wanaouonesha katika jamii. Kwa hivyo, tuwapongeze sana na tuwashukuru, pia, tuwatakie wawe na moyo huo huo wa uzalendo katika kufanya kazi zao za kuwashughulikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikianza mchango wangu nianze katika ukurasa huu wa 3, ambapo kitabu kimeandikwa kuwa ukuwaji mchango wa sekta ya kilimo katika sekta ya kilimo katika pato la Taifa imeshuka kwa kiasi fulani, na takwimu hapa

kwenye kitabu zinaonesha. Mimi nikiri hilo kwa sababu wenyewe ni wataalamu na wameona hili suala zima la ushukaji wa pato la Taifa kwa mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, katika hotuba yake aliyokuja kututolea hapa katika Baraza la Wawakilishi, alitangaza Zanzibar tutakuwa na Mapinduzi ya Kilimo. Sasa lengo ilikuwa ni kuona mabadiliko katika sekta hii ya kilimo, hasa kwa vile inajulikana dhahiri kwamba sekta hii ya kilimo karibuni ni zaidi ya asilimia 70 ya wananchi, ambao tunategemea sekta hii ya kilimo ajira zetu. Hilo halitaki tochi Mhe. Naibu Spika, ni kweli Wazanzibari wengi, aliyekuwa sio mkulima basi ni mfugaji, aliyekuwa sio mfugaji basi ni mvuvi na mambo mengine.

Sasa watu hao katika sekta hiyo isiyo rasmi inategemea serikali kwenye kutekeleza majukumu yao hayo. Inategemea serikali zaidi ili iwawezeshe wananchi hawa waliowanyonge waweze kufikia hatua ya kile wanachokifanya basi kipato chao kionekane. Hiyo ndio imani na hilo ndilo lengo tulotegemea katika Mapinduzi haya ya Kilimo. Lakini tuseme tunashukuru, hiyo nia ilikuwa njema, lakini bado hatujafikia huko kutokana na sababu ambazo wao wenyewe serikali wanazitambua. Muda mwingi zinaelezwa katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, moja ya kuwa hatufikii lengo hilo ni kuwa yale maneno yaliyokuwa siku zote yamo kwenye vitabu ya kuwa bajeti ni finyu, pesa zilizotakikana hazikupatikana kwa wakati. Sasa hili ndio linalosababisha kuwa hatukufika kwenye hayo Mapinduzi ya Kilimo tuliyokusudia, kwa sababu bila ya pesa huwezi kufanya chochote, bila ya kwenda na sayansi na teknolojia huwezi kufanya kitu chochote katika ulimwengu huu. Kwa hivyo, ufinyu wa bajeti nao unachangia.

Mhe. Naibu Spika, pia, kutoshuka kwa pato hili la Taifa, na serikali naiomba ifanye utafiti wao. Sababu nyengine zinazosababisha ni kuwa Zanzibar bado tunategemea sana uingizwaji wa vitu kutoka ng'ambo, hatuna uzalishaji wa ndani ambao hilo pato la Taifa, au hao wazalishaji watakuwa na uwezo wa kuzalisha ili kiuzwe hapa ndani ya nchi. Bali kila kitu sasa hivi tunategemea kutoka Bara na maeneo mengine.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 2 hapa kaeleza kuwa, sababu wao walizoeleza za kushuka kwa ongezeko hilo, ni kupungua kwa eneo lililolimwa na uzalishaji kutoka ekari 94,701. Mimi nataka Mhe. Waziri, akija anifahamishe kwa sababu bado sijafahamu kuwa ni eneo gani ambalo lililimwa la uzalishaji likaweza kupunguza ili pato la Taifa katika sekta hii ya kilimo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, atakapokuja basi atakuja kunieleza.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, nije katika hiki kilimo cha maweni. Mhe. Naibu Spika, hii ni mara yangu ya pili au ya tatu, kuzungumzia suala zima katika kipindi hiki hiki cha bajeti suala la kilimo cha maweni.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoijua Wilaya yetu ya Micheweni na inavyozungumzwa, kuwa ni watu wengi, lakini ni serikali nayo kuona hali halisi ya watu wake namna walivyo. Leo huwa ni yale maneno tu, hata hapa katika hili hatukuambiwa kwamba kilimo hiki cha maweni ambacho kimefikia hatua ya kushajihisha jamii katika kulima kilimo hiki cha ndimu, mbaazi na mtama. Hawakutoa ni maeneo gani ambayo wameweza kulima hiki kilimo.
Mhe. Naibu Spika, lakini mimi nasema kutokana na Wilaya ya Micheweni, bado Wilaya ya Micheweni hawajapata uhamasishaji wa kuweza kulima katika eneo lile, kuanzia Shumba ya Mjini, Micheweni na maeneo mengine, tukiona kuwa na wao ni moja kati ya watu waliokuwa wanaishi katika sehemu za maweni. Moja nililizungumza hili katika bajeti moja. Kwa kipindi kile alikuwa anakaimiwa na Mhe. Mwinyihaji. Nikauliza kuwa wanaolima maeneo ya juu wao wamefaidika na haya Mapinduzi ya Kilimo.

Kwa mfano, waliokuwa na mabonde yao yameingia chumvi, tayari yametengenezwa ili wapate walime, lakini wengine wamefaidika waliokuwa na mabonde yao ya umwagiliaji maji, wanapata kufanyiwa ukarabati, wakaendelea na shughuli zao. Lakini hawa wao watafaidika vipi na Mapinduzi haya ya Kilimo watu walioko maweni.

Kwa hivyo, bado nasema kuwa katika Wilaya ya Micheweni bado ushajihishaji haujafika katika maeneo haya ili na wao wakapata elimu namna gani ya kuweza kufanya kazi katika yale maeneo yao. Isipokuwa kule ujenzi wa barabara ukija basi wale watu wataonyeshwa kule kwa kwenda kuchimba kifusi. Lakini kusema kweli kwa kilimo hawajafaidika na suala zima la kupata utaalamu zaidi katika suala la kilimo cha maweni.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa huu wa sita, *paragraph* ya tatu hapa kasema Mhe. Waziri, kuwa;

> "Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 tumepata mafanikio mengi sana."

Mhe. Waziri, ametaja hapa mafanikio hayo, lakini moja ni kuwa pembejeo za kilimo cha mpunga kwa msimu wa masika 2015, kataja idadi ya ekari walizopata lakini na mbolea ambazo kuwa zimetolewa si chini ya tani 750, na kataja aina za mbolea kuwa kuna *TSP* tani 150 na Urea tani 600.

Mhe. Naibu Spika, nipongeze hii hatua lakini nataka nizungumze jambo moja. Mhe. Naibu Spika, ardhi zetu zimechoka, ardhi hatuna lakini hizo tunazotumia zimechoka, zimechoka, mtu hapo hapo kieneo chake alichonacho anacholima ndio hicho hicho, habadilishi chengine. Sasa bihairi ya kulima kwenda sambamba na ulimaji wa mbolea haliwezekani ina maana utapoteza nguvu, lakini mapato yatakuwa ni madogo hasa katika mbolea hii ya *TSP* bado uagizishiaji wake ni mdogo kwa sababu hii ni mbolea ya kusilia. Shamba haiachwi hata mwaka mmoja, shamba hazilazwi tena ng'ombe hazina mbolea, inakuwa saa zote zinalimwa, bihairi ya kusia na mbolea hii ya kufulia basi hatimae ni kuona mipunga inaanza kudumaa.

Kwa hiyo, naiomba serikali kuwa mbolea hii ya *TSP* wafanye juhudi ya kuongeza kwa sababu bado mbolea hii ni kidogo ambayo ni kuwa ni mbolea hiyo unayosema ya kusilia.

Mhe. Naibu Spika, piam katika utekelezaji wa malengo hapa kwenye programu kaandika;

"Programu ya kuimarisha miundombinu ya masoko ya kilimo na ongezeko la thamani ya mazao *MIVAP."*

Ametuandikia kuwa tuangalie katika Kiambatanisho Nam. 5 ambapo Mhe. Naibu Spika, Kiambatanisho hiki Nam. 5 gharama ya mwaka 2014/2015, programu iliombewa jumla ya Tsh. 60,000,000 kutoka SMZ. Lakini mpaka kufikia Aprili 2015 wameingiziwa karibuni milioni 10. Mhe. Naibu Spika, hayo malengo kweli yatafikiwa katika hali hii ambayo kuwa inategemea kuendeleza hicho kilimo na inawaajiri watu karibuni asilimia 70 na hali yenyewe ya uingizaji wa pesa ni hiyo.

Kwa hiyo, mimi nadhani kama bado wizara hatujaipa umuhimu wala hatujaipa kipaumbele, tunatangaza tu kwa sababu tukisikia wenzetu, tulisikia Bara kwamba wanasema kuna "Kilimo kwanza" na sisi tukaona bora tuseme tuna "Mapinduzi ya Kilimo", lakini nia na madhumuni bado haijafikiwa.

Mhe. Naibu Spika, halafu niende katika Idara ya Kilimo, Idara hii ina jukumu la kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri na mambo mengine. Niende katika malengo yao moja amesema kuwa huzalisha tani 350 kutoka kwa wakulima na kununua tani 150 ya mbegu ya mpunga kutoka Tanzania Bara. Mpaka leo Zanzibar siku zote tunalima, tumezaliwa ndani ya mabonde, tumekulia ndani ya mabonde, lakini mpaka leo serikali hii bado hatujajua mbegu gani itakuwepo Zanzibar ili iweze wakulima wetu waweze kulima kwa vizuri. Mpaka leo tunategemea kuagiza mbegu au kununua mbegu kutoka Tanzania Bara, na nadhani katika mashamba yetu yote hapa basi uzalishaji wa mbegu naona kama ndani ya mabonde umo, lakini labda

hatujafanya utafiti mbegu gani ambayo Zanzibar inaweza ikanawiri, inaweza ikatoa tija tangu hii miaka mitano hii au huko nyuma zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini suala jengine malengo haya haya ya utekelezaji 2014/2015, amesema mafunzo ya muda mfupi juu ya mbinu, shirikishi za kilimo, bora kwa mabibi shamba na mabwana shamba. Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuwapongeza kwa kuweza kutuwekea mabibi shamba hawa na mabwana shamba ambao kuwa lengo lao ni kutoa taaluma kwa wakulima wetu. Lakini nasema kwamba kuwa bado watu hawa hatujawawezesha kufikia wananchi, kwa sababu bwana shamba huyu pengine mmoja ana eneo si chini ya majimbo mawili na yeye hana hata baiskeli.

Sasa itakuwaje atawafikia vipi kweli wakulima huyu, ataweza kweli huyu, kwa sababu mtu mpe wilaya nzima lakini umuwezeshe ili aweze kuwafikia wale wakulima na hawa wanaofikiwa hasa ni yale mabonde ya serikali tu, lakini watu waliomo ndani ya maeneo mabonde mengine madogo madogo hawa hawawapati hao mabwana shamba, hawawapati hata kidogo, isipokuwa wale walioko pengine mabonde ya serikali kama Saninga na Kinyakuzi yale ndio yanajuulikana wanapata ile taaluma.

Lakini maeneo mengine ya kilimo hawapati utaalamu wowote, hawapati kushauriwa kwa sababu mabwana shamba wenyewe hawajawezeshwa ila wanaekwa tu mabwana shamba, si kweli kama mtu atatoka akaweza kuzunguka majimbo mawili kama ni msimu wa kulima akasema aende akatoe taaluma, hilo haliwezekani mshahara wenyewe anaopata mkia wa mbuzi, halafu hilo linawezekana wapi.

Hilo Mhe. Waziri, nakuomba kuwa bado hawa kama mnataka wafikie wananchi na wale walioko na mashamba yao ndani ndani yaliyokuwa hawamo ndani ya mashamba haya makubwa, basi na wao waweze kufikiwa ili waweze kuwafikia wale wakulima na wao wapate taaluma kabla ya kuanza kutayarisha mashamba yao, wakifika wakati wa kufia wapate taaluma sio waoneshewe wale waliomo kwenye yale mabonde ya umwagiliaji maji, na hawa huku nao ni wananchi na ni walipa kodi wastahiki nao wapate wataalamu wa kuwaelekeza katika kilimo chao.

Mhe. Naibu Spika, pia, nipongeze katika kupanda miti hapa Mhe. Waziri, amesema kuwa kupanda miti ya misitu eneo la hekta 300 katika mashamba ya serikali. Lakini mimi sitaki kuwa hayo mashamba ya serikali, naomba serikali kwamba bado kuna vikundi ambavyo vinajitokeza watu wanapanda miti hii ya misitu na wao muwatafute na muwatambue. Mtakapowatambua basi na wenzao watapata hamasa ya kuendeleza mambo kama haya mazuri ambayo kuwa sasa hivi tunaikuta nchi yetu imekuwa jangwa. Kwa hiyo, kuna kikundi pale Kikunguni ambacho kinapanda miti, ni kikundi kizuri na hivi karibuni msitu mkubwa ambao

walifanya hifadhi yao pale. Kwa hiyo, naomba muwatambue hawa ili na wao waweze kushajihika na waone serikali yao kuwa inawajali.

Mhe. Naibu Spika, jengine limeshazungumzwa hapa katika malengo ya mwaka ya Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka ambazo amesema kuwa kuyatambua na kutaarisha mpango wa usimamizi wa mashamba ya serikali pamoja na eka tatu.

Mhe. Naibu Spika, niungane na Mhe. Mzee Mohammed, kuwa bado mashamba haya hawajayatambua, serikali bado hawajayatambua mashamba haya na mashamba haya kila siku yanauzwa na wanaouza si wengine ni hao hao serikali zetu zilizopo chini huko. Mashamba haya yanauzwa wala watu hawajali wala wafanywi chochote na halafu nataka niambie hasa wanaoshughulikia na haya ni watu wa ardhi, ni watu wa kilimo kwa sababu kila mmoja yumo hapo katika kuhifadhi mambo haya ya mashamba ya eka.

Mhe. Naibu Spika, ukienda ardhi wamo, ukija kilimo wamo na ndio haya yaliyopelekea kuna matatizo sasa hivi katika Wizara ya Katiba wale, kuna mashamba ambayo kuwa yalitolewa wakfu, lakini hayakuwahi kusajiliwa yamefika pahali mashamba hayo watu walishindwa kuyasajili katika serikali, ndio haya. Hakuna kitu kinachojuulikana kinaratibiwa wapi katika wizara gani; ardhi imo, kilimo wamo, lakini halijuulikani na ndio maana ikafika pahala hakuna linalojuulikana.

Kwa hiyo, naomba basi Serikali ifanye juhudi na maarifa, kwa sababu mimi nakumbuka hivi juzi nilivyonunua kijisehemu kina mikarafuu mitano lakini tulikuja kuletewa taarifa kwamba hii ni eka, nikawaambia mimi sijanunua kama eka, lakini akatokea mtu akasema huyo aliyekwambia hivyo hajui, ina maana wote hawajui haya masuala yako je. Kwa hivyo, kama mnafanya uratibu wa masuala haya ya kuzitambua hizi eka tatu, basi mufanye na Masheha ndio watakaowaongoza kwa sababu nyie hamujui kitu. Lakini Masheha ndio watakaowaongoza katika kukwambia hili ni eneo la Serikali, hili sio eneo la Serikali, hili sio eneo la Serikali, naomba sana Mhe. Naibu Spika.

Lakini Mhe. Naibu Spika, Idara hii ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika malengo yao moja ni kukarabati ghala moja la kuhifadhia vitu. Mhe. Naibu Spika, hii inakuwa ni nyimbo hii na kipindi cha mwaka jana nilichangia bajeti hivi hivi nikauliza nikaambiwa kwa kuwa Mhe. Mwinyihaji, akaniambia kwamba pesa zipo kwa sababu nilikuwa sijaziona, akanambia pesa zipo zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu wa Idara hii ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Lakini leo yanakuja yale yale kukarabati maghala na mimi nakumbuka nilikuweko kwenye Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, maneno ni haya haya ya kukarabati ghala moja la chakula, kwa hivyo, hebu atupe uhalisia hasa na si aibu mtu kusema kile

kinachomshinda, lakini sasa kila siku kuna ukarabati wa ghala hii ambayo kuwa hatufikii pahali pazuri.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa nataka nipate maelezo kupitia Wizara hii ya Kilimo kupitia Idara yao hii sijui niseme Idara ya Maliasili hizi zisizorejesheka, suala langu hili nililiuliza kwa Mhe. Waziri wa Fedha, kutokana na usumbufu uliopo bandarini na leo nalizungumza tena na ikija Wizara ya Miundombinu nayo pia nitakuja kuwauliza, lakini almuradi tulipatie ufumbuzi, kuna watu pale bandarini ambao kuwa unapotoka na mzigo huku kama ni meza, kiti, kabati, kitanda, ukifika pale ukitaka kutoka nje hawakuruhusu mpaka ulipie si vibaya.

Lakini sasa kile kinacholipiwa ni kuwa na wao watoe risiti, sio wakae kimabavu bavu tu, lakini Waziri wa Fedha, alinambia mtu kama huyo ukimpata wewe nenda kashitaki tu na hilo haliwezekani na Serikali hadi ifanye nidhamu kwa wananchi wake, kwa nini saa zote watu wahangaishwe, yeye itakuwaje mtu akae pale, kaekwa pale kwa mujibu wa sheria aweze kumchaji mtu kwa kuwa kapita na mzigo, kwa nini asiweze kumpa risiti.

Mhe. Naibu Spika, hili haliwezekani sasa kwa sababu Waziri wa Fedha alinambia pengine ni watu wa Kilimo wanaweka watu wao pale, basi watwambie kama ni watu wa kilimo wanaweka watu wao pale watwambie ni sababu gani za msingi ambazo kuwa watu wanaowachaji pale hawawapi risiti kama wao wapo pale kwa ajili ya nini, kwa sababu tusiwahimize watu kusali kumbe sisi hatuna nia ya kusali.

Siku zote tunapiga kelele na wafanyabiashara wa Zanzibar kwamba wanakwepa kutoa risiti kwa wanunuzi, leo sisi Serikali tunakwenda kukaa pale tunamuhangaisha mtu halafu Waziri anakwambia uende ukamshitaki, ukamshitaki wapi, pengine mtu huyo hana uwezo, mtu amekwenda kushinda mule mchana kutwa na kachoka hajapanda unamwambia lete shilingi elfu kumi ndio upite, lakini nipe risiti hana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili nakuomba uje unipe ufafanuzi mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, badala ya hayo machache, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.*(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha naomba nizungumze masuala mawili; Suala la kwanza mahudhurio yetu ni mabaya sana, nawaomba wanadhimu wa Chama cha CCM na CUF tuwaambie Wajumbe wetu waje Barazani jioni kwa sababu bajeti ya mwanzo tumeweka uporo, na dalili ilivyo na hii tutaweka uporo, si jambo zuri, bajeti mnajadili inafanywa majumuisho na tunapitisha vifungu, lakini tukianza kuweka uporo basi bajeti zote zilizobakia tutaweka uporo. Kwa hivyo, si jambo zuri na si la kupendeza, kwa hivyo, kila mmoja anayejua anakaa na mwenzake amuambie ili jioni tukija tuje kupitisha

Wizara ya Elimu, tumalizie Wizara ya Kilimo kesho asubuhi tuimalize, naomba hivyo sana.

La pili, niwashukuru kwa kunipa ushirikiano tangu asubuhi hadi hivi sasa, maneno niliyoyasema muyazingatie na muyape umuhimu wa kutosha. Naahirisha kikao hiki hadi Saa 11.00 za leo Jioni.

*(Saa.6.58 mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:** Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa jioni hii, kwanza sote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutupa afya na pumzi hizi ambazo tulizokuwa nazo mimi na wenzangu tuliokuwa tunaringia nazo. Maana yake pumzi hizi ni za kuazimwa, na mwenye kuazimwa ndiye Al-Rahman mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya Kilimo, kwa utendaji na kwa hekma na busara na usikivu mkubwa. Napenda nikiri vile vile, toka kuwa Mwakilishi wa jimbo la Uzini kwa kuwasimamia wananchi wangu, Wizara hii naweza kusema kwa Mwenyezi Mungu imenipa nafanikio makubwa sana.Kwa sababu kila ninapokuwa napata matatizo katika jimbo langu hasa sehemu ya Miwani, Kiboje, Mchangani, Bambi, basi changamoto zile nnapokuwa nnapata na wenzangu huwa miye sipigi hodi kule Wizara ya Kilimo. Lakini nashukuru Mungu *Alhamdulillah* naamini hawa wenzangu wanafahamu nini maana ya kuwatumikia wananchi, kuanzia wizara nzima, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi na nikifika tu na ujumbe wangu.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri Wajumbe wangu tunapofika kwa Katibu Mkuu nnamwambia hasa bwana mimi sina miadi, namwambia yule sekretari wake. Ndiyo nilivyo mimi, sehemu yoyote nikienda kama sina miadi huwa namwambia sekreteri sina miadi. Basi yule Katibu Mkuu ukimtizama hacheki, anakuuliza ehee! unasemaje. Maana yake yake ndivyo walivyo, yeye Naibu Katibu Mkuu kwa kweli wanatoa mashirikiano makubwa. Mimi nasema kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Uzini, maana nimesimama hapa kwa niaba ya jimbo la Uzini kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mhe. Naibu Spika, changamoto zipo, nilikuwa naomba tu kwa upande wao kwamba mawasiliano ni kitu muhimu sana. Kwa sababu ndugu zetu hawa

waliokuwa vijijini wakati mwengine hupata mafanikio ya elimu. Na lazima tunatakiwa tubadilike. Mara nyingi panapotokea msimu wa mpunga, ningeliwaomba kutilia mkazo mabwana shamba kuwatembelea, wakulima wetu hasa wa mpunga inapofika wakati namna gani tunaweza kusaidia.

Wenzangu wamesema kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wetu wa binaadamu. Lakini Mhe. Naibu Spika, kazi kubwa inayotukabili ni mashirikiano, "kidole kimoja hakivunji chawa", ni mashirikiano, kukaa pamoja na kuona jinsi gani tunaweza kusaidiana. Ndugu zetu hawa wa upande wa kilimo na ufugaji, ni kuwa tuwawezeshe tu. Kwa sababu kama sio wakulima, mimi ni mkulima na sisi ndio tulipotoka huko. Sasa mimi ningeliomba Wizara ya Kilimo ikakaa na Wizara ya Miundombinu ikaona jinsi gani ya kuwaondoshea matatizo zile barabara zilizokuwa zinawakabili katika mazao yao.

Mhe. Naibu Spika, wakulima wao lengo lao ni kuwawezesha na kuwawekea maeneo ambayo hata lile gari la ng'ombe au la punda liweze kupita ili mazao yao waweze kuyaondosha na kuyaweka barabarani baadae kupakia katika gari. Mimi wito wangu kwa Wizara ya Kilimo niko tayari kushirikiana kwa hali na mali kama ninavyokwenda nao, kuona kwamba mashirikiano haya tunaweza.

Lakini vile vile, Mhe. Naibu Spika, naiomba Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara. Mheshimiwa, kilimo haiyendi moja ni lazima kuwepo na mawasiliano, ukisema kilimo unaigusa Wizara ya Biashara, ukisema kilimo unagusa miundombinu. Sasa mimi ningeliomba Wizara hizi ikawasaidia wakulima wetu hawa. Unajua huwa kunatokea msimu kama wa machungwa, embe, mananasi. Lakini inasikitisha kwamba wakulima wameshapata mazao kama yale, utakuta kitu kama nanasi mkulima hata ile shilingi mia tano, mtu anashindwa kupata kwa sababu ya msimu. Sasa ili kuwasaidia katika mazingira ya kuondosha umasikini katika vitu hivi. Hawa wakulima lazima tuwawezeshe namna gani ya kuwatafutia soko. Kwa sababu anaweza akatoka mtu tu, akenda akamwambia hizi nanasi zote mia mbili mia mbili, pakuweka hana, hana *store*, ana watoto, anataka kuwasomesha watoto wake. Pesa hizo hizo za kulima ndizo zimsaidie mwanawe.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nafikiti ni vizuri wizara hizi zikakaa, zikafanya majadiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha jinsi gani tuweze kuwapatia soko. Masoko yapo, Dubai leo nanasi kwa pesa za Tanzania ni Sh. 10,000/= lile nanasi dogo tena changa, embe ni Sh. 5,000/=, leo ukenda sokoni embe pale mpaka zinaoza. *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu katupa neema katika ardhi yetu sasa hivi imebadilika. Wafanyabiashara wanatembea na gari za Carry, Mwenyezi Mungu awajaalie kwa neema aliyotupa. Utakuta gari za Carry zina machungwa, maembe, kwa hivyom Mheshimiwa, tutafute *solution* katika kuwasaidia kweli wenzetu hawa

wa kilimo, hasa kuwasaidia wakulima wa mboga na sehemu nyengine hizi tuweze kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, kubwa tulilokuwa tumeliona sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni suala la fedha, kwamba haya ni matatizo yanayoukabili uchumi wetu. Kubwa zaidi nimeona kwenye vitabu fedha haziingii. Mimi nakiri kwamba serikali yetu ambayo anayoiongoza Dokta Shein ni serikali sikivu sana, kuanzia Rais pamoja na watendaji wake wote. Lakini serikali kama Waziri wa Fedha, pesa zikiingia ndizo zinazoweza kutumika.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hizi mimi ningelikuwa nina mawazo na nilisema tuwe katika njia ya kuipanga bajeti hizi za kuweza kukidhi mahitaji. Mimi nikiri kama Mwenyezi Mungu angetupa neema ya kuwa na uchumi imara na tungekuwa na viwanda vya kutosha. Maana yake nchi yoyote duniani ukitaka utajirike na uendelee na uchumi imara lazima uwe na vianzio ndani ya nchi yako, kama viwanda vya sehemu mbalili. Lakini kwa kutegemea sehemu kubwa ya wahisani, kwa kutegemea sehemu kubwa ambazo unazipangia zikija, halafu haziji, kwa kweli ni mtihani wa Mwenyezi Mungu. Ndio hapo tunapofika sasa tunaanza kulaumiana.

Mhe. Naibu Spika, hii leo tunasoma bajeti, Mhe. Waziri wa Fedha, kasoma bajeti, nataka niiambiye Zanzibar leo, kwamba kama bajeti yetu hii imeathirika, mimi nasema lazima tuwe waangalifu. Tatizo lilokubalikana Zanzibar leo ndio bajeti zetu zote hapa tunazozipigia kelele ni kampuni hii inayoitwa *ESCROW*.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nimesema wazi, watu watano haimo ndani ya Muungano wala hatuna haja ya kusubiri Bunge la Katiba iseme hii ikipitisha uchumi huu utakuwa. Ni watu wachache wamechota pesa mabilioni, wao wanaita vijisenti, Mungu awazidishie, maana fimbo ya Mungu haina sauti. Mabilioni ya pesa wamechukua matokeo yake Taifa zima limekula hasara. Watu waliokula hasara ni watu ambao wapo katika *grass root*. Mheshimiwa, kila kitu kimepanda,

Kwa hivyo, bajeti yetu tuliyokuwa tumeipangia Waziri wa Fedha na serikali yetu, wahisani wamezuia misaada. Kama wahisani wamezuia misaada na Waziri wa Fedha amejipangia wakati mwengine kupata hizi. Hili lazima tulione na tulifanyie kazi, kwa sababu iko wazi ni watu wachache. Haimo ndani ya Muungano, haimo ndani ya serikali. Halafu hilo suala la waliochota pesa sio suala la Muungano. Ni *TANESCO* iliyofanya watu wakachota pesa matokeo yake sote leo hapa tunaathirika. Matokeo yake leo dola ni Sh. 202/= *Subhanallah* sijui tunakwenda wapi. Kila kitu kimepanda sasa na tunaelekea katika mwezi wa Shaabani kuelekea Ramadhani. Hii ni athari kubwa, hatuwezi kukaa tukaona athari hii ya watu

wachache ambao hata barabara zao zikiwa hazipitiki, wanachua ndege wanapakia magari yao kwenda kwenye sehemu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi hizi wizara wakati mwengine sizilaumu sana. Mimi nakubaliana na Wizara ya Kilimo kwamba ukosefu mkubwa hapa ni fedha. Lakini hizo fedha mpaka ziwepo. Mpaka Waziri wa Fedha apate hizo fedha za kuweza kuzitoa. Sasa kama makusanyo hamna, malengo hakuna, hili linakuwa ni ngumu sana. Kwa hivyo, mimi naomba watendaji wa wizara ya Kilimo yale madogo madogo ambayo ya kuwapa elimu wakulima wetu waendelee kuwa nao uzalendo huu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ina wataalamu *Alhamdulillah* wa kutosha, wana uwezo, wana hekma, ni watu. Lakini tatizo jengine haya mambo mengine hayahitaji mambo makubwa. Mimi natoa ushauri kwa wizara inayohusika unapofika msimu wa mpunga hasa wakati mwengine kuna wanyama wanahitaji dawa, wana taka elimu, sasa haya mambo madogo madogo tuweze kuwasaidia wakulima tutaweza kufika mbali sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina la kusema lakini ninachoomba kuwaomba Wawakilishi wenzangu kwamba naiyunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini kwa asilimia zaidi ya mia Wizara ya Kilimo kwa usikivu wao, kwa hekma zao, kwa busara zao na nawaomba waendelee hivyo hivyo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu wake na watendaji wake wote kwa ujumla kwa kazi zao wanazozifanya pamoja na kipindi kigumu walichonacho cha ukosefu wa fedha. Mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa sababu hii ni wizara yangu ambayo kuwa naifanyia kazi katika Kamati za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu niipongeze Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuongeza mapato ambayo kuwa yalikadiriwa kukusanya katika mwaka 2014/2015. Hizi ni dalili nzuri za watendaji wazuri wa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye mradi wa barabara hizi, mradi wa *MIVAP*, barabara za ndani ambazo kuwa zimepita vijijini. Niwapongeze Wizara ya Kilimo kwa jitihada zao walizozichukuwa katika kuimarisha miundombinu hii ya

barabara. Pamoja na miundombinu hii ya barabara bado tatizo lipo kwenye miundombinu hii ya barabara ambayo kuwa inafadhiliwa na mradi wa *MIVAP*. Kuna barabara ambayo inatoka Kiuyu Minungwini, Penjewani mpaka Kangagani, barabara hii ambayo kuwa imetengenezwa na Wizara ya Kilimo kwa kifusi. Barabara hizi wakati wa kuzijenga hawakuweka mabomba ya kupitisha maji wakati wa mvua, matokeo yake Mhe. Naibu Spika, wananchi wanaokaa kwenye maeneo hayo wakati wa kipindi cha mvua walilazimika kuzichimbua barabara hizi na kuweka misingi.

Mhe. Naibu Spika, hili lilitokana na tatizo la maji kutaka kuingia ndani ya majumba ambayo kuwa wanaishi wananchi hao wanaotoka Kiuyu Minugwini, Penjewani mpaka Kangagani. Niiombe Wizara kwa kushirikiana na wafadhili ambao kuwa au wakandarasi waliokubaliana kuzijenga barabara hizi wakubaliane waweke mabomba ya kupitisha maji kwenye barabara hizi ili kuondosha usumbufu au maafa ambayo yanawapata wananchi wakati wa kipindi kikubwa cha mvua za masika.

Mhe. Naibu Spika, wakati barabara hizi zinatengenezwa baadhi ya barabara hizi mlikuwa mmepita mabomba ya maji ambayo kuwa wanatumia wananchi. Mabomba haya mpaka leo hayajaingizwa kwenye barabara hizi. Wananchi wanaoishi kwenye barabara hizi wanapata usumbufu mpaka leo hii. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anipe maelezo ya kina kuhusu mabomba haya ya maji yamefikia hatua gani mpaka kufikia leo hii bajeti hii inapochangiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Kilimo. Niwapongeze sana Wizara ya Kilimo pamoja na changamoto nyingi walizonazo, lakini wametekeleza mengi tu Wizara hii ya Kilimo. Pamoja na changamoto zote hizo zinazowakumba, niiombe Wizara ya Fedha, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunakaa hapa tunapitisha bajeti, tukishakupitisha bajeti matokeo yake Wizara ya Fedha hawawaingizii fedha kwa wakati na wanapowaingizia fedha kwa wakati wanawaingizia fedha ambazo kuwa hazitoshi kukidhi yale malengo ambayo kuwa wameomba kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ya Kilimo, Chuo cha Kilimo Kizimbani kimepatiwa mradi wa maendeleo kufikia mwezi wa *April* 2015 fedha zilizopatikana kwa kazi za maendeleo ni asilimia 60 na ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani ni asilimia 45 tu. Hili ni jambo la kusikitisha kabisa kwenye Wizara kama hii ambayo kuwa ndio uti wa mgongo wa nchi hii. Leo mpaka sasa hivi wamepewa asilimia 45 ya ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Naibu Spika, Mapinduzi ya Kilimo hayapatikani tu kwa maneno. Mapinduzi ya Kilimo yanapatikana kwa vitendo. Ikiwa Mhe. Rais anatamka kwamba sasa hivi

kilimo kitapewa kipaumbele. Ni kipaumbele gani ambachokuwa Wizara ya Fedha wameipa Wizara hii ya Kilimo. Pembejeo hazitoki kwa wakati, matrekta ukienda Pemba, ukija Unguja unaambiwa matrekta sijui mawili ndio yanayofanya kazi, yaliyobakia yote ni mabovu.

Hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, mwaka jana tuliidhinisha hapa kulinunuliwa matrekta, matrekta yale mengine yalipelekwa Mafunzo, mengine yalikwenda kwenye Wizara ya Kilimo. Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha katika ziara zetu za Kamati tuliyakuta matrekta yale mengine yameshaanza kuwa mabovu. Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Zanzibar walio wengi ni wakulima, wanategemea wizara hii iwasaidie.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mradi wa ujenzi wa Kituo cha Usarifu wa Mazao Kizimbani. Mradi huu wa Kituo cha Usarifu wa Mazao Kizimbani umekuwa ni mradi ambao unatajwa tu, kwa sababu tayari wameshapatiwa zana za kufanyia kazi lakini cha kusikitisha zana hizo mpaka leo ziko bandarini na zinaharibika.

Mhe. Naibu Spika, kituo hiki ni muhimu sana katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Wazanzibari wana matunda mengi, maembe, mananasi, machungwa na mengineyo. Kama kituo hiki kitamalizika basi Wazanzibari watafaidika sana, cha kusikitisha kabisa Wizara ya Fedha, na Waziri anisikilize asizungumze, cha kusikitisha Wizara ya Kilimo waliomba fedha lakini masikitiko makubwa kituo hiki hakikuingiziwa fedha, kituo hiki mpaka kimalizike kinahitaji shilingi milioni mia nne. Sisi wanakamati tulilazimika kupunguza fedha kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara hii ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, je, tuko tayari? Hivi Serikali ipo tayari? Wakati kituo hiki ni muhimu tunasubiri wafadhili, kila kitu tunategemea wafadhili tu, tutategemea wafadhili mpaka lini, *abebwaye hujikaza! (Makofi).*

Mwalimu Nyerere alisema uchumi tunao lakini tumeukalia, matokeo yake ni haya. Wizara hii ya Kilimo inajitahidi kutafuta fedha, imevuka lengo la kutafuta fedha lakini matokeo yake milioni mia nne tu hazikupatikana kupewa Wizara ya Kilimo, Chuo cha Kilimo Kizimbani kumaliza kituo hiki.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja asilimia mia moja nikijibiwa pamoja na kuwa ni Mjumbe wa Kamati, hoja zangu zitakapojibiwa naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi na mimi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia

uhai mpaka muda huu tukaweza kukutana mahala hapa katika kufanya majukumu yetu.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi niweze kusema machache katika Wizara hii ya Kilimo.

Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze uchangiaji wangu katika ukurasa wa 5 ambao unasema Kilimo cha Maweni. Kilimo cha maweni kama tutakifuatilia vizuri kuna uzalishaji mzuri unapatikana, lakini bado inatakiwa juhudi kubwa ya kuwahamasisha watu wetu waweze kushiriki katika kilimo hicho cha maweni.

Mhe. Naibu Spika, mfano upo Pete niliuona nilikwenda kutembelea sehemu nikakuta kuna migomba ya umwagiliaji yaani ndizi hata kuinyanyua huwezi.

Kwa hivyo bado iko fursa kubwa katika Serikali ya kuweza kuwashawishi walimaji hawa, ili tuweze kuitumia vizuri sehemu ya maweni kuna uzalishaji mkubwa na mzuri na kweli ardhi yake ina rutba nzuri. Na kumeelezwa hapa kuna kilimo cha ndimu, yaani watu tukijitahidi kulima, sasa hivi tunahisi bado kwa kuwa hatujawa na viwanda vya kusindika ndimu zetu, lakini kwa baadae Serikali kila kukicha inaendelea kujipanga tutakuja kuweza kufanikiwa baadae kupata viwanda na sisi ili zije zitufae katika maisha yetu.

Kwa hivyo naiomba Serikali izidi kuhamasisha wananchi wasipuuze kulima kilimo cha maweni, manufaa yapo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 7 ambapo kuna Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Wizara katika malengo yake ya mwaka 2014/15 lengo lake moja lilikuwa kutayarisha michoro ya miundombinu ya umwagiliaji na ikataja mabonde yenyewe ambayo yanakusudiwa kuyafanywa hivyo.

Kwa kweli kilimo cha umwagiliaji kama Serikali itajikita katika kilimo hiki ndio kilimo ambacho kinaonekana kitakuwa na manufaa makubwa. Kwa sasa tunaona hali ya hewa ilivyo, kwa kweli mvua saa nyengine zinatukataa, kwa hivyo kilimo cha umwagiliaji ndio kitakachokuwa mkombozi. Kwa hivyo niiombe Serikali kweli kujikita nguvu zake katika kilimo hiki basi hii michoro iendelee, na hatimaye

utekelezaji wake upatikane ili kilimo hiki kiweze kufanikiwa na wananchi waweze kufaidika nacho.

Mhe. Naibu Spika, pia niiombe Serikali kuangalia mashamba haya ya umwagiliaji, endapo hiyo mbinu inayokusudiwa kufanyika itaweza kutekelezwa. Kwa hivyo kwa sababu katika kilimo ukiangalia kuna wengine wanalima eneo hili, eneo hili linaachwa, eneo hili linalimwa, eneo hili linaachwa. Kwa kweli hii haileti sura nzuri katika kilimo, ni vizuri mabonde tunapoyalima basi yaweze kulimwa yote kwa pamoja, na yaonekane mashamba yale yako safi na kitakachopatikana pale kiweze kuwa na manufaa kwa wananchi.

Niiombe Serikali labda kuna watu saa nyengine na sasa tuna upungufu wa ardhi, na kuna watu wanahitaji kulima lakini hawana sehemu za kufanya kilimo hicho. Kwa hivyo tunapoona mtu hatolima, yeye mwaka huu anapumzika, basi aweze kumpatia fursa mwenzake kwa makubaliano maalum; wakubaliane ambapo kutakuwa na ushahidi kamili kwamba hii sehemu si yako umeazimwa ulime lakini ili uweze kulima na zile sehemu zisikae wazi, ili wale ambao hawana sehemu za kulima na wao wawe wanapata maeneo kwa makubaliano maalum.

Mhe. Naibu Spika, pia katika Wizara hii miongoni mwa malengo yake imeeleza juu ya kilimo hiki cha alizeti, haya mafuta ambayo yameonekana hapa kumekamuliwa mafuta tani 6.5 za mafuta ya alizeti. Lakini pia kumepatikana lita 422 za mafuta haya na kilo 863 za mashudu.

Mimi niiombe Serikali kwa sababu hiki kilimo kwetu bado ni kigeni, mimi sijaelewa mpaka sasa hivi haya mashamba ya alizeti yapo wapi na wapi mpaka muda huu, kwa hivyo ningeomba kwa faida ya kilimo hiki ili wananchi wajue sasa kama kuna kilimo ambacho nacho kinaweza kikawaingizia mapato.

Kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja hapa tueleze haya mashamba ya alizeti yako mahala gani, lakini katika haya mafuta yaliyokamuliwa na haya mashudu nayo yana kazi ili watu waweze kuhamasika juu ya kilimo hiki, waweze kukipa na wao kipaumbele wananchi wakilime ili waweze kupata manufaa makubwa.

Pia niipongeze wizara hii kwa kufikia mafanikio makubwa, na kwa kweli wenzangu wamesema hapa kama katika watu wenye wataalamu wengi basi ni watu wa Wizara ya Kilimo, hongereni sana kwa juhudi zenu hizo, lakini tunataka hii elimu sasa iwasaidie wananchi katika kilimo chetu ambacho tunaendelea nacho.

Kwa kweli wakulima wanajitahidi kulima lakini bado wataalamu hawajaongeza juhudi za kuwapatia elimu hiyo, lakini sisi tunawashukuru kwa kuwatayarisha hawa wataalamu, mumejitahidi kufundisha wanafunzi lakini hata Idara ya

Uendeshaji na Utumishi pia inaonekana kuna wafanyakazi 100 ambao wanawaendeleza kimasomo. Hili ni jambo zuri na la kupigiwa mfano, lakini elimu hii basi irudi sasa iwasaidie wakulima wetu katika kilimo chao ili na wao waweze kulima kisasa waweze kupata mafanikio makubwa katika kilimo hicho.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu huu katika ukurasa wa 10 ambapo utekelezaji wa malengo ya mwaka pia inaonekana kuna utafiti wa mazao ya mboga mboga na matunda katika soko la kitalii.

Hili ni jambo zuri na siku zote huwa tunalalamika wakulima wanajitahidi kulima lakini bado wanahangaishwa sana na masoko. Kwa kweli soko ni tatizo, na utalii kwetu upo, kwa hivyo kama Serikali kweli itajikita katika kufanya hili, wananchi wetu wanaweza wakafaidika, wakalima na wakaweza kupata fedha nzuri kwa kutegemea mazao yao watayauza katika sehemu za watalii.

Mhe. Naibu Spika, pia nikiendelea na mchango wangu huu niende katika ukurasa wa 14 kwenye Idara ya Kilimo. Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalamu, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, pamoja na utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao yanayosafirishwa na kuingizwa nchini.

Mhe. Naibu Spika, lengo hili ni zuri, lakini niseme bado tunahitaji usimamizi mzuri. Kwa sababu pembejeo hizi na zana hizi za kilimo zinachelewa kuwafikia wakulima, wakulima wanalimiwa lakini si kwa wakati ule ambao wanautarajia.

Kwa hivyo Serikali bado inatakiwa iongeze juhudi zake ili zana hizi basi ziweze kuwafikia wakulima kwa wakati muafaka. Lakini pia jambo zuri kabisa ni hili la utibabu wa mimea.

Mhe. Naibu Spika, wakulima huvunjika moyo pale wanapolima mazao yao na baadaye yakakumbwa na msukosuko wa maradhi lakini wakakosa watu wa kuwapa utaalamu huu au wa kuwatibia mimea yao, ili na wao wakaweza kupata faraja maalumu.

Sasa kama jambo hili lipo katika mpango, basi niombe Mwenyezi Mungu awajaalie muweze kufanikiwa haya ili wakulima na wao wawe na watu wa kuwasaidia.

Pia kuna kipengele kinachoendelea kusema kuendeleza kazi za karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia kutoka nje ya nchi, ikiwemo karafuu kwa ajili ya usafirishaji na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, hili kwenye kitabu lipo lakini sijui kama katika vitengo vyetu lipo rasmi, kwa sababu nakumbuka sisi tulipopita katika *airport* ya Pemba wakati tumepita na kamati yetu tukawa tunauliza hapa kuna kitengo cha afya tukaambiwa kipo lakini hakina dawa.

Watu wa kilimo hapa wapo tukaambiwa hapa hawapo, maana hata ofisi hawana. Kwa hivyo hili ni suala muhimu sana, kwa sababu kunaweza sisi saa nyengine tukakuta mazao yetu yanapata maradhi lakini kumbe yanasababishwa na miti, watu wamesafirisha kutoka mahala kwengine na wakapeleka mwahala kwengine.

Sasa kudhibiti hizi sehemu za usafiri kuwa na vitengo hivi vya kilimo ni jambo muhimu sana, kwa sababu mimi mpaka Mkokotoni hapo nishawauliza, kitengo hiki mnacho? Na pale kunapitishwa wanyama wanasafirishwa kutoka wapi na wapi. Inawezekana wakashushwa wanyama wana maradhi, au ikashushwa miti ina maradhi ikaletwa katika nchi yetu, na ikaathirika nchi yetu kwa kuwa tumekosa uangalifu wa maeneo haya. Kwa hivyo Serikali niiombe kushukughulikia vile vitengo vyote vinamopitishwa hii miti katika kusafirishwa, waweze kuwa makini juu ya hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuna jengine linaeleza utafiti wa ukuaji wa miche ya mikarafuu kwa kutumia udongo tofauti unaendelea katika kituo cha utafiti cha Matangatuani.

Hili suala la utafiti na kweli wizara yenu hii inajitahidi kufanya tafiti mbali mbali, tunakupongezeni sana lakini utafiti huu wa mikarafuu ni jambo muhimu, kwa sababu sasa wakulima tunajikita sana katika kuona tunarejesha hali ya mikarafuu, kwa sababu hapo nyuma tuliikata sana, lakini sasa mnavyotoa miche mnatuhamasisha kupanda, lakini tunapandaje bila ya utaalamu?

Kwa kweli mikarafuu tunaipanda inayopona michache na inayokufa mingi, lakini pengine tungeweza kupatiwa hii elimu mapema tungeweza kuotesha mikarafuu ile kwa utaalamu na pengine tungeweza kufanikiwa kuiponesha mingi.

Kwa hivyo hili ni suala muhimu Mhe. Waziri mimi naomba hili litiliwe mkazo, kwa sababu mikarafuu tunapanda lakini inayopona michache. Pia mimi sikuoneni kama mnakuja kutukagua, nani kachukua mikarafuu au mbinu gani, au mbiu gani mnatupigia kama jamani ee wakulima wetu wa mikarafuu hebu mnapopata miche tulieni, watakuja wataalamu ili wakufahamisheni taratibu, tunajipandia tu kiholela.

Kwa hivyo Mheshimiwa ni vizuri jambo hili mkalifanyia utafiti wa kina, na hatimaye likaweza kuleta mafanikio makubwa nchini kwetu, kwani sasa hivi tukiweza kuipanda mikarafuu kitaalamu maana yake itaweza kuzaa kwa muda mfupi, na wakulima wataweza kufaidika na hilo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Katika malengo haya kwa mwaka 2014/15 lengo lao moja linasema kuotesha miche milioni moja ya misitu na miche laki tano ya matunda na viungo katika vitalu vya Serikali, na kuzalisha miche milioni moja ya mikarafuu.

Kwa kweli hili mimi bado ninasisitiza miche kweli ipo, miche inatolewa, lakini ni kiasi gani mnafuatilia kuona sisi tunaopanda miche hii au Serikali huwa ina mbiu yake ya upandaji wa miti, na tunaona zoezi lile linafanyika, lakini je hurudi nyuma baadae kuhesabu ni miti mingapi tuliyoipanda mwaka ule imeweza kuota au tukishapanda ndio basi.
Kwa hivyo hili zoezi ni muhimu sana, lakini tunahitaji baadae kuwa na mrejesho wa kujua kiasi gani tumeweza kufanikiwa, kwa mwaka huu tumepanda miche mingapi, na mingapi imeota na mingapi ilikufa. Kwa hivyo hili tukilisimamia vizuri, maana yake tutaweza kuwa na miti kila wakati na mvua kwetu zitaendelea kuonekana.

Pia kuyatambua na kutayarisha mpango wa usimamizi wa mashamba ya Serikali. Mheshimiwa hili ni jambo ambalo mnaliacha na mnalitupa sana, ni kweli mashamba ya Serikali yapo tu. Niseme tulikuwa na shamba linaniuma bado kila siku nikichangia wizara hii nalisema, kulikuwa na shamba Kipange la Ufugaji wa Ng'ombe, shamba lile limeondoka na hatunalo mikononi mwetu wala hatujaona mbadala ambalo tumepatiwa.

Kwa hivyo jamani ni vizuri mashamba haya yanapowekwa yanawekwa kwa malengo maalum, na yakiondoshwa basi wananchi waambiwe limeondoshwa kwa sababu gani na wamepatiwa jengine mahala gani.

Kwa hivyo Mheshimiwa ni muhimu sana kuzitambua hizi mali za Serikali. Mali za Serikali huwa tunaziachia muda mwingi, tunaziachia pengine bila ya kuziwekea utaratibu wa kuzizingia, matokeo yake huwa zinakuja kuingiliwa na kumegwa taratibu na watu, baadae tunakuja kupata shida ya kuanza kuzitafuta wakati ambapo tayari zimeshamegwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 25 ambapo kuna Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Mhe. Naibu Spika hili ni jambo muhimu, na tulilisema na tulilipokea kwa furaha kubwa wakati tulipoletewa mswada hapa na Mheshimiwa yule mwenzetu ambaye kwa sasa hapa hatunaye Mhe. Mansour Yussuf Himidi.

Alileta mswada wake huu na tuliupokea kwa furaha kubwa, kwa kuona sasa serikali inajitayarisha kuwa na uhakika wa chakula kwani uhakika wa chakula ni jambo muhimu, tunaishi lakini lazima tuwe na akiba ya chakula.

Na mimi nilisema hapa wakulima mnawaachia mahindi yao wanayavuna mabichi, wanayachoma, hakuna mahindi makavu ya akiba, siku likitokezea wala Mungu asitujaalie, lakini siku likitokezea tutahangaika, kwa sababu hakuna chakula cha akiba, tunachopata tunakula chote kwa wakati mmoja. Hili si jambo zuri, Waswahili wanasema *"akiba si ubahili"*, kwa hiyo sasa kuwa na akiba ya chakula ni jambo muhimu.

Halafu kuna ghala hili linalojengwa, ni muda mrefu kweli tangu ulipoletwa ule mswada tunaambiwa kuhusu hili ghala.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu kweli wizara yetu ina ufinyu labda wa bajeti, lakini mimi niseme lazima tujipange katika masuala mengine. Masuala mengine ni muhimu lazima tukate pua tuunge wajihi, ili mojawapo tulipate, isiwe tuna miradi hii tele lakini mwisho wa siku hatukufanikiwa hata mmoja, lakini tukisema tuache hili tufanye hili moja tunaweza tukafanikiwa. Kwa hiyo, kuwa na ghala la akiba ili tukaweza sasa kujiwekea akiba ya chakula, jamani ni jambo muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, hii Idara ya Maji tayari niliielezea kama kuna umuhimu wa kuwa na mashamba haya ya umwagiliaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mchango wangu ulikuwa ni huo. Naomba tu nichukue fursa hii kuipongeza sana wizara hii kwa jitihada zake, na *inshaallah* ongezeni jitihada hizo, kwa sababu wizara hii sisi ndio mkombozi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kilimo kama walivyotangulia wenzangu kusema, ndio uti wa mgongo. Huu ndio uti unaowasaidia wanyonge, wanyonge wote wanapitia katika kilimo, lakini hata na wenye uwezo wao pia wanashiriki katika kilimo. Kwa hiyo, ni vizuri wizara hii tukaipa kipaumbele kama tunavyozipa wizara nyengine, kwa sababu Wizara ya Afya ni muhimu, mtu kama afya yake sio nzuri atakuwa hawezi kushughulika na majukumu ya kazi. Lakini Wizara ya Elimu pia ni muhimu kama mtu hakupata elimu anaweza akashindwa kufanya majukumu yake mengine. Lakini na wizara hii ni muhimu sana kama hujala huwezi kuja kufanya chochote.

Kwa hiyo, naomba sana wizara hii nayo tuipe kipaumbele, kuona lazima tuwe na chakula, lazima tuwe na vitendea kazi katika kilimo ili wakulima waweze kufaidika na kilimo chao, na waweze kujizalishia mali, lakini pia usarifu wa mazao ambao humu mumeuzungumza ni jambo muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika wakulima wana mazao yao mengi, lakini bado hawajui vya kuyafanya, hatimaye yanaoza. Tukiweza kuwafundisha usarifu wa mazao, wakulima wanaweza wakapata faida kubwa, hivyo naiomba wizara sana kuyaangalia haya kwa umakini ili wananchi waweze kujitegemea katika kilimo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja wizara hii. Ahsante.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia akanipa hazina ya uhai wake na uzima, nikafika hapa kusimama kwenye Baraza hili kwa ajili ya kazi maalum ya kuwatetea au ya kuwasemea wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze Mhe. Kaimu Waziri kwa dhati kabisa jinsi alivyosoma hotuba hii kwa umakini na ikafahamika vizuri. Pia sitokuwa mwizi wa fadhila, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu, Mwenyezi Mungu awazidishie imani na mapenzi juu ya nchi yao, ili tufanikiwe katika nchi hii juu ya suala la kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kama wenzangu waliotangulia walivyosema kama kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni roho, kilimo ni kila kitu katika nchi hii na nchi nyengine za jirani.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais katika hotuba yake ya mwanzo hapa tulipoingia kwenye Baraza alilizungumzia suala hili la Mapinduzi ya Kilimo kwa nia safi.

Mhe. Rais alilizungumza lile kwa sababu maalum ya kuwapenda wananchi wake, na kuona kwamba kilimo ndio kila kitu katika nchi hii. Hivyo akaona katika kuwasaidia wananchi wake wa nchi hii na kuwajali aelezee hili suala la Mapinduzi ya Kilimo, lakini kwa bahati mbaya yamekuwa ni vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Wizara hii ya Kilimo inaonesha bajeti yake ni ndogo, na wizara hii mambo yake yote hakuna hata suala moja ambalo linatakiwa litumie pesa kidogo, linataka litumie pesa nyingi ili kuonekana tunafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze katika ukurasa wa 3 mwanzo kabisa hapa kuna mwaka 2014 ukuaji wa sekta ya kilimo.

Hapa mwanzo tu unaonesha kama umeshuka kwa asilimia 0.4 kutoka wastani wa asilimia 13.2 ya mwaka 2013, wakataja miongoni mwa sababu zilizochangia ushukaji wa ongezeko hili la kupungua kwa eneo lililolimwa la uzalishaji kutoka ekari 94,701 hadi ekari 87,944, na sababu nyengine wakasema miongoni mwa hizo sababu ya kukosekana hilo ni hali ya hewa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nikubaliane na hali ya hewa, kwa sababu hali ya hewa ni makadirio ya mwenyewe Mwenyezi Mungu, ijapokuwa na sisi binadamu tunasababisha kwa njia moja au nyengine katika hatua nyengine, lakini hili nikubaliane nalo.

Mhe. Naibu Spika, hapa itabidi niulize swali wanasema ni kukosekana kwa eneo lililolimwa la uzalishaji. Sasa naomba hapa Mhe. Kaimu Waziri anipe ufafanuzi zaidi eneo hili lililolimwa limekosekana kivipi, kwa sababu pengine vifaa vya kulimia vilikuwa hamna au hilo eneo lilikuwa na matatizo gani mpaka likakosekana, hapa ikawa upungufu mmoja uliopo huo ni kupungua mpaka kufikia ekari hizo kutoka mwaka 2013 na 2014.

Mhe. Naibu Spika, hali ya uzalishaji pia imeelezwa katika ukurasa huo huo, imeelezwa inaonesha kupanda kwa baadhi ya mavuno, na katika baadhi ya mavuno waliyoyaeleza wakaweka kwenye kiambatanisho namba 1.

Na katika kuangalia ni kweli baadhi ya mavuno yamepanda sana, lakini sasa niwapongeze hawa waliofanya utaratibu huu hapa yakapanda haya mavuno baadhi yake kama viazi na mananasi; kutoka tani hizo 11,583 kwa mwaka 2013 mpaka 13,258.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna changamoto zake katika haya mambo yaliyopanda na kuongezeka pia kuna changamoto zake, kwa sababu tunayaona maeneo ya wenzetu mengi tu hapa Pemba na Unguja kuna watu wamejitokeza sana na kuitikia wito wa kilimo katika kupanda hivi vitu vilivyoonekana hapa kama mboga mboga, mananasi, viazi. Lakini sasa kwa bahati mbaya sana ukifika msimu wa vitu hivi Mhe. Naibu Spika utavionea huruma, hawana pa kuviuza, sisi walaji tuliopo hatuvimalizi, na lengo lao ni kula na biashara pia ili na wao wapate kujiendeleza kimaisha.

Sasa naiomba wizara inijulishe wamechukua hatua gani ya kuwasaidia hawa katika kuwatafutia masoko, ili mazao yao haya wapate nguvu zaidi na wao mara nyengine wapate kuongeza mradi huu na ilimradi wapate mafanikio zaidi. Lakini kama wataendelea na kuwa wameongeza uzalishaji na pa kuuzia hapana, inakuwa ni tatizo na watavunjika moyo. Mara nyengine watabakia vile vile na yale Mapinduzi ya Kilimo yatakuwa hayakufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, tukija kwenye kilimo cha maweni. Wamezungumza wenzangu kilimo cha maweni kama Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikiongeza nguvu katika kuendeleza kilimo cha maweni ikiwa kilimo cha ndimu, mbaazi, mtama, uwele na viazi vikuu; kwa mazao ya chakula na biashara, jambo ambalo limewapa wakulima tija ya haraka na kipato kizuri.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli nakubaliana na hili lakini nataka niseme katika maeneo ya Kusini niliyoyatembelea katika msimu wa ndimu utazikuta ndimu zimezagaa ndani, maana yake yale mashamba yenyewe hata wakisema wazichukue wazipeleke mjini basi ile gharama ya kuzitoa kule katika maeneo yao mpaka kuzifikisha mjini, basi hailipi, kwa sababu inafika wakati fungu la ndimu la shilingi 500 wewe unayelinunua unawaonea huruma.

Sasa hapa ningeishauri wizara na serikali, kwa jumla wangetutafutia angalau wakulima hawa, kwa sababu sisi tunanunua achari za ndimu madukani kichupa kidogo sana kwa shilingi 2500 au 3000, kwa nini hawawafanyii utaratibu wowote ule wa usarifu wa mazao haya, angalau kiwanda kidogo ili na wao wakanunua wakawatafutia wawekezaji wakanunua hizi kwa bei kubwa na wao wakapata manufaa.

Mhe. Naibu Spika, kinyume na hivyo tutakuwa tunaendelea kuwahamasisha wananchi wetu kujikaza kupanda lakini matokeo yake kama nilivyolizungumza hawapati maeneo mazuri ya kuuza biashara zao na wanabakia kuwa masikini. Lengo la Mapinduzi ya Kilimo ni kuwatoa wananchi katika umasikini na kuwaweka katika kipato chengine.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna wizara imeotesha miche ya mikarafuu Unguja na Pemba. Sasa Mhe. Naibu Spika, juu ya kuwa miche mingi wanasema wameiotesha Wizara ya Kilimo, na kwa sababu Wizara ya Kilimo wenyewe binafsi wana mashamba yao ya kilimo, na wao pia wanachukua miche hii hii wanaisambaza katika mashamba yao ya serikali. Sasa katika kusambaza watu binafsi wako wengi waliohamasika katika kupanda na kuhuisha zao letu hili la karafuu, lakini kwa bahati mbaya hii mikarafuu juu ya kuwa watu wanaiotesha kwa wingi lakini haitimii na watu hawafanikiwi, ukitaka miche 50 unapewa miche 20, ukitaka miche 10 unapewa miche 5.

Sasa naiomba Wizara ya Kilimo wafanye utafiti katika vitalu vyote wanavyopanda vya watu binafsi pamoja na vya serikali, ili kujua kama watu katika msimu huu kabla ya ule muda wa kupanda, wajue ni idadi ya watu wangapi wanaohitaji mikarafuu, halafu na wao angalau wapate asilimia japo 50 ya watu wanaotaka wapate ile mikarafuu ya kuhuisha zao letu kwa vizazi vya sasa na vya baadae.

Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze Wizara imefanikiwa kununua mtambo wa kukamulia mafuta ya alizeti.

Wenzangu wengi wamesema hili ni jambo zuri lakini liwe jambo endelevu, lisiwe jambo la kupita ikawa imenunuliwa kesho inaharibika hakuna jengine la kufanya. Naomba hapa liendelezwe sana hili suala ili tupate mafanikio.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye ukurasa 14 kwenye Idara ya Kilimo. Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalamu, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na utibabu wa mimea.

Mhe. Naibu Spika, kwa uandishi wa ndani ya kitabu hili suala ni zuri sana, lakini kwa utekelezaji lina ugumu unapofika wakati wa msimu wa kilimo.

Mhe. Naibu Spika, haya yaliyoambiwa hapa yote; huu usimamizi, sijui tuseme wasimamizi wanakuwa wachache au pengine hizo zana zinakuwa hazipo, lakini kiukweli watu wetu wanapata tabu sana katika kupata matrekta, kupata hizo pembejeo, kupata na vitu vyengine vyote.

Kwa hiyo, naiomba serikali iwe makini katika suala hili la kufuatilia ili wakulima wetu wapate zana hizi mapema, na serikali kupitia wizara iwatafutie wizara hii hivi vifaa ili watu wafanikiwe, kwa sababu watu wengi katika maeneo yetu wanatumia matrekta ya watu binafsi, na ni gharama kubwa mno ambayo hawaimudu, wakati matrekta ya serikali yapo lakini pia yanakuwa hayakidhi haja, hayatoshi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye ukurasa wa 24 kuna mpango umetayarishwa wa kujikinga na matukio ya moto. Uchimbaji visima 11 katika maeneo ya Jozani na Ghuba ya Chwaka, Jambiani, Muyuni, Kiwengwa na Pongwe.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika misitu yetu matukio mbali mbali yanajitokeza ya moto yanayosababishwa na sisi wenyewe wananchi kwa sababu tofauti; wengine pengine wanakwenda kwa kufua nyuki, wengine wanaingia wanavuta sigara wanaacha vipande ovyo ndio inatokezea haya matatizo.

Sasa katika kuhuisha misitu yetu ambayo baada ya kukosa hii misitu kuungua moto sisi tunapata matatizo makubwa, mpaka ndio hali ya hewa inaanza kuchafuka. Sasa nawaomba sana wizara wawe na mikakati maalum ya kuilinda misitu yetu kwa maslahi ya nchi yetu, na watu wetu wanaokuja hapa kwa kuangalia misitu yetu, misitu ni mali sana.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwapongeze wizara hii kwenye Idara ya Umwagiliaji kwa kuchimba visima viwili katika vituo vya Kibondemzungu Unguja na Ole kwa Pemba. Pia nataka niwape pole katika suala hili. Nasema niwape pole kwa sababu gani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana na ndio tegemeo letu, lakini Mheshimiwa katika kitu chenye gharama ni hiki, na ukiangalia bajeti za Wizara ya Kilimo ni ndogo mno na kupandisha maji katika visima vyetu na kupeleka katika mashamba yanataka gharama za umeme, na gharama za umeme ni kubwa, na sifikirii kama Wizara ya Kilimo au idara hii inaweza kumudu gharama hizi za kulipia umeme. Bila ya bajeti kuwa kubwa basi na hili litakuwa ni tatizo kwetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka nije katika ukurasa wa 44 kwenye kiambatanisho namba 2. Hapa kuna taarifa ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka pamoja na makusanyo kuanzia mwezi wa Julai, 2014 hadi Aprili, 2015 halafu kuna makadirio na hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika Ofisi Kuu Pemba kuna idadi ya mazao ya misitu, ada ya uuzwaji wa mawe na mchanga.

Ada ya uuzaji wa mawe na mchanga Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2013 kwenye mazao ya uuzaji wa mawe na mchanga inaonekana imeshuka. Sasa kwa sababu inaonekana sasa hivi wajenzi wameongezeka wanaotumia vifaa hivi vya mawe na michanga ni wengi ukilinganisha na hii idadi iliyoshuka.

Sasa naiomba wizara ikija hapa inieleze kwa nini imeshuka, itakuwa imeshuka kwa sababu watu hawajengi au kwa sababu pengine hawa watendaji waliowekwa hapa katika kufuatilia suala hili hawafanyi wajibu wao.

Pia nikija kwenye ukaguzi wa mauzaji ya mazao na miche. Hapa kuna makadirio milioni 500 lakini ukija huku pia inaonekana kwenye hali halisi hamna kitu. Sasa hapa nataka niulize katika maeneo haya haikuuzwa hii miche mpaka ikawa hapa hamna kitu au imekuwaje. Sasa naomba pia Mhe. Kaimu Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi katika mauzo ya miche kwenye ukurasa huu wa 44.

Mhe. Naibu Spika, halafu pia katika ukurasa wa 45 kuna mauzo ya miche na ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu. Katika makadirio ya ukodishaji wa mashamba ya mikarafuu kuna milioni 5, lakini katika uhalisia hapa hamna kitu na huku pia hamna kitu.

Sasa naomba kujua hapa, kwa nini hamna, karafuu hazikuzaliwa, haya mashamba labda hayajulikani, pia katika hili naomba nimwambie Mhe. Kaimu Waziri anipe idadi ya mashamba yaliyopo ili tujue mashamba yetu ni mangapi mpaka tukajua

makadirio haya au makadirio haya shilingi milioni 5 kwa uuzaji au ukodishaji wa karafuu ni madogo mno, kwa sababu katika kitu amacho ni mali ni karafuu.

Sasa ukiona mashamba ya mikarafuu tuliyonayo Wazanzibari Unguja na Pemba; hasa katika Kisiwa cha Pemba, tuna mashamba makubwa ya mikarafuu, kwa ufahamu wangu mimi ninavyoelewa naona yanakodishwa kwa pesa nyingi, lakini hapa makadirio ni shilingi milioni 5. Sasa Mhe. Naibu Spika naomba Kaimu Waziri anifahamishe idadi ya mashamba, ili tuyajue mpaka yakawa makadirio ni madogo kiasi hiki.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie kwa suala ambalo wamelizungumza sana wenzangu hapa, suala la usarifu wa mazao, naomba nilizungumzie tena.

Mhe. Naibu Spika, tuna matunda ya aina nyingi katika visiwa vyetu viwili hivi. Katika msimu wa embe huwa kuna embe mpaka nyengine huna vya kuzifanya, bado naendelea kusema tunanunua kichupa cha juisi ya embe kwa shilingi 800 ambacho kuwa yule mtoto mchanga ukimpa basi haridhiki anataka apewe nyengine. Lakini ukitizama embe zilivyozagaa zinatembezwa kwa vi-*carry*, zinatembezwa kwa magari kila pahali tunaziona, akinamama wanafanya kazi hiyo wenye mashamba yao wanachukua embe wanazikusanya. Sasa je, ni lini serikali itaamua kutafuta japo mwekezaji kuja kutupatia kiwanda kidogo hapa angalau cha kusarifu matunda yetu, ili wananchi wa nchi hii wakaneemeka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii sina shaka nayo, lakini bado naiomba serikali isimamie Mapinduzi ya Kilimo kama alivyokuwa na nia nayo mwenyewe Mhe. Rais katika kufanya Mapinduzi ya Kilimo, isiwe Mapinduzi haya ya Kilimo yamo kwenye vitabu tu, lakini kwenye utekelezaji ikawa ziro. Nakushukuru.

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake, kwa kutufikisha hapa leo na tunajadili bajeti ya Wizara yetu ya Kilimo na Maliasili.

Vile vile nakupongeza na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia.
Mhe. Naibu Spika, mimi katika mchango wangu nitaanza ukurasa wa 5 kifungu cha (2)(4) Kilimo cha Maweni.

Mimi kama mdau wa kilimo hiki cha maweni leo nitachangia kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kitabu chetu kinasema kwamba, Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikiongeza nguvu katika kuendeleza kilimo cha maweni kikiwemo kilimo cha ndimu, mbaazi, mtama, uwele na viazi vikuu. Kilimo hiki kinalimwa sehemu

za maweni kweli, kuanzia Nungwi, Matemwe, Makunduchi, Bwejuu, mote humo mnalimwa kilimo hiki. Kwa vile na wizara yetu hii ya kilimo ni *fifty, fifty,* wanakijua sana kilimo hiki kwa sababu asilimia kubwa ya vilimo hivi kwa hivi sasa wanalima kinamama.

Mhe. Naibu Spika, kitu chochote kile kinataka elimu. Naiomba Wizara ya Kilimo na Maliasili ituletee wataalamu katika kilimo chetu cha maweni, kwa sababu tunalima sana kama vile mbaazi na ndimu, lakini hatulimi kiutaalamu, tunalima tulivyozoea.
Kwa hivyo, naiomba wizara ituletee wataalamu wa kulima kilimo hiki cha maweni.

Jambo la pili Mhe. Naibu Spika, hapa pametajwa kilimo cha ndimu, hivi sasa ndimu sehemu ya maweni inalimwa sana, wananchi wanalima vya kutosha, lakini wakati wa kuuza hizi ndimu zinakuwa hazina faida kubwa. Kwa sababu hakuna sarifa yoyote inayofanywa katika ndimu.

Ndimu itatolewa Matemwe iletwe marikiti, marikiti inamwagwa wanakuja watu pale kununua, wakishanunua nyengine zinawekwa hapo hapo na hizi ndimu zina kawaida wakati zinapokuwa nyingi basi hazitakiwi na mtu. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo, iwafanyie maarifa wananchi hizi ndimu zisarifiwe ili watu wapate kusafirisha, watafutiwe wananchi masoko, watafutiwe viwanda vidogo vidogo vya kuweza kusindika ndimu na embe. Tunaona juisi nyingi tu hapa za embe, lakini juisi zile zinatoka nchi za nje wakati ndimu tunazo, embe tunazo.

Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo, iwatizame wananchi kuwapatia faida kwenye kilimo chao ili wasivunjike nguvu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika sehemu ya utafiti. Mheshimiwa naiomba tena Wizara ya Kilimo ituletee watafiti.

Kule Matemwe zamani kidogo kulikuwa kunalimwa tungule nyingi sana, na zikiletwa tungule za Matemwe wakati huo basi mtu wa mjini yeyote anafurahika, anasema leo nitakula tungule, nitakula maloba; lakini hivi sasa tungule za Matemwe zimekutwa na maradhi. Kwa hivyo, naiomba wizara ije kufanya utafiti katika *area* hizi hasa Matemwe, watufanyie utafiti haya maradhi ya tungule yanakuja vipi.

Naiomba wizara, Mhe. Waziri akija hapa atuhakikishie kwamba atatuletea wataalamu kule Matemwe tufanye utafiti wa maradhi ya tungule. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika ukurasa wa 22; Misitu. Hivi sasa Zanzibar misitu hatuna, misitu imekwishakutumika kwa mahitaji ya wananchi.
Kwa hivyo, sasa hivi serikali kupitia Wizara ya Kilimo itabidi sasa wananchi wapewe miche ya miti ili waanzishe kupanda miti katika sehemu zao, hasa zile za mashamba zilizobakia bakia, huku mjini sisemi kwa sababu sasa hivi mjini hakuna pahali, mote mshajengwa. Lakini kuna sehemu za mashamba kama kwetu Matemwe sasa hivi watu wanahitaji wizara iwaletee miti tupande ili tuhifadhi.

Hali ya hewa yetu sasa hivi inakuwa mbovu kwa sababu miti hakuna. Kwa hiyo, naiomba serikali ituletee miche tupande miti hiyo wananchi ndani ya mashamba yetu.

Nikienda katika ukurasa wa 34 Ukulima wa Umwagiliaji.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ya Zanzibar haina mito mikubwa kama wenzetu. Hebu niiulize wizara itafanya rai gani hata mabonde tuliyokuwanayo kama pale Kehimarini pana bonde kubwa sana la mpunga, na wananchi wanalihitaji. Lakini wananchi wale hivi sasa ukulima wao kama haijafika mvua hawapati. Mhe. Waziri ningeliomba wakati atapokuja hapa awahakikishie wananchi wa bonde la Kehimarini kama watachimbiwa visima vya kumwagilia. Kwa sababu katika bonde ambalo liko kavu na halina maji ni lile pale, Kehimarini hapo Mhe. Waziri anapaelewa.

Kwa hivyo, wananchi wale nao wanahitaji maji, sasa ningeliomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo na pale pachimbwe visima vya kumwagilia pindi ukipatikana uwezo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukulima. Ukulima wa mpunga Zanzibar ni tegemeo sana, lakini sasa wakulima wa Zanzibar wanachelewa kulimiwa.

Aidha kwa ukosefu wa matrekta, wanachelewa kupanda na wanachelewa kuburugiwa mashamba yao. Kwa hivyo, naiomba wizara iwahakikishie wananchi kuwalimia kwa wakati, kwa sababu wananchi wengi wanakosa kulimiwa kwa wakati, na wanatoa pesa zao baada ya kutoa pesa zile ukulima haulimwi wanachelwa hatima yake wanakula hasara.

Kwa hivyo, mimi kidogo ningelipenda kumuuliza Mhe. Waziri mwaka huu hasa wakulima wangapi ambao hawakulimiwa, kama wapo watawachukulia hatua gani wengine wameshalipa pesa.

Vile vile wakulima wengine wana ukosefu wa kupata mbolea kwa wakati, wana ukosefu wa madawa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje atuhakikishie ni tatizo gani

ambalo wakulima wetu wanapolima haya madawa wanakosa? Ni tatizo gani wakulima wetu wakati wanapolima hizi mbolea wanazikosa? Ni tatizo gani wakulima wetu wa Zanzibar wanachelewa kulimiwa?

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi sivai buti wala kiatu cha ndara, lakini waziri aje atueleze tu, kwamba atahakikisha wananchi watalimiwa kwa wakati, watapewa mbolea kwa wakati na madawa yatakuweko kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutujaalia leo na ninamuombea Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili bajeti yake hii ipite, ili wakulima wetu walimiwe kwa wakati na hasa sisi wakulima wa maweni tuje tupate wataalamu, tutafutiwe masoko tuuze ndimu zetu, embe na hata mapapai.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki nafikiri kama yamo sijaona mapapai.

Mapapai vile vile ukulima wa maweni, maboga ukulima wa maweni. Kwa hivyo, haya yote yanataka utaalamu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja.

**Mhe. Abdalla Mohamed Ali:** Mhe. Naibu Spika ahsante.

Kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mola kwa zile neema zake alizonitunukia hajazichukua mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa hata sitaki nizungumze mengi naacha hiyo *NERICA* iendelee kunufaisha watu tu huku, lakini ikabidi kidogo nizungumze kwa sababu watu wengi hapa walizungumzia bonde la Makombeni, na unajua tena *"mcheza kwao hutunzwa"*. Huko ndio kwetu nataka na mimi niseme kidogo kuhusu hili bonde la Makombeni.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba ikumbukwe tu, kwa sababu Waheshimiwa wengi hapa walikuwa wanaisifia sifia kwamba hivi sasa wale watu wanaanza kulima mpunga, vi-*plot* vimeshawekwa na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, juhudi kubwa imepita pale, na naomba niwakumbushe Wajumbe kwamba kwa programu ya serikali basi bonde lile ilikuwa lianze kuzalisha tokea mwaka 2011, lakini limechukua miaka minne hadi hivi leo bonde lile ndio labda mwaka huu wananchi wataanza kuvuna. Kwa hiyo, hiyo inayoonekana kwamba labda ni kazi ndogo imepita wajue kwamba pale pamepita

kazi kubwa sana ya kuwaelimisha wananchi mpaka wakafahamu, kwamba angalau hicho kilimo cha umwagiliaji kitawawezesha au kitawasaidia namna gani.

Ninalotaka kusema Mheshimiwa kwamba hiki kilimo mimi nafikiri tulikurupuka, kusema kwamba tunataka kuleta Mapinduzi ya Kilimo. Mapinduzi acha yale, lakini katika kilimo naona kwamba tumefanya kosa kutangaza kuwa tunataka kuleta Mapinduzi ya Kilimo.

Mimi naona labda tuseme tunataka kuleta maendeleo katika kilimo lakini kuleta mapinduzi si rahisi.

Mhe. Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji mawaziri ni mashahidi hapo, hatujaanza kusema leo, serikali imeanza kuingiza pesa tokea mimi naingia katika Baraza lako Tukufu, na kwa taarifa yako nilikuwa katika Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo nikiwa ni Mjumbe wa Kamati inayosimamia mambo haya.

Nimezunguka Unguja na Pemba hayo mabonde yaliyotajwa ya Kibokwa, Mangapwani, Kibonde Mzungu, Kwa Jibwa, Kwa Punda yote tumeyapita na tumeona. Lakini Mheshimiwa ukienda kusema kweli unasikitika, ni taarifa tu unayoipata, lakini nyote ni mashahidi, kwa sababu tunakwenda huko mashamba tunaona.

Hivyo kuna bonde gani hivi sasa tunaloweza kulitilia maanani, tukasema hili limeanzishwa mwaka 2011, na serikali pamoja na wafadhili wameingiza fedha kwa ajili ya kilimo, lakini mpaka leo hakuna lolote lililokwenda.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikupe mfano mmoja sijui maeneo ya kwenda Kiwengwa kulikuwa na Mjapani pale, Mjapani yule aliweka kijishamba kidogo cha mfano ikawa mambo mazuri, watu wanakwenda wanajifunza na mengineyo, mbele yake kuna hicho kilimo cha umwagiliaji.

Juzi Mheshimiwa katika kutafuta chungwa za kula nikasema hebu nipitie kule, kuna siku nilipita nikaona pana kilimo cha umwagiliaji, nilisikitika sana nikakuta kwamba mashamba yale baada ya kuwa yamelimwa huo mpunga mengine yana mtama na mengine yana mahindi.

Kwa hivyo, mimi nafikiri serikali ingeangalia uwezekano mwengine, lakini kusema kweli tuna- *inject* pesa nyingi za serikali na pesa za wafadhili, ukiangalia hata ripoti ya mwaka huu basi inaonesha kwamba kilimo cha mpunga kimepungua.

Sasa sababu nini? Ikiwa pesa zipo, maji yanapatikana, kwa nini tena mpunga upungue?

Mimi nilitarajia kila mwaka tukienda mbele kwamba mpunga utakuwa unaongezeka, lakini matokeo hayo ninayokwambia kwamba yale mashamba ambayo tulikuwa tunatarajia yalimwe kilimo cha umwagiliaji, basi hivi sasa kuna mahindi, kuna mabamia na kuna viazi.

Mhe. Naibu Spika, bado serikali iangalie tena, na nafikiri kuna haja sasa ya kurudi nyuma kuangalia, hivyo kweli miaka mitano imeshapita tuna *progress* gani katika kilimo cha umwagiliaji?

Mhe. Naibu Spika, hili bonde la Makombeni muda wa miezi miwili iliyopita mimi na Mbunge tulikwenda kuwatembelea wananchi, lakini haja yao kubwa ni kwamba ule umeme hawana uwezo wa kuulipia, ikabidi tu-*inject*, tuingize pesa ili tukawasaidie katika kulipia umeme Mbunge na Mwakilishi ndio kazi zetu hizo. Sema ndiyo! Ndiyo kazi zetu za kwamba tukatie umeme kwenye mashamba ya kumwagilia.

Sasa huyo kama hajawezeshwa *from the beginning*, hivyo kweli ataliweza hilo shamba la umwagiliaji?

Hawa wananchi wa Makombeni wamewezeshwa ndio wakaingia ari ya kusema kwamba sasa sisi basi tutakwenda tukapige hivyo vi-*plot.*

Mheshimiwa hapa tuna-*inject* pesa zetu bure, kama ikiwa serikali imefanya utafiti, na hapa ndio nataka niiulize wizara, kwa sababu hapa tumeletewa habari mpya mimi naona kwangu kwamba hivi sasa kuna kilimo cha alizeti.

Kilimo hichi cha alizeti naona kimeshapewa kipaumbele. Sasa sijui niulize hii taasisi haya ni mazao ya Taasisi yetu ya Utafiti, kwamba wamefanya utafiti wakaona kwamba zao hili la alizeti linamea na linaweza likawanufaisha wananchi wetu au ni vipi. Limetokea tu matokeo mtu mmoja kenda kulima mpunga Bara akarudi akaona alizeti inazalishwa akaanza kuzalisha, ndiyo matokeo ni hayo ni vipi naona mambo yanakuja juu tu haya.

Kwa sababu leo tunaambiwa kwamba mashamba yamekuwa kidogo kwa ajili ya kulima mpunga, na ndio ukawa kidogo mpunga, na ndio muhogo ukawa kidogo na ndizi zikawa kidogo.

Sasa leo tunaambiwa kuwa kinakuja kilimo cha alizeti kita- *replace* nini hichi kwa utafiti wetu. Kinakwenda ku- *replace* muhogo, kinakwenda ku- *replace* mpunga kinakwenda ku- *replace* ndizi. Hebu tuambieni umeshakamilika huo utafiti, hata na sisi tuingie hamu? Mimi nataka kiinua mgongo changu Mheshimiwa niende

nikapande alizeti, hasa kwa hivi nilivyoambiwa. Lakini je, kweli ni kilimo kweli cha kuwa nikitegemee.

Mhe. Naibu Spika, Bonde la Makombeni liko pande mbili narudi pale pale, hicho kisima kilichochimbwa ukienda wenyewe walio na bonde hili wanakwambia maji hivi sasa yameshakuwa kidogo hayawezi kutosheleza bonde lile lote.

Hiyo sehemu moja tu hivi sasa basi imeshakuwa mashaka, na kuna sehemu nyengine. Sasa Programu hii ya toka 2011/2015 pengine ndio tutapata angalau kuvuna vipunga kidogo. Sasa hivi kweli miaka yote mitano hapo tunakwenda, halafu tunasema kwamba tunataka kufanya Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri serikali sasa iko haja ya kufanya *review* ya Programu zake zote, kuangalia kweli. Hebu tufanyieni tu *subsidization,* tuleteeni mchele iko huko, sisi tunataka mchele hatutaki kilimo cha umwagiliaji au wananchi wanataka maji ya kumwagilia? Wananchi wanataka mchele ulio rahisi! Sasa hivi hizi fedha mziweka huku bure tununulieni mchele mtufanyie *subsidization, finish!* Tunahitaji mchele hatuhitaji kumwagilia maji sisi.

Sasa kumwagilia maji inaonesha tumeshindwa, miaka mitano awamu inamalizika, bonde gani lililo- ***materialize*** tukasema sisi tunazalisha mpunga hapa. Ukienda huko utaambiwa *JICA* wanakuja, *KOICA* wanakuja, washaika, wameshafanya kila wanalofanya hamna mpunga! Mheshimiwa tuambiane ukweli. Sisi tunataka mchele tu bwana, sasa kama mchele uko wanunue mchele watuletee *subsidization,* zile pesa ambazo wana-*inject* kwenye *irrigation* wawaambie wazungu watusaidie tu, na nashangaa mara hii hapa ile Programu ya Wajapani waliokuwa wakitusaidia kufanya angalau pembejeo za kilimo sijaiona kutajwa humu.

Kwa sababu Wajapani walikuwa wanaleta mchele kwa ajili ya kusaidia uuzwe mchele ule tupate pembejeo tukalime, sijui wameona hakuna *Progress* yoyote inayoondelea hawakuleta, hebu Mheshimiwa Kaimu ukija uje utwambie mara hii hatukupata mchele kutoka Serikali ya Japan. Maana mwaka jana ulikuja sijui ukagaiwa Tanzania Bara ukagaiwa wapi, mara hii vipi hatukupata ule tukapata angalau vijisenti, tunaweka pesa huko kwenye pembejeo za kilimo.

Mhe. Naibu Spika, hetu twambie hapa mara hii vipi ule mchele kutoka Japan, mara hii haukupatikana au ulipatikana tukapata kiasi gani sisi SMZ na SMT wamepata kiasi gani. Kwa sababu mimi najua Programu hii inasaidia serikali katika kupata fedha za kununulia pembejeo za kilimo pamoja na uwekaji wa chakula cha lishe kwenye maghala.

Sasa chakula na lishe kwenye *irrigation* hamna, utakwenda huko mpango huu baada ya kuzalisha chakula unalizasha miti ndio maana yake. Ukienda utaambiwa kuwa mti huu chakula na lishe unakwenda kuoneshwa ile miti ya njiani wanaita mikeshia inahusika na nini Mheshimiwa.

Sasa hebu ibadilisheni hii Programu, sisi tunataka mchele hatutaki kilimo cha umwagiliaji, tunataka mchele tule tu hapa, tufanye *subsidization* basi!

Mhe. Naibu Spika, niende tena kidogo katika Idara hii ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Hapa kuna utaratibu wa kuyatambua na kutayarisha mpango wa usimamizi wa mashamba ya serikali pamoja na eka tatu. Hivi serikali inajua nini kuhusu eka tatu, hivi sasa zipo? Kwa sababu naona sisi tumeshanunua zote tumeshajenga wanataka kuratibu nini wao hivi sasa. Labda utaratibu wao ni vipi, mimi kama baba kafa kuna utaratibu wowote ziko hizo eka ziko vipi na hayo mashamba yakoje.

Siku moja nilikwenda Makurunge kule, nikaambiwa kuna shamba la serikali la mikarafuu. Mashamba haya hivi sasa yanamilikiwa na nani na sijui hizi pesa zikipatikana huwa zinaingia katika mfuko gani wa kukodishwa haya mashamba ya mikarafuu.

Jengine Mheshimiwa Kizimbani, wametwambia kwamba wana ziara nyingi sana, wamefaidika wamekwenda ziara sijui Norway na sehemu nyengine. Hapa ilipokuwepo bajeti ya Mhe. Makamu wa Rais wa Kwanza na Makamu wa Pili na Mhe. Rais mwenyewe huwa tunauliza hizi ziara zao wanapokwenda huko faida yake nini, wametuletea nini?

Hebu twambieni na hizi ziara zenu Chuo cha Kilimo mmebadilisha ziara mmekwenda sijui Chuo cha Sokoine, sijui mmekwenda wapi, mmefaidika nini katika masuala haya mumesoma, mmejifunza, mumefanya utafiti, utafiti wake umezaa nini katika mashamba yetu ya kilimo yaliyopo Kizimbani? Au mmekwenda Norway baada kurudi hapa ndio mmesharudi kama alivyokwenda Mhe. Abdi Mosi kenda China kaona nyumba kubwa, kaona watu wanakula mawe, karudi hapa yamemalizika! (*Makofi*)

Jengine kuna huu mpango wa Programu hii ya Miundombinu ya masoko, uongezaji wa thamani na huduma za kifedha vijijini.

Mhe. Naibu Spika hapa mimi nina wasi wasi sana. Programu hii wanavyotueleza kwamba wao waliomba milioni sitini kutoka serikalini. Bahati nzuri serikali imejitahidi imetia milioni kumi *alhamdulillah Rabil- alamina*, sawa. Lakini wafadhili baada ya bilioni mbili wametia bilioni nne, ndio programu inavyosema

hapa 2014/15. Kwa sababu mimi mawazo yangu sijakaa na pesa sana, lakini bilioni nne Mhe. Naibu Spika, kwa mimi zingepata *tangible thing,* nikaiona hii hapa kwamba barabara hii imetiwa kifusi.

Nimeangalia tabu kubwa hili kidogo kupekura pekura japo sijalijua uzuri pengine labda Mhe. Kaimu Waziri utakapokuja nieleze kidogo. Sijaona kitu kwamba zile bilioni nne zimezalisha nini katika programu hii. Hebu utakapokuja Kaimu, hebu kidogo uje unieleze kidogo hapa pamefanyika nini?

Pia katika Programu zake imesema kwamba kuchangia kwa asilimia sabini na tano ununuzi wa mashine ndogo ndogo za usarifu wa mazao. Matokeo yake wanasema vikundi vitatu vilikubalika kunufaika na mpango huu baada ya kukidhi vigezo vilivyotakiwa. Lakini hadi sasa vimeshindwa kukusanya mchango wao wa asilimia ishirini na tano unaotakiwa kutolewa kabla ya kununuliwa mashine.

Sasa hawa baada ya utafiti Mhe. Naibu Spika, walikubalika vipi kwamba vigezo vyao vimekamilika wakati wao asilimia ishirini na tano ya kutoa wao hawajazipata.

Sasa ikiwa wamenunuliwa mashine zimekaa tu hazifanyi kazi yoyote, hizi fedha bado zinakaa tu hazifanyi shughuli yoyote pale bado tunaendelea kuwasuburi hawa watu tu. Hizi pesa zina masharti fulani, kwani mpaka hawa wananchi watoe? Kwa sababu naona katika ujenzi wa barabara hakuna masharti hayo, kwamba wananchi wanatakiwa wachangie kiasi fulani. Sasa hizi mashine walilazimika wananchi kwamba watoe hii asilimia ishirini na tano ndio wao wapewe hii asilimia sabini na tano iliyobakia, hebu Mheshimiwa Kaimu ukija hapa niambie.

Mhe. Naibu Spika, tunaziweka tu hizi mashine ndani hazifanyi kazi yoyote, kwa sababu hawa watu hawajalipa hizi asilimia ishirini na tano.

Mhe. Kaimu Waziri nisimpe mengi maana yeye yuko Ikulu, hawa wako shamba, yeye haendi shamba sana hayajui mengine.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika hapa leo sote tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2015/16 kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Pia nimpongeze Mhe. Dkt. Sira Ubwa na watendaji wake wote wa wizara hii kwa kazi yao nzuri. Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa juhudi zake kubwa na kwa ripoti yao nzuri ya kamati waliyotusomea hapa leo hii.

Pia nimpongeze muwasilishaji Kaimu Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri sana aliousoma hapa kwa umakini mkubwa kabisa, Mhe. Mohammed Aboud nampongeza sana kwa uwasilishaji mzuri sana.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nianze katika ukurasa wa 4 kifungu namba 2.3.2.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua msimu wa kilimo wa mwaka 2013/14 takwimu zinaonesha kushuka kwa mavuno kwa baadhi ya mazao ikiwemo karafuu ambayo imeshuka kutoka tani 5.2 kwa tani elfu tano mia mbili thamanini mwaka 2013 hadi kufikia tani elfu nne mia moja hamsini na tatu kwa 2014.

Mhe. Naibu Spika, hii ni hali mbaya kweli kweli, kwani hili zao tunalitegemea kama ni zao la Taifa letu.

Mimi niseme kwa nia njema ya serikali, naomba nimuulize Mhe. Waziri mwaka jana katika bajeti yake alisema kama atatoa miche laki tisa arubaini na moja mia moja sabini na sita miche ya karafuu ili wapewe wakulima bure bila ya malipo miche ile. Sasa naomba Mhe. Waziri unambie miche ile iliyotoa serikali bure bila ya malipo karibu laki tisa arubaini na moja sabini na sita kwa wakulima imefikia wapi, na maendeleo yake naomba unambie miche ile inaendeleaje, kwa sababu fedha nyingi serikali inapoteza kuwapa wakulima wetu, lakini je, kazi zao zinakuwa vipi?

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea ukurasa wa 4 kifungu namba 2.3.2. Mhe. Naibu Spika kama kitabu chetu kinavyotwambia mpunga pia kushuka tani elfu thalathini na tatu mia sita hamsini na tano kwa mwaka 2013 hadi kufikia tani ishirini na tisa mia tano sitini na nne 2014. Tukiangalia pia zao hili la muhogo limeshuka kutoka tani laki moja sitini na nne 2013 hadi tani laki moja hamsini na nane 2014. Kuna upungufu karibu wa tani elfu kumi hapa zimeshuka ya muhogo.

Mhe. Naibu Spika, pia nije kwenye ndizi kutoka tani sitini na nane elfu katika mwaka 2013 zimeshika kutoka tani sitini na nane elfu hadi kufikia tani hamsini na saba elfu.

Pia kuna wastani imeshuka karibu tani elfu kumi hapa za ndizi katika mwaka 2014 ambao ni mwaka uliopita.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua haya mazao ni muhimu sana katika maisha yetu, hasa katika kipindi hichi cha mwezi wa Ramadhani, ukiangalia mpunga tunauhitaji sana, tukiangalia muhogo ni zao kubwa ambalo tunakula sana mwezi wa Ramadhani, tukiangalia ndizi ndio halikadhalika.

Sasa ukiangalia takwimu hizi Mhe. Naibu Spika kwa kweli inatia wasi wasi mkubwa.

Pia hapa kuna mambo yameelezwa kama kupungua kwa eneo linalolimwa, maradhi na kutumia mbegu zilizokuwa sio za kisasa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba serikali ina nia njema sana na wananchi wake na inajitahidi kupita kiasi.

Mimi nije kwenye ukurasa wa 10 kifungu namba 2.5 naomba ninukuu hotuba ya kitabu cha Bajeti cha mwaka jana 2014/15;

"Wizara ya Kilimo na Maliasili imeongeza zana za kisasa kwa lengo la kuimarisha ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua. Jumla ya matrekta ishirini mapya yamenunuliwa na kuweza kusaidia kazi za uzalishaji wa mpunga".

Mhe. Naibu Spika, hii ni ishara tosha kwamba serikali yetu inajitahidi sana kama ilivyosema mwaka jana imenunua matrekta ishirini kuwapa wananchi wetu ili waweze kulima. Lakini naomba Mheshimiwa atakapokuja kufanya majumuisho anambie hayo matrekta ishirini yamegaiwa vipi na hali yake yanaendeleaje. Kwa sababu serikali pesa inajitahidi kutoa ili kuwaimarisha wananchi wetu hawa wa kilimo waweze kupata mazao yao kwa urahisi, hasa pembejeo kama hizi za trekta.
Na Mheshimiwa Rais kaenda kununua mwenyewe mwaka jana, na tuliona kwenye vyombo vya habari alikwenda India na akasema kwamba kanunua matrekta ishirini. Kwa hiyo, naomba matrekta yale kujua hali yake iko vipi, na wananchi wanaendelea vipi katika kufaidika na matrekta yale.

Mhe. Naibu Spika, niendelee pia katika wizara hii kuna changamoto nyingi Mheshimiwa. Ukitizama uingizwaji wa fedha ni mdogo kwa wizara hii. Ni sekta muhimu ya kilimo, na ukitizama fedha zinaingizwa kidogo, hasa sekta hii ya kilimo ni kama uti wa mgongo wa nchi hii au kwa maisha ya wananchi.

Pia mimi niwashukuru sana watendaji wa wizara wana bidii kubwa, na wanajitahidi sana katika kufanya kazi zao japokuwa hali ngumu, lakini wanaweza kufanya kazi kwa kujitolea na kwa jitihada kubwa kuleta maendeleo ya kilimo.

Mimi nawapongeza sana watendaji wa wizara hii kwa moyo wao mkubwa, na naomba sana wasivunjike moyo, waendelee na serikali inajua kwa nia yake njema kabisa inajitahidi siku baada siku kuimarisha sekta hii, na hali kama nilivyoeleza inaonekana kwa kweli.

Mhe. Naibu Spika, niendelee tena katika sekta hii kwa kweli imekuwa na wastani mdogo haujaimarika kiasi fulani, kwani kufikia mwezi wa Aprili 2015 kwa kazi za maendeleo ni asilimia sitini. Kwa kweli ni kazi ndogo haijakuwa kubwa kwa mwaka huu. Lakini niseme tu pia jengine na ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Naibu Spika, ruzuku ukitizama pia ni karibu asilimia arubaini na tisa wanapata, na ukitizama chuo hichi ndicho kinawapa mafunzo hawa wakulima wetu na utaalamu wa kisasa ili kuwafahamisha jinsi gani waweze kupata mazao yao.

Sasa ukitizama ruzuku zao chuo hichi kinapata arubaini na tano. Kwa hiyo, naomba sana ruzuku hii Mhe. Naibu Spika, iongezeke kwa ajili ya kuwapa utaalamu wakulima wetu.

Niingie kwenye ukurasa wa 6 kifungu namba 3.3.3. Mimi niseme bidii inaonesha kweli kweli kwa wizara yetu sio masihara, wanafanya kazi na wanajitahidi.

Na nasema hivi kwa malengo na utafiti nilioufanya. Nilitizama kwenye kitabu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/15 ilikadiriwa kukusanya mapato jumla ya shilingi milioni mia nane arubaini na tano, hadi Aprili wizara imekusanya jumla ya shilingi milioni mia nane mia mbili hamsini na mia tatu na sitini, karibu milioni mia nane thamanini na mbili wamekusanya.

Kwa kweli hili ni jambo la kupongezwa, ni sawa wa asilimia mia *point* nane. Kwa hivyo, hili ni jambo la kupongezwa sana kwa wizara. Mimi nasema wana bidii kubwa, sema changamoto kidogo zipo kwa wizara hii lakini naipongeza sana wizara pamoja na serikali kuvuka malengo haya ya wizara kukusanya pesa hizi nyingi. Lakini naamini wanaweza kuendelea kukusanya mapato zaidi ya hayo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee pia niseme wananchi wengi wanashindwa kumiliki chakula hasa kwa sasa. Ukitizama pembejeo hizi kidogo mazao yetu kidogo yameshuka, lakini vyakula vinapanda bei siku baada ya siku. Ukitizama pia

umuhimu wa wataalamu tunao kidogo, kwa kuwashajihisha watu wa kilimo waweze kufanya kazi zao na kulima kwa vizuri.

Kwa hiyo, serikali naomba sana iangalie suala la wataalamu ili iweze kuwasaidia pia katika kilimo cha kisasa.
Mhe. Naibu Spika, wananchi wengi sekta hii ni ajira kwao, ukitizama wananchi wetu ni wanyonge, ukitizama asilimia karibu thamanini au sabini ni wakulima na wanategemea sekta hii.

Hata ukitizama sasa hivi marikiti ukienda jioni watu wanafanya biashara mpaka usiku, kwa sababu hii ni muhimu na inawapa ajira watu wengi na mimi naipongeza serikali kwa kuwaachia kufanya kazi mpaka usiku, kwa sababu ni moja ya ajira, vijana wetu wanaweza kupata ajira na kukidhi maisha yao.

Kwa hivyo, mimi naipongeza sana serikali kwa sekta hii hasa kwa upande huu wa kuuza mazao yao haya ya kila siku, imepelekea wakulima wengi kuongeza matumaini Mhe. Naibu Spika, hasa katika sekta hii ya kilimo.
Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana kama nilivyoeleza mwanzo, serikali iangalie sana changamoto za wizara hii zote ziweze kuondoka, ili wananchi pia wawe na moyo na serikali yao pamoja na kuweka matumaini makubwa katika sekta hii ya kilimo. Sekta hii ni muhimu sana, na mimi nasema ni kama uti wa mgongo kweli. Kwa sababu vyakula vingi tunavyotegemea sisi kula vinatoka hapa hapa Zanzibar, tukisema kwamba vyakula vyote tuagize kutoka nje, hiyo gharama itakuwa ni kubwa na tutashindwa kuvinunua vyakula vile. Kwa hiyo, mimi naomba sana sekta hii Mhe. Naibu Spika, tuiangalie uzuri.

Jengine naomba sana Serikali iangalie kutafuta *investors;* kuwashajihisha ku-*invest* kwenye suala la kilimo. Hivyo wasiendelee ku-*invest* mambo mengine, lakini ninawaomba sana Serikali iwape fursa kubwa wawekeze kwenye sekta hii ya kilimo.

Kama tunavyojua sekta hii inatakiwa fedha nyingi uwe nazo, lakini kama kutakuwa na wawekezaji wana fedha nyingi, ninaamini sekta hii itakuwa na itaweza kuwapatia ajira wananchi wetu, ili kuwasaidia na sisi wenyewe kutusaidia kupata vyakula vilivyokuwa vizuri na bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwenye ukurasa wa 7. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa juhudi zake kubwa inayofanya kwa nia njema kwa nchi yake na kwa wananchi wake.

Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu katika bonde la umwagiliaji maji liliopo Makombeni ambapo ekari 22.5 zimelimwa na kunufaisha wakulima karibu 120.

Hili ni jambo la kupongezwa kwa Serikali, yaani wakulima 120 wameweza kufaidika kwa juhudi za Serikali kuchukua kuweka miundombinu hii vizuri. Hivyo ninaipongeza Serikali kwa juhudi, ninajua siku moja baada ya siku tunabadilika na tunaweza kupiga hatua kwa haraka sana.

Pia niipongeze Serikali kwa juhudi zake kubwa kuhusu ujenzi wa barabara za maeneo ya kilimo, kuweka miundombinu vizuri kwa Unguja na Pemba umeanza na imewekewa kifusi cha kilomita 20.

Mhe. Naibu Spika, hili jambo ni zuri kabisa, kuwa miundombinu ya barabara kuweza Serikali kuona umuhimu wa kuweza kupata wakulima wetu kwenda kuchukua mazao yao na kurudi kwa gari vizuri kwa kuweka kifusi kwa kilomita 20. Hili jambo zuri na mimi ninaipongeza sana Serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze tena Serikali kwenye ukurasa wa 8 kwamba Wizara imefanikiwa kununua mtambo wa kukamua mafuta ya alizeti yenye uwezo wa kukamua tani 6.5 kwa kila siku.

Hili ni jambo jema kabisa, na nimesema mwanzo Serikali yetu kila siku inapiga hatua kwa nguvu sana. Mimi ninasema tukiangalia hali yetu kidogo ni maskini lakini kwa kutegemea wafadhili wanaotusaidia na wahisani mbali mbali, na nimpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar kwa juhudi zake kutafuta wahisani kuweza kutusaidia.

Hili ni jambo zuri kwa mtambo huu uliowekwa wa kukamua mafuta ya alizeti kwa siku tani 6.5, siyo kiasi kidogo. Mimi ninapongeza sana kwa juhudi zake hizo nzuri.

Vile vile jumla ya lita 422 za alizeti zimekamuliwa. Kwa hivyo mimi ninaona ni jambo jema kabisa na ni mfano mzuri.

Mimi nilisema mafuta haya Mhe. Naibu Spika, mafuta ni mazuri. Sasa ukiangalia mafuta mengine sasa hivi tunayokula haya ya kawaida, ukitazama yapo mengi sasa hivi lakini mafuta haya ukienda ukiyanunua kama yanatoka nje, utakuta lita nne unanunua kwa elfu hamsini na mafuta yale ukitazama mazuri kwa binadamu kwa ufupi. Kwa sababu hayamfanyii binadamu madhara ya maradhi yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata bahati ya kwenda India kuna kipindi, katika kwenda kule India nikapima *pressure*, nikapima sukari, nikapima na vitu vyengine. Lakini bahati mimi nikamwambia daktari mimi sili sukari, hula sukari kwa kiasi fulani ninajiangalia kwa ufupi, akaniambia unakula mafuta, nikamwambia mafuta

ninakula mengi na kama kawaida wala sijali kula mafuta. Sasa akaniambia sawa pima sukari, *pressure*. Sawa ipo vizuri, lakini mafuta yanasababisha kuwa na ugonjwa wa sukari, nikamwambia kwa nini. Kwa sababu anasema ukila mafuta mengi na ukiwa na *cholesterol* nyingi kwenye mwili, ile *cholesterol* ndiyo inayosababisha wewe kuwa na sukari hata kama huli sukari, unaweza kuwa unakula sukari nyingi lakini ugonjwa wa sukari hupati. Lakini unaweza ukala mafuta mengi ukapata ugonjwa wa sukari pia.

Kwa hivyo, ile *cholesterol* yako ikipanda kwenye mwili, ugonjwa wa sukari utaupata. Hivyo mimi ninaipongeza Serikali kwa juhudi yake hii ya mafuta haya ya alizeti kuweza kutumika hapa, na watu kupikia na mengine kuweza kusafirisha nje; maana mafuta ni mazuri sana kwa maisha ya binadamu. (*Makofi*).
Mhe. Naibu Spika, mwisho nimalizie katika huu mradi wa ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao Kizimbani.

Kituo hichi Mhe. Naibu Spika, kipo kwenye jimbo langu na ninakijua na kituo hichi ni muhimu sana. Ninasema hivyo kwa wakulima wetu na wadau wengine kama taasisi ya viwango.

Mhe. Naibu Spika, na ujenzi haujamalizika mpaka sasa hivi tunavyojua, ujenzi huu unasuasua muda mrefu, unakwenda unasimama. Sasa mimi sijui tatizo linakuwa nini, lakini kipo karibu na jimbo langu kama nilivyosema nimeshatembelea mara mbili au tatu.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa kituo hichi hatua nzuri sana imefikia, na niipongeze sana Serikali na Wizara kwa hatua waliyofikia ni nzuri sana.

Vile vile mashine na vifaa vyengine vimekamilika. Vifaa vilivyokusudiwa vimekamilika lakini vipo vifaa vimekaa sasa hivi bure havina kazi, na lile jengo halishi lakini vifaa vimenunuliwa na vimekaa bure. Kwa hivyo ninaomba sana hili jengo Mhe. Waziri uliangalie sana likamilike ili hivi vifaa vipate kufanya kazi, ili ile pesa ya Serikali isiweze kupotea bila ya sababu.

Pia Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana Kamati kuona kwenye ripoti yao kwa kusema kuwa Wizara ifanye marekebisho ya matumizi katika kazi za maendeleo kwenye kupunguza fedha kwa baadhi ya miradi, ili zile fedha ziweze kumaliza kuweza kuweka ujenzi wa kituo cha usarifu.

Mimi ninamuunga mkono Mwenyekiti wa Kamati hii, wazo lake na wajumbe wote walioko kwenye Kamati yake na ripoti yao tumeiona wametusomea leo, kuweza kutenga milioni mia nne ili kumalizia hichi kitu kimalizike ili kiweze kufanya kazi,

ili pesa yote iliyoingizwa pale ya vifaa na jengo iweze kumalizika na iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, milioni mia nne siyo nyingi kwa Wizara, ninaamini wanaweza kukata sehemu pesa hizi ili tuweze kumaliza kituo hichi ambacho kitawasaidia wakulima wetu na mambo yetu mengi hasa ya kutizama, kupima na mengineyo.

Kwa hivyo naomba sana hili wazo la Kamati Mhe. Waziri aliangalie na aweze kuwasaidia ili tuweze kufanikisha hichi kituo kimalizike kwa salama na amani kama Serikali ilivyokuwa inataka, lengo lake liwe vile vile basi naomba sana kimalizike.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia bajeti hii wala sina mashaka nayo.

Mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu, tuna imani kubwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutuletea maendeleo, hakuna mwengine mkombozi wetu, ni Serikali hii tu ya wanyonge basi mimi ninaamini kabisa na ninaunga mkono kwa asilimia mia, sina mashaka.

Mhe. Naibu Spika ahsante. (*Makofi*).

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsane Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Sasa nafasi tunampa Mhe. Salim Abdalla Hamad baadaye Mhe. Ashura Sharif na muda ukibakia tutampa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwemo katika jengo hili Tukufu na kutoa michango yetu kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa bajeti yake ya mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ni moja kati ya Wizara za Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, na ni Wizara ambayo wananchi tunategemea iweze kufanya kazi ambayo itatuwezesha kupata chakula bora cha kutosha, kusafirisha mazao mengine nje ya nchi na kuipatia Zanzibar fedha za kigeni. Hiyo ni maana ya kukuza uchumi pamoja na kuwa na uhifadhi endelevu wa maliasili zetu ambazo tunaendelea kuhujumiwa kila uchao.

Ni Wizara iliyo na majukumu makubwa yanayowagusa jamii moja kwa moja kwa maisha yao. Ninashukuru kwa kusikia kuwa ni Wizara yenye wataalamu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kama Wizara hii haikuwezeshwa na kufanya kazi zake ipasavyo, hapana budi itatupelekea katika mahala ambapo nchi hii itazidi kuingia katika umaskini kwa kulazimika kuagizia vyakula na mambo mengine kutoka nje ya nchi, ambapo kama Wizara ingelikuwa ina umakini wa kupata pesa za kutosha, ingeliweza kuotesha hapa hapa na hilo tatizo kuondoka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba kuchangia moja kwa moja kwa kuanza kwenye jadweli la kwanza liliopo kwenye ukurasa wa 43.

Jadweli hili au kiambatanisho hichi namba 1 kinaeleza kuhusu takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa tani kwa mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna uzalishaji wa aina mbili. Hapa kuna uzalishaji wa mazao ambayo yaliongezeka kutoka mwaka 2013 na 2014 ukilinganisha na yaliyoongezeka, na kuna yale ambayo yalipungua na mazao haya yote yanaoteshwa katika ardhi hii hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano tukiangalia mahindi, mtama, viazi vitamu, mboga mboga na mananasi, haya yote uzalishaji wake ukiangalia wa 2013 na mwaka 2014 umeongezeka kwa kiasi ilivyoonekana katika kitabu.
Haya mazao mengine kwa mfano mpunga ambao ndiyo chakula chetu kikuu, ndizi vile vile ni chakula chetu kikuu, muhogo ndiyo kabisa kwa sisi maskini, viazi vikuu pamoja na njugu nyasa hivi ni vyakula ambavyo ni muhimu, ndivyo tunavyotegemea kwa maisha yetu na vinapungua.

Ukiangalia uzalishaji wa mwaka 2013 na 2014, hapa pamekuwa na upungufu kinyume na yale mazao niliyoyaeleza mwanzo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 4 unaeleza kuwa kwa kilimo hichi kilichopungua wanasema sababu imetokana na kupungua kwa eneo lililolimwa, maradhi na wakulima kutumia mbegu za asili.

Mimi naomba kujua Wizara au Serikali imejitahidi kutafuta pembejeo, imetengeneza matrekta 31 katika matengenezo ya kawaida, watu wanaongezeka. Moja kwa moja ni kusema na wakulima wanaongezeka, ulikuwa na sababu gani kuwa na upungufu wa eneo lililolimwa badala ya kuongezeka.

Mimi nilifikiria kwa kila mwaka ilivyokuwa tunaongezeka na si kwa uuzaji tu lakini pia kwa watu walioingia, na wanajishughulisha sana na shughuli za kilimo, kwa hivyo nilidhania eneo kubwa zaidi lilikuwa lilimwe na tupate chakula cha kutosha, lakini kwa nini ikawa eneo hilo limepungua. Naomba nipewe maelezo.

Halafu maradhi na wakulima kutumia mbegu za asili. Mimi ninajua Wizara inavyopambana sana na maradhi ya mazao kama walivyoeleza katika kitabu. Ningeomba kujua kwa nini katika kilimo cha mboga mboga na mambo mengine yanayohusiana na hayo hatukuona kuwa kulikuwa na matatizo ya maradhi, lakini hapa kuna matatizo ya maradhi, na kwa vile wanachukua juhudi kila siku ya kupambana na maradhi, ni maradhi gani hayo na kiasi gani cha kipando kilichoharibika mpaka ikawa uvunaji ni mdogo.

Mwisho katoa sababu kwa kutumia mbegu za asili. Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyojua pamoja na kuwa kuna utaalamu unaendelea, na mimi ninaheshimu sana, lakini hakuna kitu cha kujali kama mbegu ya asili, isipokuwa sisi wajibu wetu ni kuifanyia *improvement,* kwa kufanya hiyo *cross breeding* au utaalamu wowote wanaojua wataalamu.

Kwa sababu mbegu ya asili imeshakuwa inaishi, kwa hivyo inapungukiwa hata na maradhi, inakuwa inaishi, inakuwa ni ya asili na inachukua muda mrefu kwa sababu inakuwa na vigezo vya kutosha kutokana na maumbile na mazingira kuweza kuendelea kuishi na kuzaana kila siku zikienda mbele.

Kwa hivyo wajibu wetu ni kuichukua mbegu hii na kutafuta mbegu inayofanana na hii ambayo labda ina sifa bora zaidi, tukafanye hayo mambo yetu ya utaalamu ili tukapata mbegu bora ambayo itatusaidia katika kupata mazao mengi kwenye sehemu ndogo ya kilimo na haya ndiyo maendeleo.

Hapo hapo ninauliza swali. Mpunga umepungua lakini hapa tulikuwa na mbegu ile ya *NERICA* ilisifiwa inaota kila mahala, inaota vizuri, inazaa vizuri, inaondoa umaskini na ipo haijahama bado.

Kwa hivyo ni sababu zipi zilifanya mpunga huu ukapungua, na kupungua kwa mpunga kwa Zanzibar ni kuagizia kwa mchele kutoka nchi za nje ni kuitia hasara Serikali kwa jambo ambalo sisi wenyewe tunaweza kupambana nalo. Naomba sababu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa yale mazao ambayo yameongezeka, ninashukuru sana na sababu iliyotolewa ni kuwa hali hii imetokana na wakulima walio wengi kulima mazao ya mboga na matunda ambayo ni ya muda mfupi, na tija ya haraka pamoja na huduma zinazotolewa na sekta binafsi zikiwa taasisi za uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda, maua na kadhalika.

Ninashukuru juhudi kama hii ya wataalamu hawa, kwa nini pia isipewe katika chakula hichi ambacho sisi wenyewe tunategemea kwa maisha ya kula, si biashara tu ikawa tukakubali huku kuanguka.

Kwa hivyo, la mwisho la hapa ningeliomba nijue kuwa Wizara ina mpango gani wa kuona kuwa tatizo hili linaondoka ili mwaka 2015/2016 tuone kuwa mashamba mengi yanalimwa, mbegu nzuri inatumika ambayo ni endelevu na sisi tunatokana na balaa hili la njaa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo na kwa ruhusa yako twende na kilimo cha maweni. Taarifa ya kilimo cha maweni ipo ukurasa wa 5 wa kitabu hichi cha bajeti.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hichi kinaeleza kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikiongeza nguvu katika kuendeleza kilimo cha maweni ikiwemo kilimo cha ndimu, mbaazi, mtama, uwele na viazi vikuu ikiwa ni mazao ya chakula na biashara, jambo ambalo limewapa wakulima tija haraka na kipato kizuri. Hili mimi ninalipongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, kilimo cha maweni ni zaidi ya hichi kilichoelezwa. Sasa kwa nini Wizara ikajaribu kuendeleza kwa utaalamu, aina hii tu ya kilimo wakati vipo vyengine vinaota, tena vinaota sana na ni vyenye bei nzuri. Kwa mfano, mipapai maweni inaota kwa wingi, na papai ni tunda muhimu sana kwa binadamu kwa aliyelijua faida yake.

Papai ni dawa hasa, hata kwa kidonda sugu ndiyo linalotumika ikiwa madawa yameshindikana. Papai lina kitu kinaitwa *terpine* ni *protein* iliyo muhimu sana mwilini, hapa haikuingizwa wakati hao tunaosema watalii wetu wanapenda sana kutumia matunda haya ya mapapai. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, wakati ndimu zinaota maweni na tukiangalia michungwa na milimau ni aina ya miti ambayo ni *close related* na hii midimu. Je, kwa nini miti hii ambayo inakaribiana sana, na naamini inaweza kuota huko maweni, kwa nini haikuingizwa?

Kwa hivyo, naomba hilo nipate jibu, nazungumza hivyo kwa sababu kila tukipanda sana, tukitumia ardhi yetu ya maweni, tukipanda matunda aina kwa aina, basi ndivyo nchi yetu itakavyoneemeka kichakula. Tutapata chakula cha aina mbali mbali, ndivyo tutakavyopata lishe bora, na ndivyo tutakavyoepukana na maradhi.

Kwa hivyo, kwanza kwa nini miti mingine haikuingizwa wakati kuingizwa kwao ni muhimu sana.

La pili nahimiza kuwa zaidi ya haya na mengine yashughulikiwe ili nchi hii isiwe na hata sehemu moja ya ardhi iliyobakia ovyo, hasa kutokana na kuwa hii nchi ni *over populated* na sehemu ya kilimo ni ndogo sana.

Halafu hapa hapa niende kwenye maliasili. Maliasili Mhe. Naibu Spika, ni muhimu sana katika nchi yetu. Tumeingiwa na maendeleo katika dunia, mazingira yanaharibika, kunaongezeka hewa ukaa, ni miti pekee ndio inayoweza kuwa dawa ya kuihami nchi yetu na ongezeko la hewa hiyo ya hatari ambayo sisi hatuna mamlaka ya kuizuia.

Tunahitaji nchi yetu iwe na unyevunyevu, ili miti iweze kuota, tunahitaji tupate mvua kwa miongo, tusipate mvua ya *monsoon* tu, inayosababisha kuleta mvua vile vile ni miti.

Mhe. Naibu Spika, sasa huu mtindo wa umaskini tuliokuwa nao wa kukata miti ovyo na bila ya kuipanda mengine, basi kunasababisha kufukarisha nchi hii kiafya na vile vile kimapato, kwa sababu kunasababisha ukame katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba kuzungumza kuhusu Jimbo langu la Mtambwe. Yuko Mhe. Mjumbe mmoja kasema kwamba Zanzibar sasa kuna msitu, lakini Zanzibar yako majimbo yana miti mingi sana ambayo inasaidia, inasaidia kuhifadhi maji na mambo mengine. Na kila siku napiga kelele na mimi naamini kama Wizara ya Kilimo haitaki, kwa hivyo hujuma haiwezi kufanywa. Naiuliza wizara, ni jambo gani hasa lililosababisha mpaka watu wote wakaacha kwenda katika maeneo mengine, wakakimbilia katika Jimbo la Mtambwe kwa kukata miti ovyo?

Watu wote wenye matanuri yao wanakata miti kule mibichi, wanaojenga wanakata kule miti mibichi, na pale Bahanasa pana Bwanashamba kazi yake ni kutoa kibali na kukusanya pesa, lakini miti au msitu katika Jimbo la Mtambwe unateketea.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Naibu Spika, sitokuwa tayari kuipitisha bajeti hii na hasa kwa kifungu hiki cha maliasili, mpaka Mhe. Waziri anipe jibu la kutosha, kwa nini hakuna uhamasishaji wa kutosha wa kupanda miti katika jimbo langu, lakini wanaachiwa watu wanakata miti ovyo, kiasi ambacho lile jimbo wanalifanya jangwa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, tumetembea hasa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba Wilaya ya Micheweni, tumeona namna Kampuni zinazohusika na ujenzi wa barabara zinavyoiharibu ardhi, wanachimba mahandaki.

Mhe. Naibu Spika, sisi wanatwambia uchimbaji usizidi mita tatu, lakini hata mita tisa mahandaki mabaya tunaona, watu kwa sababu ya umaskini wao wanachimba mawe wanafukarisha kila kitu.

Hebu tuone hii wizara inayohusika na maliasili isiyorejesheka, inafanya mpango gani kwa kushirikiana na wizara nyengine kuona kuwa hakuna ulazima wa kuharibu mazingira kiasi kile na binadamu wale waweze kujiendeshea maisha yao. Vyenginevyo huko tunakokwenda mwisho itakuwa ni hadithi tu, lakini tunakwenda pahala pabaya sana, na mimi silaumu ni kwa sababu watu walifanya hivyo kutokana na umaskini, ni kazi ambayo hawaipendi.

Kwa hivyo, wizara hii itajihusisha vipi na wizara nyengine zinazohusika na maendeleo ya kijamii, ili kuona kwamba watu wale hawaachiwi kuharibu ovyo mazingira kiasi kile kwa sababu ya umaskini wao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nimeona katika hiki kitabu ukurasa wa 8 kuwa, wizara imefanikiwa kununua mtambo wa kukamulia mafuta ya alizeti, wenye uwezo wa kukamua tani 6.5, sawa na kilo 6,500 za alizeti kwa siku.

Nalipongeza hilo, lakini napongeza sana kuona kwamba angalau kama ndivyo mnavyozungumza tumepata mtambo kabla ya kuwa na uzalishaji wa kutosha. Lakini katika maelezo ni kuwa jumla ya lita 422 ya mafuta ya alizeti yamekamuliwa na kilo 863 za mashudu zimepatikana kutokana na alizeti iliyozalishwa.

Naomba kujua ni kiasi gani cha alizeti iliyozalishwa, ni kiasi gani imekamuliwa na kiasi gani bado, kwa sababu haikuelezwa humu ni kiasi gani imezalishwa.

Halafu Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wizara kwa makusudi kwa mwaka huu ina mpango wa kununua mbegu za alizeti na mbegu hizi zitapandwa katika eka 3,000. Eka 1,500 mabondeni na eka 1,500 maeneo ya juu kwa Unguja na Pemba. Swali kwa nini wakati tuna mtambo huu wa kukamulia unaoweza kukamua tani sita na nusu kwa siku, tuamue kupanda eka 3, 000 tu, wakati kwa mujibu wa hiki kitabu kinavyoeleza ni kuwa kumbe alizeti inaota juu na mabondeni.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningetarajia baada ya huo mpunga kama walivyoeleza wenyewe kuvunwa, tungepanda alizeti kwa wingi ili utakapokuja msimu mwengine wa kupanda mpunga ikawa kiwanda kinafanya kazi na tunazalisha. Tukizalisha mafuta ya alizeti kwa wingi, tutapunguza kununua kutoka nje, hivyo ni ku-*save* fedha zetu na kuleta maendeleo. Naomba kupata maelezo kuhusu mtambo huu na uzalishaji wake kama nilivyoeleza.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea tuna Idara ya Kilimo na hii ni taarifa iliyopo kwenye ukurasa wa 16.

Mhe. Naibu Spika, katika taarifa hii ya Idara ya Kilimo. Hii idara ni moja katika idara muhimu sana kwenye wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Na idara hii ina majukumu makubwa, ikiwa ni pamoja na kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Hiyo ni kazi kubwa sana, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalamu ni muhimu kwa kupata kilimo endelevu chenye manufaa, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za aina ya kilimo, ni kazi inayohitaji fedha nyingi kwa wakulima. Pamoja na utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao yanayosafirishwa na kuingizwa nchini. Ni idara yenye majukumu makubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende kwenye ukurasa huo wa 15 kuna maelezo hapa yanayosema kwamba;

"Kuzalisha tani 350 kutoka kwa wakulima na kununua tani 150 za mbegu za mpunga kutoka Tanzania Bara na kuzalisha tani 5 za mbegu za mahindi, tani 2 za mtama na tani 8 za jamii ya kunde katika kituo cha uzalishaji mbegu Bambi na mashamba ya JKU".

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nataka kujua hizi tani 350 zilizotiwa hapa ni aina ya mbegu gani na gani, kwa sababu haikufafanuliwa. Halafu inasema kununua tani 150 ya mbegu ya mpunga. Tani 150 ni mpunga mwingi sana, na mpunga huo wote unanunuliwa kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, ninavyojua mimi achilia mbali kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Hata ndani ya hii hii Zanzibar sio kila sehemu ya ardhi inafaa kwa aina ya mpunga, kwa sababu zinatofautiana, na kwa hivyo lazima mbegu zitofautiane kutokana na uhalisia wa ile sehemu ilivyo. Kwa hivyo, sisi tunanunua tani 150 hizi ni sawa sawa na kilo 150,000; ni mpunga mwingi sana huu. I

li tusije tukaharibikiwa kwa kuuchukua mpunga kutoka Bara kwa sababu unaota vizuri tukauleta hapa tukaulima, watu maskini ya Mungu wakatumia nguvu zao, pesa zao kwa shida sana na kuharakisha miongo ili wafanikiwe, ikajakuwa tukapanda mpunga huu ikawa ni hasara.

Mhe. Naibu Spika, mimi najua majumbani hakuna mbegu ya kutosha kutokana na umaskini mpunga wote tumeshaula. Naamini wakulima wanasubiri mpunga huu kwa hamu, lakini hii mbegu imefanyiwa utafiti gani? Isijekuwa balaa katika nchi hii, ikawa ni kuwaweka wakulima katika hali ambayo haitambuliki. Isije ikatokea kama *nerica*, mara tunaambiwa unataka maji mengi, mara sijui hivi, mashaka matupu!

Nataka nijue kama hakujafanywa utafiti, kwa hivyo wakati upo ufanywe, tusije kuangamiza wakulima wetu. Ule msaada wa maafa wa kupeleka shilingi 20,000 kwa kila wanaofikwa na maafa hausaidii kitu. Mtu ni kupanda akavuna akapata chakula cha kula.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika,

**Mhe. Naibu Spika:** Bado dakika tano.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mheshimiwa niachie nachangia. Tokea juzi sijachangia.

**Mhe. Naibu Spika:** Hiyo dakika tano unatimiza nusu saa, dakika 30.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Haya. Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa kumeelezwa kuwa kuwaelimisha wakulima 1,500 na wakulima hawa wataelimishwa juu ya mbinu za kilimo bora kwa kupitia mabwana na mabibi shamba, skuli za wakulima na Jumuiya zao.

Wazanzibari wengi Mhe. Naibu Spika, ni wakulima. Kwa nini kipaumbele kikachukuliwa kwa watu hawa 1,500 tu na kati ya hawa ni wangapi watatoka Unguja na wangapi watatoka Pemba, sio kwa ubaguzi lakini ni kwa kutaka kujua ni namna gani taaluma hii inatolewa.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile bado dakika tano, naomba nizungumzie kuhusu tafiti za mbegu zilizofanywa.

Wameandika hapa Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma ni kuwa, kuanzisha na kuendeleza tafiti za mbegu na mbinu mpya za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara; ikiwemo nazi, mpunga, mazao ya mizizi, migomba, mboga na matunda.

Mhe. Naibu Spika, tafiti hizi ni mpaka lini? Hawa watafiti na skuli yao wako miaka mingi sana, haya malimo yanaendelea kulimwa mpaka leo, maana yake ndio kwanza kuanzisha. Mimi nahisi kwa sentensi hii imetiwa tu kujaza kitabu, lakini haiendi kabisa na wakati, naomba maelezo.

La mwisho kwa sababu ya wakati, sio kwa sababu ya kuwa sina la kuzungumza kwa leo. Naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Misitu na Mali Zisizorejesheka katika ukurasa wa 22. Mhe. Naibu Spika, hapa tumeambiwa kwamba kuna miche ya mikarafuu 2,076397 (317,530 Unguja na Pemba 374,842). Kuna miche ya misitu 1,089,140 (917,140 kwa Unguja na 172,000 kwa Pemba), na kuna miche ya

matunda na viungo 294,885 (230,585 kwa Unguja na 64,500 kwa Pemba). Miche hii kwa mujibu wa taarifa imeoteshwa katika vitalu vya serikali, na miche hii tunajua ni kwa ajili ya wakulima.

Mhe. Naibu Spika, naomba kusema kuwa mikarafuu kuna aina na aina. Kuna *species* yenye mashada yake makubwa, kuna *species* karafuu mbili mbili, na kuna *species* karafuu zake sio nzuri.

Kwa hivyo, wakisema wameotesha mikarafuu yote hii, je, wamefanya utafiti kuwa hii ndio mbegu bora, au wanaotesha tu matende halafu wanagawa, huu utafiti kule wanaufanya? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu palipo na wataalamu hapana tena maana ya kufanya tuharibikiwe halafu ndio tukafanye utafiti. Hii miti yote waliyoifanya na kuigawa kwa wananchi, wameifanyia utafiti kuwa ndio mbegu bora, na ikiwa si hivyo kwa hivyo tunakwenda tu na maandishi katika kitabu, kama hatutakuwa hadhir na wataalamu wetu wakafanyakazi ipasavyo, basi tutabakia hivi hivi kila siku, kuvuna kidogo na kulima sana.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, sitounga mkono mpaka nielezwe vya kutosha yale mambo yote niliyotaka ufafanuzi.

Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu na kuniongeza dakika.

**Mhe. Ashura Sharif Hamad:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia uhai, lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo kwetu humu, ili kutekeleza majukumu yetu. Lakini haya yote ni kwa maslahi ya wananchi wa Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama na wewe sikukushukuru kama usingenitaja nisingepata fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako hili Tukufu. Kwa hivyo, nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, pia niichukue tena fursa hii kumshukuru Mhe. Kaimu Waziri jinsi alivyoiwasilisha ripoti hii au kitabu hiki cha bajeti mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu yake kwa matayarisho ya kitabu hiki.

Mhe. Naibu Spika, nianze kusema kwamba mwaka 2010 Novemba, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliingia katika Baraza hili

akilizindua na alitoa hotuba yake, katika hotuba yake kulikuwa na mambo mengi. Miongoni mwa mambo ambayo Mhe. Rais aliyazungumza katika hotuba yake hiyo, ambapo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu, wengi wetu tuliinuka wakati wa kuichangia kwake tukasema kwamba hii ndio dira ambayo tutaiangalia, tutayatekeleza na hatimaye tuone kwamba tumewafanyia mambo wananchi wetu waweze kufikia maendeleo ya kweli.

Mhe. Naibu Spika, moja kati ya mambo aliyoyasema Mhe. Rais ni kuleta mapinduzi ya kilimo au tuseme mageuzi ya kilimo. Alilisema hili kwa uelewa mkubwa kwamba asilimia sabini (70%)_ya wakaazi wa Zanzibar wanaishi kwa kutegemea kilimo, na ndio maana Rais akaona aseme hilo ili kuona kwamba wakulima wanapata fursa ya kuona wanapatiwa mabadiliko ya kweli ili waweze kuzalisha na hatimaye kupata tija, ikiwemo chakula cha kujikidhi na watoto wao, lakini hatimae waweze kuzalisha kwa ajili ya biashara na kuweza kujikimu yale mengine yote ambayo ni mahitaji yanayohitajika kwa mwanadamu yeyote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi wangu huo sasa mimi nianze na mchango wangu wa bajeti hii iliyopo mezani ambayo ndio matumaini ya Wazanzibari kwenye shughuli zetu za kilimo, ambapo tunasema ndio uti wa mgongo wa Taifa letu katika maendeleo ya uchumi pamoja na ustawi wake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa thalathini wa kitabu hiki kuna mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mimi nikiangalia humu katika kitabu hichi ambacho tulisema kwamba kwa miaka ile ya mwanzoni mwa Dkt. Shein nilidhani tutapewa tathmini ya miaka minne ambayo tumekwenda kwenye mapinduzi ya kilimo.

Dhana yangu ilikuwa hiyo, tuelezwe miaka minne yote tathmini yetu ya kwenda kwenye mageuzi ya kilimo ni moja mbili, tatu, nne na hatimaye tuingie sasa kwa kuondokana na bajeti ile iliyokwenda huko na leo tumekuja kwenye mfumo mpya 2015/16 kwamba tunakwenda kwenye *Program Based Budget(PBB)*.

Sasa miaka minne hii na mageuzi ya kilimo tuone basi tumefanikiwa kwa kiasi gani na mapungufu yetu ni yepi, na tukianza sasa kupitia hayo hayo Mapinduzi au mageuzi ya kilimo tunaanza na hii *PBB* tunakwenda vipi.Na matarajio ya kuusema ukurasa huu dhana yangu kubwa ilikuja hivyo.

Lakini kwa bahati mbaya sana hili sikuliona katika kitabu hichi, jambo ambalo nimeliona nami niseme kwamba kuna ukurasa huu wa 43 ambao unaeleza takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa tani kwa mwaka 2014. Nilitarajia nione hapa ni kuona kwamba tangu tumeanza hayo mabadiliko 2011/12, 2012/13, 2013/14 na kuelekea 2015/16 basi nione kwamba hayo mahindi yaliyozalishwa kwamba

tumefikia kiasi hichi, ili haya maneno tuone ni ya kweli, lakini humu nachukua zao moja tu niliseme.

Na zao hilo ndilo lile ambalo Wazanzibari wanalipenda ndio chakula chetu kikubwa ni mpunga, ambao hadi hivi leo kitabu hichi kinaingia humu bado hatujaweza sisi kuumiliki mpunga bila ya kuagizia nje, jambo ambalo haikuwa ndani ya matarajio yetu kwa mujibu wa mabadiliko yale ambayo kwa mujibu wa sera zile ambazo alizisema Dkt. Shein.

Hali hii inaonesha dhahiri kwamba zao la mpunga linaendelea kushuka badala ya kupanda. Mhe. Naibu Spika, imani yangu wakati nikiwa nasikiliza vyema kabisa hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, ambayo ilisomwa kwa niaba alieleza wazi wazi kwamba kuna idara zilizopatiwa asilimia saba tu jambo ambalo ni hatari sana.

Mhe. Waziri wa Fedha angekuwepo, lakini naamini Serikali ipo mbele yangu basi naomba nipate jibu kwamba kwa utaratibu huu wa kwamba zao la mpunga ndio zao pekee ambalo wananchi wanalipenda haswa, ni sababu zipi zilizopelekea kwamba tusiweze kufanikiwa, na ni sababu zipi zilizopelekea kwamba mgao huo ambao unawagusa wananchi moja kwa moja kwenye pembejeo za kilimo zikosekane.

Pia kuna zao jengine la ndizi. Watu wetu wote sasa Zanzibar tumekuwa na mtihani mkubwa wa maradhi ya sukari, watu wetu wanakula ndizi na kuzalishwa kwake ndio kama huku, kama Serikali haikufanya juhudi hii zitaweza kuzalishwa? Maana yake hata hao wagonjwa itaendelea kuwa hali ngumu zaidi, maana tunajua chakula kikubwa kabisa ni ndizi.

Mhe. Naibu Spika, naondoka hapo sasa ninakosogea ni kuuliza hivi, naomba nipewe taarifa katika mradi wa ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao kuhusu ujenzi. Nalisema hili nikiwa najiuliza na kupata shaka, hivi mtu ambaye hana nguo ananunuaje viatu? Wewe huna suti unanunua viatu vizuri na unaviweka *polish* halafu utatembea kweli?Unaweza ukatoka kwa aina hiyo? Hili limefanyika katika taasisi hii, kwamba tumepata vifaa na mashine za usarifu wa mazao lakini jengo hatuna, hili jambo kwa kweli haliendani wala halifanani. Na naiambia Serikali itwambie hasa hivi, hii ni mipango madhubuti inayokubalika tuvae viatu nguo hatuna ndio maana yake, wengi wa Wazanzibari ni wakulima, na matunda mengi yanapatikana hapa kwetu Zanzibar.

Mashine tunazo vifaa tunavyo, jengo hatuna aaa! Mhe. Waziri naomba utakapofika hapa uje unipatie majibu ya kina, kulikoni Serikali ishindwe kusimamia jengo hili kumalizika. Kwa nini unawatia hasara wananchi wa Zanzibar, kumbe uwezo tunao

wa kufanya hili na kuweza kuokoa na wananchi wetu kupata uchumi, kwa nini serikali ishindwe kufanya hili? Tunataka jibu.

Pia kama kuna uzembe uliofanyika ikiwa fedha hizi za wafadhili zinaambiwa kwamba sio za wananchi, mimi nasema za wananchi, kwa maana msaada huu kama si wao usingeletwa, maana yake tuna tabia pesa za wafadhili zinakuwa haziumi sana, lakini nasema hivi hiyo ni mali ya wananchi na lazima tujue hilo, na tuelezwe kwa kina tufahamu, kulikoni hizi fedha? Ni zao lakini Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee na mchango wangu.

Nikitoka hapo kwenye utafiti na mafunzo ya kilimo, Mhe. Naibu Spika, kama kweli tulikuwa tayari kuweza kutekeleza kwa vitendo au kuleta mageuzi ya kilimo, basi tafiti ilikuwa ni suala la mwanzo. Watalimaje wakulima kama hizo mbegu za kulimiwa hazikufanyiwa tafiti ya kweli? Zifanyiwe tafiti, kufanya tafiti mpaka maeneo yao ambayo wanazalisha, je udongo huo mbegu gani hasa inaweza ikastawi na kushamiri na kuweza kuleta tija kwa mkulima huyo ambaye wakati mwengine ni wa kijembe kongoroka, hata hilo trekta halipatikani.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa fedha inaingizwa kwa asilimia nduchu kabisa, halafu tunajisifu tuna mapinduzi ya kilimo, tuna mageuzi ya kilimo, jamani, mumewaangalia hao wakulima kweli mmekwenda kuwaona?

Mimi mwaka jana nilisimama hapa hapa katika meza ya mbele hapo, nilikuja na kusema kwamba Serikali iliwakopa wananchi mbegu Mtwango niambiwe uongo, na hiyo mbegu baada ya kujenga ubia kwao mkawapa utaalamu wakazalisha mlishindwa kuinunua hadi mbegu hiyo inaharibika, nilisema bajeti iliyopita hapa hapa, tena nilimwambia Mhe. Waziri wa Fedha, nilianza naye katika bajeti kuu ya serikali, nikamwambia kawalipe kwanza wakulima bwana halafu ndio uje ulete mengine.

Sasa naomba nipate maelezo, yale maradhi ya matunda tafiti zinasemaje? Tumekabiliwa na matatizo makubwa ya maradhi ya matunda, hebu twambieni kitengo cha tafiti kinasemaje kuhusu haya, jamani na wakulima ndio wanayohitaji hayo wakulima wetu, na ndio wakulima, lakini wao ni wakulima mimi na nyinyi ni watumizi pia tunahitaji. Nielezwe tafiti inasemaje.

Sasa nataka niseme kuna jambo jipya limejitokeza ambalo katika macho yangu mimi nimeliona kama miezi miwili mitatu hivi ugonjwa wa mipapai.

Mapapai yamepata ugonjwa kabisa, maana ilikuwa maradhi mengine ya matunda mengine yana wadudu sasa na mapapai jamani kama utafiti hakuna kweli tuna matumaini ya kwamba tutakuza kilimo chetu na kuleta mabadiliko kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa huzuni na masikitiko makubwa, kwamba kama tafiti hazifanyiki maana yake hakuna kilimo endelevu wala tija kwa wakulima wetu, na wala hatuwezi kubadilisha hali za unyonge kwa kupitia kilimo, huo ndio ukweli.

Na nasema kwamba miaka hii minne ambayo sisi tulikwenda huko na Serikali ikajijengea mikakati, na sheria tutakatengeneza humu kwenye Baraza lako hili Tukufu Mhe. Naibu Spika, ilikuja sheria humu lakini matokeo ya miaka minne hatukuelezwa, na tukaambiwa tumefika hapa na tumegeuza sasa mfumo tunakwenda kwenye *PBB*, maana yake tunauziwa mbuzi kwa mlio sasa hivi kafungwa ukubali kwanza halafu ndio ungoje matokeo.

Tulipokuwa tunaidhinisha na tunaona hakuna matokeo, na leo tumefungiwa kwa mlio tunaambiwa tuje tusubiri matokeo, nani atauliza hatambulikani maana yake sote hatujui kama tutarejea katika Baraza hili, maana yake tukishakupinda zikishafungwa umeidhinisha basi wewe kaa kitako kimya utakuja kuoneshwa kilichofanywa.

Na Mdhibiti na Mkaguzi naye alisema ana matatizo ya wataalamu wa ukaguzi huo, ilisomwa humu humu bajeti ikasema hivyo, sasa tena hakuna Mkaguzi hakuna Mdhibiti, kwa hivyo haya tena za wanyonge kwapani sawa.

Mhe. Naibu Spika, niende sasa kwenye kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kama Serikali ingelikuwa kweli imekubali kwenda katika kilimo cha umwagiliaji maji cha mpunga tungekuwa tumepiga hatua sana. Tusingehitaji kuagizia mchele, watu wetu wamekuwa wafanya biashara wa kwenda hapa kwetu Tanganyika kuchukua na kuleta.

Imani yangu kwa idadi yetu, pamoja na upenzi wetu mkubwa wa ubwabwa, tungemudu kabisa kabisa, na ingefika pahala sisi tungesafirisha mchele, hili linawezekana. Miundo mbinu ni mibovu haiwezi kufikiwa, ukienda kwenye huo umwagiliaji unakuta konde hizi zinasitishwa, hizi nyengine safari hii nyinyi limeni, nimekagua mabondeni jamani nimekwenda.

Na kitabu hichi hichi kimesema kuna baadhi ya maeneo hayakulimwa, kwa hivyo yanathibitisha kauli yangu kwamba kuna sehemu tunaziacha tupu, yaani hazilimwi wanaambiwa nyinyi maji safari hii sio kwenu, kwa hivyo wao hawalimi. Laiti wangepewa fursa na ikatumika vizuri utaratibu huu wa umwagiliaji, imani yangu kwamba tungeweza kuzalisha mpunga wa kutosha na njaa kwa watu wetu ya hii ya zao hili ingelikuwa *alhamdullillah,* sidhani kama kungekuwa na tatizo.

Sasa naomba nije nipewe majibu Mhe. Waziri  ile mbegu yetu ya *kificho* na *nerica* zimekwenda wapi na zikoje na zimekuwaje, uje uniambie hapa Mhe. Waziri,

Serikali itujibu. Mlitwambia na ndio tuliyoanza nayo hiyo mwaka 2010 mwishoni mwaka 2011/12 ilitajwa hii bajeti yake jamani *kificho* na *nerica*, Spika alikuwa anacheka hapo tulikuwa tunaitaja *kificho* na *nerica* akawa ana furaha.

Hebu twambieni ni mbegu moja ambayo ilitajwa inaweza ikalima na ikahimili kukosa maji, kwamba inalimwa juu juu ambapo ilisifiwa mno. Hebu tuelekezeni, jamani huko maweni inakubali na vipi na vipi tena yamekwendea wapi, maweni haikubali tena hii tunasema mje mtupe majibu.

Aidha, kwa nini mnaichukua miradi nusu nusu haifiki mwisho, ukifika pale unakuja mwengine, awamu hii huu au tukiupata ule ule Jamani nasema tena, naomba niseme kwamba *nerica* na *kificho* tupewe taarifa, naamini kwamba wataalamu waliopo juu wana uwezo mkubwa na wana uwezo wa kufanya haya, fursa hatuwapi hawa, tungewapa fursa mabadiliko yangewezekana sana, tumebana mno, wakipanga mipango wataalamu hatukubali kuifuatilia tukifika tunaingiza ya kwetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije hapa kwenye ukurasa wa 36 ambao unazungumzia programu ya uhakika wa chakula na lishe. Hehee, hapa shughuli! Uhakika wa chakula na lishe, mama wajawazito na watoto wasije wakafa, waje wastirike kwenye lishe na chakula.

Mhe. Naibu Spika, unajua hii dhana haikuwa mbaya, na kwa kweli uwepo wa uhakika wa chakula na lishe kwa wananchi ni moja katika msingi mzuri kabisa ambao unasimamia msingi wa haki za binaadam.

Mwanadamu anatakiwa aweze kupata angalau milo mitatu, na mtoto yule wa lishe ni mara tano kwa siku, hii ndio mpango wenyewe wa chakula na lishe. Kwa hivyo mara tano kwa mtoto, na nia kitabu hichi kimesema kwamba kunusuru hawa mama na mtoto pia wametajwa, na nyinyi kinababa kama hamjala mambo hayawi.

Mhe. Naibu Spika, lakini utaratibu ni huo, hebu Serikali ije iniambie hii dhana yetu hasa ya chakula na lishe kwenye ule utaratibu wa maghala, tuna maghala mangapi na tuna kiasi gani hicho cha akiba, naomba nipatiwe jibu, Serikali itwambie ina akiba hasa ya kiasi gani au kama Serikali hamna, mumewaelimisha vipi wananchi wetu namna ya uhifadhi wa mazao yao wanayozalisha wenyewe, ili kama wamezalisha yamezidi waweze kuhifadhi na hatimaye dharura ikitokea mbele waweze kutumia.

Naliomba na hilo nalo mtwambie, taaluma mliyowapa wakulima wetu ambao wakimaliza kulima namna ya uhifadhi, maana nyinyi nadhani hamuna utaratibu wa kuyanunua hayo mazao na hatimaye labda Serikali ikaweza kusimamia na kuona

kwamba inaweka kwenye maghala yake, lakini wao kama wananchi ni taaluma gani ambayo wameweza kupatiwa.

Na Mhe. Naibu Spika, napenda niseme maneno ya kumalizia kwa kuiomba Serikali kwamba, kwa uhakika hasa kuna utaratibu huu wa mwisho kabisa wa programu ya maendeleo ya rasilimali ya misitu na mali zisizorejesheka.

Mimi nataka mnambie mashamba ya Serikali ni mangapi mbali yale ya wananchi yanayohifadhiwa, lakini pia niambiwe mbali na haya ambayo nyinyi mmeyasema mnaotesha miti, mniambie ile miti yetu ya asili ya matunda ile mikubwa mikubwa je, utaratibu wake ni upi wa kusema kwamba ipandwe; tumepoteza mifenesi, misheli sheli, midoriani na miembe ile ya asili ambayo sehemu mbali mbali ilikuwepo ilikatwa na iliathiriwa sana watu wakitumia kwa makaa.

Serikali kwa bahati kwamba haijaweza kwenda kwa asilimia mia moja kuweza kudhibiti ukatwaji wa miti ovyo, na wananchi hawawezi kuacha hili. Wananchi wataacha hili kwa kuwepo mbinu mbadala ya kupata nishati mbadala, wananchi lazima wapike ili wale, watu wa vijijini watatumia kuni, hakutumia kuni atatumia mkaa na bado ni kuni.

Serikali imarisheni nishati ya umeme wananchi waimudu, ili tuondoke huko Serikali lazima iimarishe, wananchi iwafikie huduma ya umeme, itakapowafikia huduma hii ya umeme basi ni kweli kabisa tunaweza kudhibiti haya, watakuwa wana uwezo wa kutumia iwe kwa bei ya chini ambayo wananchi wataimudu, kwa hivyo tutapanda miti yetu itaweza kubakia na kusalimika, lakini unamwambia usikate mti maana yake imekuwa tatizo, imekuwa vile lakini mbinu mbadala ni ipi?

Tumeambiwa kuna makaa ya makaratasi, jamani yale tusidanganyane bado hayajamudu kuenea na watu kuweza kutumia, si kweli! Tuseme tunajaribu kufanya hayo mambo tufikie lakini si kweli kwamba hayo makaa wanaweza kutumia ndio ikawa imekidhi shida yetu ya wananchi. Wananchi wetu bado ni wanyonge; wako vijijini lazima watumie miti kwa kuni ili waweze kupika na kula na kuweza kuishi katika hali ya usalama.

Mhe. Naibu Spika, napenda niambiwe kwamba, je, Serikali ina mbinu gani mbadala sasa ya matumizi ya wananchi ili tuepukane na hiyo kukatwa kwa miti ovyo kwa mpango huu wa 2015/16 na kuendelea huko, lazima Serikali itwambie ili wananchi waweze kuona muelekeo huo kwa wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo na baada ya kugongewa sana, najua muda nao pia umetimia, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Ahsante *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha naomba nisisitize jambo moja muhimu sana. Kesho tukijaaliwa kufika salama tuna matumaini asubuhi baada ya maswali na majibu tupitishe Wizara zetu mbili hizi, sasa kama *quorum* haikutimia, tukisoma Wizara ya tatu itakuwa jambo la aibu sana.

Naomba upande wa Serikali Mawaziri pamoja na *back bencher* kesho tuje mapema ili tuweze kumaliza Wizara mbili na jioni tusome Wizara ya tatu.

Ninachokiomba kila anayekaa na mwenzake wa karibu amueleze, wanadhimu wa vyama C.C.M na *CUF* tuhimizane ili tuweze kwenda kwa utaratibu. *(Makofi)*

Baada ya hayo mjadala wa Wizara ya Kilimo tumeufunga, amebaki mchangiaji mmoja Mhe. Mahmoud atamalizia asubuhi ili baadae tuendelee na utaratibu kama *order paper* itakavyoeleza.

Baada ya hayo naahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 10/06/2015 Saa 3:00 za Asubuhi.

*(Saa 1:46 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 10/06/2015 Saa 3:00 za Asubuhi)*